

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

- 1.Mhe. Kamal Basha Pandu Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
- 2.Mhe. Ali Mzee Ali Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
- 3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
- 4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
- 5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary Kiongozi wa Upinzani/“Waziri Kivuli”–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
- 6.Mhe. Haji Omar Kheri Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
- 7.Mhe. Haji Faki Shaali “Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
- 8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
- 9.Mhe. Hamza Hassan Juma MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.

- 10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
- 11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
- 12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
- 14.Mhe. Samia Suluhu Hassan MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
- 15.Mhe. Burhan Saadat Haji MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
- 16.Mhe. Asha Abdalla Juma MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
- 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
- 18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
- 19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
- 20.Mhe. Zainab Omar Moh'd MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
- 21.Mhe. Idi Pandu Hassan Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25. Mhe. Khamis Jabir Makame Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27. Mhe. Tafana Kassim Mzee Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28. Mhe. Zahra Ali Hamad “Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29. Mhe. Zakiya Omar Juma “Waziri Kivuli”-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30. Mhe. Said Ali Mbarouk “Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31. Mhe. Abdulla Juma Abdulla “Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak “Waziri Kivuli”–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

- 33.Mhe. Hamad Masoud Hamad “Waziri Kivuli”–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
- 34.Mhe. Omar Ali Shehe “Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
- 35.Mhe. Rashid Seif Suleiman “Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
- 36.Mhe. Mohamed Ali Salim “Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
- 37.Mhe. Asaa Othman Hamad “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
- 38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman “Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
- 39.Mhe. Najma Khalfan Juma “Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
- 40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin “Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi Jimbo la Chambani.
- 42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
- 43.Mhe. Ali Abdalla Ali Jimbo la Mfenesini.
- 44.Mhe. Ali Denge Makame Jimbo la Amani.
- 45.Mhe. Ali Haji Ali Jimbo la Mkwajuni.

46.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
49.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
64.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
65Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

66.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
67.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
68. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
69.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
70.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
71.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
72.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
73.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
74.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
75.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
78.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim

Katibu wa Baraza la Wawakilishi.

Kikao cha Saba – Tarehe 28 Januari, 2010

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu hoja inayohusu Mapendekezo ya Uanzishwaji wa Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 69

Ongezeko la Matawi ya Benki Zanzibar

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla sijajibiwa swali langu naomba nifanye marekebisha katika kifungu cha 2 mstari wa 3, badala ya kusema zinatoa riba ndogo, isomeke hazitoi riba ndogo. Baada ya hapo naomba nijibiwe swali langu nambari 69.

Benki nyingi hivi sasa zinafungua matawi yake na kufanya biashara hapa Zanzibar. Pamoja na wingi huo bado benki hizo zinatoa riba ndogo kwa wateja, lakini benki zenyewe zinatoa riba kubwa kwa wateja wao wanaokopa fedha kutoka benki hizo.

- (a) Je, Mhe. Waziri, ongezeko hilo la benki linaashiria nini kiuchumi.
- (b) Kwa nini riba wanazototwa wateja hazipungui, wakati zile wanazopewa wateja hazipandi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako , ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba ongezeko la benki zinazofunguliwa Zanzibar ni kubwa. Hadi kufikia mwezi Disemba 2009, idadi ya mabanki imeongezeka kwa asilimia 50 na kufikia mabanki tisa, ukilinganisha na mabanki 6 yaliyokuwepo kwa kipindi kilichoisha mwezi Disemba 2008.

Mhe. Spika, ongezeko hilo limetokana na benki nyingi zilizoko Tanzania Bara kufungua matawi yake hapa Zanzibar. Ukiacha Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) ambayo makao makuu yake yapo Zanzibar, benki nyingine nane zenye Makao Makuu Tanzania Bara zimefungua matawi yake Zanzibar. Benki zinazofanya biashara Zanzibar ni pamoja na *PBZ, Diamond Trust (T) Limited, Exim Bank (T) Limited, Barclays Bank (T) Limited, Postal Bank, NBC (T) Limited, Kenya Commercial Bank (KCB), FBME Bank na NMB Bank*. Kati ya benki hizi tisa, ni benki mbili tu zina matawi yake huko Pemba. Hizo ni *PBZ* na *NMB*.

Kuongezeka huko kwa uanzishwaji wa mabanki Zanzibar ni kutokana na mazingira bora ya uwekezaji yaliyowekwa na serikali. Pia, usalama na amani kwa nchi. Halikadhalika kuimarishwa kwa miundombinu na mazingira ya uwekezaji kumechangia kwa kiasi kikubwa katika kuongeza utashi wa benki za ndani na kigeni kufungua matawi sehemu mbali mbali nchini, na hivyo, kuboresha huduma kwa wananchi.

Ongezeko la mabanki kwenye uchumi wa Zanzibar linaashiria kukua kwa uchumi wa nchi. Shughuli nyingi katika sekta mbalimbali za uchumi zinapoongezeka huhitaji pia kukua kwa taasisi za fedha zitakazokidhi utoaji wa huduma kulingana na ukuaji huo. Uchumi wa Zanzibar umekuwa ukiongezeka kufuatana na ongezeko la uzalishaji mali na huduma mbalimbali nchini. Kwa mfano mwaka 2000 ukuwaji wa uchumi ulikiwa kwa asilimia 3.6. Katika mwaka 2005, uchumi ulikuwa kwa asilimia 4.9 wakati mwaka 2008 uchumi ulikuwa kwa asilimia 5.4.

Mhe. Spika, ongezeko la mabanki kwenye uchumi wa Zanzibar, linaashiria kukua kwa uchumi wa nchi. Shughuli nyingi katika sekta mbali mbali za uchumi zinapoongezeka huhitaji pia kukua kwa kiasi kwa taasisi za fedha zinazokidhi utoaji wa huduma kulingana na utoaji huo. Uchumi wa Zanzibar Mhe. Spika, umekuwa ukiongezeka kufuatana na ongezeko la uzalishaji mali na huduma mbali mbali nchini.

Kwa mfano mwaka 2000 ukuaji wa uchumi ulikua kwa asilimia 3.6, katika mwaka 2005 uchumi ulikuwa kwa asilimia 4.9 na wakati mwaka 2008 uchumi ulikuwa kwa asilimia 5.4.

Mhe. Spika, ongezeko la matawi mbali mbali ya mabanki Zanzibar, vile vile, linaashiria kukua kwa mwamko wa wananchi katika kutumia huduma za benki. Mwaka 2005 amana zilizotunzwa na benki ziliongezeka kadi kufikia Tsh 104.8 bilioni kutoka Tsh 30.7 bilioni mwaka 2000 ni sawa na asilimia 29.29 la ongezeko la amana.

- b) Mhe. Spika, Kufuatia mabadiliko ya mfumo wa kifedha nchini kuanzia mwaka 1991 serikali imejitoa kabisa katika uthibiti wa moja kwa moja wa shughuli za kibenki nchini ili kuruhusu ushindani huru. Hivyo, viwango vya riba za mikopo yaani (*lending rates*) na riba za amana yaani (*deposit rates*) sasa zinapangwa kwa kutegemea nguvu ya soko yaani (*Market Forces*). Katika kupanga viwango vya riba, mabanki na taasisi za fedha yanazingatia gharama za upatikanaji wa fedha yaani (*cost of funds*), gharama za uendeshaji, riba za dhamana za serikali na sifa alizonazo mkopaji yaani (*Credit worthiness of a borrower*). Mambo yanayopelekea kuwepo kwa riba kubwa ni:
- i) Kukosekana kwa taarifa sahihi za wakopaji na kutokuwepo kwa taasisi ya kuhakiki ukweli wa taarifa za waombaji mikopo yaani (*Credit Reference Bureau*).
 - ii) Kutokuwa na uhakika na usahihi wa mahesabu yanayowasilishwa na waombaji wa mikopo, mabanki hayana namna nyingine ya kupunguza hasara ambayo inaweza kutokea kwa kutumia hesabu ambazo si sahihi na inawalazimu kuweka kiwango kikubwa cha riba.
 - iii) Ukosefu wa amana yaani (*collaterals*) zinazokubalika na kuuzika kwa urahisi, ambapo wakati mwingine inachukua muda mrefu kuuza amana hiyo na kuwa chini ya thamani. Viwango vya riba huzingatia haja ya kufidia hasara hiyo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize kama ifuatavyo. Mhe. Spika, Mhe. Waziri, amekiri kwamba hivi sasa kampuni nyingi zinafungua mabanki hapa kwetu.

- (a) Je, mabanki hayo yanaruhusiwa kufungua kwa mtaji wa kiasi gani.

- (b) Kwa kuwa Benki ya *Greenland* iliwahi kufungua tawi lake Darajani na ikafilisika na kufunga tawi na baadhi ya wateja walikuwa wanaidai. Je, wateja hawa walipata haki zao.
- (c) Kwa kuwa tayari Benki ya *Greenland* ilionesha tatizo. Je, serikali ina mikakati gani ili matatizo kama hayo yasitokee tena.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwanza naomba radhi kwamba Pemba nako hivi karibuni tu kumefunguliwa tawi jipya la *Barclays Bank* pale Chake Chake. Naomba kuongezea katika orodha hiyo.

Mhe. Spika, msimamizi wa mabanki na anayetoa leseni ni Benki Kuu ya Tanzania na wao wameweka benki yoyote ikifunguliwa na kuendesha shughuli zake, basi isipungue na mtaji wa shilingi bilioni tano, hicho ndio kiwango walichoweka.

Mhe. Spika, *Greenland Bank* kwa kweli kadri tunavyokumbuka baada ya kufilisika benki ile na baada ya kufungwa, basi serikali ilichukua dhima kwa kusaidiana na Benki Kuu kuwatafuta wadai wote wa benki ile na walijitokeza na wakalipwa haki zao zote. Kama wako ambao bado wanada, basi namuomba Mhe. Ali Abdalla Ali, atusaidie wajitokeze na tutawafuata wahusika kama wapo. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, miongoni mwa taasisi za kifedha ambazo ziko Zanzibar na kukopesha wananchi ni pamoja na *Blue Bank* ambapo mteja akikopa shilingi milioni 2, basi hutakiwa kulipa milioni 6 kwa mwaka.

- (a) Je, Mhe. Waziri, suala hili analielewa.
- (b) Je, kwa sasa taasisi hii ipo Zanzibar na kama haipo iko wapi.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba huko nyuma kulitokea taasisi moja inayoitwa *Blue Bank*. Mhe. Spika, wao kweli walikuwa wakifanya shughuli za kukopesha na wengi wetu tuliingia katika utaratibu wao wa kukopa na kwa bahati nzuri tukakopesha. Lakini kwa bahati mbaya kukawa kuna matatizo ya ulipaji, lakini wadai walikuja serikalini tukawasaidia na wakapata pesa zao.

Mhe. Spika, nafikiri utaratibu wao na hasa riba zao ulikuwa mgumu kwa watu kukubali kukopa kwao. Nafikiri walikuwa na ujanja mwingi wa kupata pesa kuliko kutoa mikopo. Sasa wenyewe wamekosa biashara na wameondoka hapa Zanzibar.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza naipongeza serikali kwa usimamizi mzuri wa kusimamia vyema maendeleo na mambo mbali mbali kwa ajili ya wananchi wake, hasa tukizingatia kwamba Zanzibar hivi sasa kuna ushindani mkubwa wa kibiashara kuhusu mabanki tisa.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi hiyo Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri, kama ifuatavyo. Kwa kuwa wananchi wetu wa mijini na vijijini, wenye vikundi na mmoja mmoja wanategemea kupata taaluma nzuri ya kupata ukopeshwaji wa pesa kutoka mabanki haya. Je, kwa kuwa wananchi wa mjini wako karibu na benki hizi na vijijini wako mbali, kuna mpango gani au taratibu gani zilizopangwa ili kuwafikia wananchi wa vijijini na kuwapa maelekezo na kupata mahitajio yao ya mikopo na kuendesha maisha yao ya kila siku.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba ni vyema benki hizi zikatoa huduma za mikopo kwa wananchi wetu wengi ambao wako vijijini. Lakini kuna masuala mawili.

Kwanza sisi kama taasisi ya fedha yaani Wizara ya Fedha na Uchumi na mabanki yenyewe tunazidi kuwaelimisha wananchi wetu waache tabia ya kuweka pesa nyingi au hata kidogo katika nyumba zetu. Tutumie fursa ziliopo za kibenki kuweka hizo pesa benki kwa sababu hapo nyuma, nitatoa mfano *PBZ* tulikuwa na matawi mbali ya mjini, tulikuwa na matawi Mkwajuni, Chwaka, Makunduchi na pia nakumbuka kwa Pemba katika Wilaya zote tatu zile tulikuwa na matawi ya benki mpaka Micheweni.

Lakini Mhe. Spika, matawi yale yalikuwa hayana kazi hatimaye matawi yakafungwa na wakarudi, kwa sababu ya kukosa wateja ndio wakarudi na huduma zao wakaziweka mijini. Lakini tunashukuru kukua kwa uchumi na kuimarika kwa miundombinu, sasa hivi watu wengi wanaona ipo haja ya kuweka pesa zao benki. Kwa hivyo, tutazidi kuwaelimisha kwanza watu tujenge tabia ya kuweka pesa zetu benki na sisi kwa upande wetu wa serikali. Pia, tutayahamasisha mabanki hata kupitia magari, *mobile banks* waende vijijini wawafuate wateja badala ya wateja kuwafuata wao. Ahsante.

Nam. 84

Upungufu wa Wafanyakazi Idara ya Ardhi

Mhe. Ali Denge Makame - Aliuliza:-

Je, Mhe. Waziri, Wizara yako inachukua hatua gani kuondokana na upungufu wa wataalamu katika Idara ya Ardhi na Upimaji.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 84 kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, kutokuwepo kwa wataalamu wa kutosha kwenye Idara za Ardhi ni suala lililowazi wala halihitaji mjadala. Ili kazi za idara hizi ziende ipasavyo, Idara ya Upimaji na Mipango Miji kwa Unguja na Pemba inahitaji wataalamu wa upimaji na ramani wenye Shahada ya kwanza na kuendelea kwenye fani hiyo wasiopungua 12.

Aidha Idara hiyo inahitaji wataalamu wa upangaji miji na vijiji (*Town and Country Planners*) kwa idadi hiyo hiyo na wenye kiwango hicho cha utalamu kwenye fani hiyo. Idara ya Ardhi na Usajili inahitaji wataalamu 10 kwa Unguja na Pemba waliohitimu masomo ya Usimamizi wa Ardhi kwenye kiwango cha Shahada ya kwanza au zaidi. Kwa upande wa Idara ya Utawala wa Ardhi wataalamu 6 wa fani ya Usimamizi wa Ardhi wanahitajika.

Mhe. Spika, hali halisi kwa sasa ni kwamba Idara ya Upimaji Miji ina wataalamu 7 wa Upimaji - Unguja na Pemba akiwemo Mkurugenzi wa Idara hiyo. Kwa upande wa wapangaji Mji/Vijijini Idara hiyo ina wataalamu 6 kwa Unguja na Pemba. Idara ya Ardhi na Usajili ina wataalamu wawili Unguja na Pemba pia akiwemo Mkurugenzi mwenyewe. Kwa upande wa Idara ya Utawala wa Ardhi yupo mtaalamu mmoja tu mwenye sifa hiyo.

Mhe. Spika, ardhi ni sekta muhimu sana hasa ukizingatia uchache wa ardhi tuliyonayo. Pengo la wataalamu kwenye sekta hiyo litaleta athari kubwa katika usimamizi bora wa rasimali hiyo muhimu kwa maisha yetu. Wizara imeliona hilo na imekua ikichukua juhudi za kuhakikisha wataalamu wanapatikana kwa sekta hiyo. Hata hivyo, juhudi hizo hugonga ukuta kutokana na kukosa fedha za kusomeshea vijana. Juhudi za hivi karibuni na ambazo zinaelekea kuzaa matunda ni kuzungumza na Serikali ya **Finland** kwa madhumuni ya kuingiza

mpango wa mafunzo kwenye fani na viwango hivyo kwenye awamu ya pili ya Mradi wa Usimamizi wa Ardhi na mazingira (*SMOLE*) unaofadhiliwa kwa pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Finland. Mategemeo ni kupata wataalamu zaidi ya 20 watakaosomeshwa kupitia ufadhili wa mradi huo. Pamoja na juhudi hizo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kupata ufadhili zaidi ili kuwezesha sekta ya ardhi kuwa na wataalamu wa kutosha na katika muda mfupi ujao.

Mhe. Said Ali Mbarouk: Ahsante Mhe.Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, kwa kuwa wizara hii ni wizara ya kiufundi na wataalamu wengi kama walivyosema wenyewe ni wale ambao wamemaliza *degrees* za Chuo Kikuu katika fani ya masomo ya sayansi, ikiwemo hesabu na fizikia. Kwa sababu wanafunzi wengi hivi sasa hawana hamu ya kusoma masomo haya ya sayansi kwa sababu ya matatizo kadhaa, ikiwemo maslahi madogo ya wahandisi na wataalamu wengi serikalini.

Je, wizara yake ina mpango gani wa kuandaa *scheme of service* ya wahandisi na wataalamu wa kiufundi ili kuzuia waliopo wasiondoke na pia kuongeza wengine serikalini.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba vijana wetu wengi ama kwa sababu ya hofu au sijui vipi, hawapendelei sana kusoma masomo haya ya sayansi na hisabati na kwa idara hii masomo haya yana umuhimu wake. Wizara Elimu na Mafunzo ya Amali nataka niseme kwamba sasa hivi inajitahidi sana kuona wanafunzi wanasoma masomo haya ya hesabu na sayansi ili waweze kwenda katika fani hizo.

Mhe. Spika, ni kweli tusipokuwa waangalifu sana si tu katika idara hii na wizara hii, bali tusipokuwa na utaratibu mzuri wa kuwawekea mazingira mazuri, basi wataalamu wetu watatukimbia.

Mhe. Spika, jambo hili tumeliona na kwa upande wa wizara yetu tunajaribu kuweka utaratibu mzuri kwa maslahi ili wataalamu hao tutakapokuwa nao wasiweze kutukimbia.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuongezea majibu mazuri ya mwenzangu Mhe. Tafana Kassim Mzee, Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Kabla sikwenda huko naomba kwa ruhusa yako kwanza uniruhusu nimwamkie Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi Mkoa wa Mjini/Magharibi yupo hapa na wenyeviti wenziwe wa Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Magharibi na wasaidizi wao. Waheshimiwa Shikamooni. (*Vicheko/Makofi*).

Mhe. Spika, pia, kuna rafiki yetu mkubwa sana hapa wa nchi yetu Balozi wa Norway. Mhe. Spika, kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri, kwamba tuna mradi wa usimamizi endelevu wa ardhi na mazingira kwenye wizara yetu ambayo sasa umeingia kwenye awamu ya pili.

Awamu ya mwanzo mradi huo haukuwa na utaratibu wa kusomesha vijana wetu masomo ya Shahada, lakini wengi walifaidika na masomo ya muda mfupi na semina mbali mbali kwa Unguja na Pemba.

Awamu ya pili ya mradi huo, tumezungumza na wafadhili wetu Serikali ya Finland na wako tayari sasa kutusomeshea vijana wetu masomo ya Shahada ili kuziba pengo kubwa tulilokuwa nalo kwenye idara zetu za ardhi. Ninawashukuru sana pia Wakurugenzi wa idara hizo kwa juhudi zao. Ni kweli kwamba mapungufu tunayo na kwenye sekta hii muhimu kwa mustakabali wa uchumi wa nchi yetu, tunapaswa kuongeza jitihada. Tuna tatizo dogo sana tu la ajira ya hao ambao tutawapeleka kusoma.

Lakini tunaandaa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ambayo tuna mashirikiano ya karibu kama tulivyokuwa naye kwenye masuala ya fani ile ya utafutaji na uchimbaji wa gesi asilia, ili kuona namna tunavyoandaa *scheme of service* ambayo itakuwa ni bora zaidi kwa hawa ambao wanaajiriwa katika idara hizi za ardhi na utaratibu wao pia wa kupata ajira na kuendelea na masomo ya Shahada.

Mhe. Spika, nakuomba uniruhusu nimuombe Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, atusaidie kidogo kwenye majibu ya nyongeza ya suala hili. Nafikiri itakuwa ni kwa faida ya Baraza letu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, na mimi nawasalimia viongozi wetu wote waliokuwepo hapa, pamoja na Balozi wetu wa Norway. Mhe. Spika, ameuliza swali zuri sana Mhe. Said Ali Mbarouk, na kanigusa kidogo alipozungumza kwamba hamu imepungua ya usomaji wa masomo ya sayansi.

Mhe. Spika, jana tu nilikuwa kwenye shughuli fulani na nikaeleza hali ilivyo hasa ya somo la hesabu. Nikasema tatizo kubwa la somo la hesabu halifanywi vizuri, inawezekana pengine zamani masomo yalikuwa kidogo kuliko sasa hivi, lakini ule utamaduni wa kuuliza zile *tables*, umeondoka sana katika madarasa yetu mbali mbali, kuanzia *primary* mpaka kuendelea.

Mhe. Spika, sote tunakumbuka hapa kwamba asubuhi ukiingia darasani tu unaulizwa *tables*. *Tables* zilizokuwa rahisi nyengine zinajulikana ukisema saba

mara saba, kila mmoja anaijua, nane mara nane anaijua. Lakini mwalimu analiyekuwa anataka kukupima basi atakuuliza saba mara tisa, kwa sababu kidogo zina matatizo yake. Lakini katika suala hili la kuendeleza sayansi na teknolojia, ndio maana mwaka jana tu tumeanzisha Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Chuo cha Karume katika kuimarisha masomo ya sayansi na ya kiufundi.

Mhe. Spika, nashukuru sana na naomba nichukue nafasi kuwapongeza sana hasa bodi ile ya taasisi ile, wamekuja na mipango mizuri kweli kweli na baada ya miaka miwili au mitatu basi tutaona kuna mabadiliko makubwa kwenye chuo chetu au taasisi yetu ile.

Jengine tumeanzisha madarasa maalum ya sayansi na hata matokeo ambayo tutayatangaza Jumamosi, jana tumetoa kwa muhtasari tu. Kuna madarasa maalum ya sayansi tumefungua pale *Fidel Castro* na hapa Unguja tumefungua vile vile madarasa ya masomo ya sayansi.

Vile vile, kuna madarasa maalum ya wanawake ili waendeleo kuipenda sayansi. Kwa hivyo, tumefungua madarasa yao. Lakini katika suala zima la muundo wa utumishi *scheme of service*, kuna mishahara tuliyopendekeza kwamba walimu wa sayansi basi waangaliwe vizuri zaidi, ili iwe kama ni *incentive* kwa wengine waweze kujiunga na fani hiyo. Mhe.Spika, nakushukuru.

Nam. 40

Magonjwa kwa Wanawake Wenye Watoto Wachanga

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Utafiti uliofanywa na wataalamu wa afya Tanzania unaonesha kuwa zaidi ya asilimia tisini (90%) ya wanawake wenye watoto wachanga nchini wanakabiliwa na hatari ya kupata magonjwa ya mlipuko kwa kuchezea vinyesi bila ya tahadhari za kiafya ikiwemo kunawa kwa sabuni.

- (a) Mhe. Waziri, hali hii kwa Zanzibar ikoje.
- (b) Kama Zanzibar hali ni mbaya inatokana na nini na lipi suluhisho lake.
- (c) Ni aina gani ya vijidudu vinavyopatikana katika vinyesi vya watoto ambavyo vina nafasi kubwa ya kuambukiza maradhi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 40 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, nakubalina na Mhe. Mwakilishi, kwamba ni kweli mwanamke wa Tanzania mwenye watoto ana asilimia kubwa ya kupata maradhi ya mripuko.

- a) Mhe. Spika, kwa upande wa Zanzibar pia inaweza ikawa na asilimia kubwa kama hivyo.
- b) Mhe. Spika, hali hiyo inatokana na mambo yafuatayo:-
 - Malezi na matunzo ya mama kwa watoto.
 - Hali ya mazingira inayokabili jamii yetu katika maeneo anayoishi, ambayo yamezungukwa na vyanzo vya maradhi.
 - Uelewa mdogo wa jamii zetu kuhusiana na taathira zinazoletwa na magonjwa ya mripuko.

Mhe. Spika, suluhisho la hali hiyo ni kutoa taaluma ya afya ya jamii kwa mama wajawazito kabla ya kujifungua na wakati wa malezi ya watoto wetu.

- c) Mhe. Spika, kwa ujumla kuna aina nyingi za vijidudu vinavyopatikana katika vinyesi vya watoto na watu wazima ambavyo vina nafasi kubwa ya kuambukiza maradhi mbali mbali.

Baadhi ya vijidudu hivyo ni:-

- a. *Salmonella* - Husababisha maradhi ya kuharisha na homa za matumbo.
- b. *Vibrio cholera* - Husababisha Kipindupindu.
- c. *Askarias* - Husababisha maradhi ya Safura.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu kimoja. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri, amekiri kwamba Zanzibar pia inawezekana hali ya tukio hili ni kubwa.

Je, kuna mpango gani wa makusudi wa serikali ambao watachukua ili kuwaelimisha wanawake kuchukua hadhari juu ya maambukizo haya ya maradhi ambayo husababishwa na vinyesi vya watoto.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, tahadhari tunayoichukua ni kuwaelimisha hawa akina mama hasa wanapofika katika kliniki zetu, huwa wanaelimishwa pale jinsi ya kujitunza wao wenyewe, jinsi ya kuwatunza watoto na jinsi ya kuchukua tahadhari ya maradhi ya maambukizo ambayo yanaweza kuwaathiri wao wenyewe pamoja na watoto.

Vile vile, huwa tunafanya utaratibu wa kutembelea vijijini kwa ajili ya kupita na kutoa elimu hiyo, pia kuwapa mafunzo yote yanayohitajika katika kujikinga na maradhi hayo.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri, alipotoa maelezo hasa sehemu ya tatu alisema kuwa vijidudu hivi mara nyingi vinasababishwa na hali ya mazingira ya maeneo.

Lakini serikali yetu inayo Idara ya Mazingira, pia kuna Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, tukiangalia baadhi ya maeneo katika masuala ya miundombinu bado haijakamilika ambayo inaweza kuweka mazingira mazuri hasa suala la maji, kwa mfano Kijini.

Je, wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi pamoja na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, atawashauri lini kupeleka maji ili kuepukana na tatizo hilo ambalo limo kwenye suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, ni kweli nilieleza miongoni mwa matatizo yanayosababisha vijidudu hivi kupatikana ni mazingira. Sasa yeye ameshauri kuwa vipi tutaweza kushirikiana na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi.

Mhe. Spika, kwa kweli nataka kumwambia Mhe. Mjumbe, kuwa Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto katika masuala kama haya tunashirikiana kikamilifu kwa ajili ya kuhakikisha watoto wetu pamoja na akinamama wanaishi kwenye mazingira mazuri.

Vile vile, kuhusu suala la kuishauri Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, niseme kwamba serikali kwa makusudi hivi sasa inachukua jitihada ya

kuhakikisha masuala yote au kero zote ama miundombinu yote inayohitajika kwenye nchi yetu yanafanikishwa. Kwa kweli hili halitaki tochi na mambo yanaonekana yanavyokwenda.

Isipokuwa kama kijiji cha Kijini kama hayajafika maji, basi tutashirikiana na Wizara ya Maji kwa ajili ya kuwashauri kwa nguvu zote, ili kuhakikisha kwamba maji yanafika na kuweza kunusuru tatizo hili kuwafika wananchi au wanakijiji. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumsaidia Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kuhusiana na masuala ya maji Jimbo la Matemwe katika kijiji cha Kijini.

Kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Ame Mati Wadi, kwa ustahamilivu wake mkubwa sana, pia niwashukuru wananchi wa jimbo lake kwa kumstahamia yeye pamoja na serikali yao. Kweli ni tatizo la siku nyingi katika Jimbo la Matemwe hasa kijiji hicho ambacho amekitaja Mhe. Mwakilishi. (*Makofi*)

Isipokuwa kuna mipango miwili ya serikali kwa ajili ya kutatua tatizo la maji kwenye jimbo la Mhe. Mwakilishi pamoja na Kaskazini kwa maana ya Nungwi hadi Matemwe.

Mradi mmoja ambao tunakwenda nao hivi sasa *JP5*, maana ya *John Program Five*, ambao unaofadhiliwa na Umoja kwa Mataifa. Hatua ya mwanzo ni kuongeza visima viwili vya kusukumia maji Kiashangwe na tumefikia hatua nzuri. Kwa kweli kisima kimoja tayari kimeshachimbwa na tunaendelea na hatua ya ukamilishaji wa umeme pamoja na mabomba kwa kiasi yameshatandikwa kwa ajili ya kuelekea kwenye kisima hadi tangini.

Vile vile, tunaendelea na hatua ya ukamilishaji wa uchimbaji wa kisima cha pili, lakini kwa bahati mbaya tumepitia katika mtihamu mgumu wa kukosa umeme, kwa maana hiyo kazi hizo zimesita.

Mradi wa pili ni ule ambao unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, ambayo imetoa jumla ya bilioni 65, lengo hasa ni wanawake na watoto. Kwa maana ya msingi wa afya yao pamoja na ustawi wao. (*Makofi*)

Mradi huo hivi sasa umo katika harakati za kutangazia wakandarasi na tunategemea mwaka huu utakuwa umefikia hatua nzuri sasa. Kwa hiyo, pengine katikati au mwisho tutaingia kwenye hatua ya utekelezaji. Mradi huo lengo lake ni kutatua tatizo la maji ambalo amelizungumza Mhe. Mwakilishi, ambao utahusisha maeneo mbali mbali yakiwemo Nungwi hadi Matemwe,

Wilaya ya Kati Unguja, Miji Mkuu ya Pemba na maeneo ya vijijini kwa upande wa Pemba na Unguja. (*Makofi*)

Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo. Duniani kote hivi sasa serikali nyingi zimo kwenye mfumo maalum wa usafishaji mazingira *Ecological Sanitation*.

Je, wao kama wizara wamejishughulisha vipi katika shughuli hii, pia, wamewahi kuhudhuria mikutano yoyote ya kimataifa ambayo inaendeshwa duniani.

- (a) Miradi mingi ya vyoo vilivyojengwa nchini kote inaonekana miradi ile ni vyoo tu havina maji. Sasa kwa afya ya wananchi, yaani watoto, wanawake na zaidi wa wanafunzi wa skuli, wakati wanapokwenda haja iwe kubwa au ndogo na kwa sababu hakuna maji, basi hawanawi hata mikono. Kwa hivyo, hawaoni kwamba bila ya maji vyoo vile vitapelekea watoto kuambukizana maradhi ambayo yanaambukizwa ama kwa kutokunawa au njia nyengine.

Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, nakushukuru. Kwa kweli hakuna usafi bila ya maji, ndio maana nikasema sehemu kubwa ya mradi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika wamelenga huko, skuli za Unguja na Pemba pamoja na vijijini ni misingi hiyo hiyo.

Vile vile, kuwapa mafunzo maalum ya usafi wanafunzi wetu, kuanzia mikono, matumizi ya vyoo au namna ya kutumia vyoo pamoja na kuwapelekea miundombinu muhimu hivi sasa ya kuwa na maji ya kufanya yote hayo. Kwa hivyo, Sekta ya Wizara ya Elimu na vijijini akina mama na watoto kwa misingi ya Sekta ya Afya. (*Makofi*)

Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 64

Matatizo katika Kilimo

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo bado kina mchango muhimu katika uchumi wetu, lakini kimekumbwa na matatizo mbali mbali endelevu, ikiwemo ukosefu wa pembejeo, uchache wa wataalamu na wingi wa wanyama waharibifu.

Je, Mhe. Waziri, wizara yako ina mikakati gani kukabiliana na matatizo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kutambua hayo wizara yangu imekuwa na mikakati mbali mbali endelevu, ili kukabiliana na matatizo tofauti yanayokwamisha maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Miongoni mwa mikakati hiyo ni kubuniwa miradi kwa lengo la kusaidia kuondoa matatizo hayo. Baadhi ya miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

- (i) *MACEMP* kusaidia kuimarisha maendeleo ya ukanda wa pwani na uvuvi kwa ujumla. Kama nilivyosema jana kwamba pia tunajishughulisha na upandaji wa mikoko,
- (ii) *PADEP* kuwawezesha wakulima kwa kuibua miradi na kuwapatia nyenzo,
- (iii) *ASSP/ASDPL* kutoa elimu kwa wakulima na kusaidia nyenzo za kazi za watendaji,
- (iv) *Food Security* kuhakikisha upatikanaji wa nyenzo ambazo zitasaidia uhakika wa chakula katika familia, kwenye mpango wa uzalishaji wa mbegu unaoendelea sasa.

Mhe. Spika, mbali na juhudi hizi vitengo tofauti vilivyomo ndani ya wizara vinaoimarishwa kama vile Kitengo cha Elimu kwa Wakulima kimepewa nyenzo mpya pamoja na kupatiwa wataalamu, Kitengo cha Utibabu wa Mimea, ambacho kina jukumu la uhifadhi na utibabu wa mimea, kupita miradi mbali mbali kimekuwa kikipatiwa nyenzo, kwa mfano uwekazji wa mitego ya kunasia nzi wa matunda.

Pamoja na hayo, kufuatia mpango wa kuwashirikisha wakulima katika ununuzi wa dawa za magugu, kiasi cha madawa kimeongezeka kutoka lita 4,000 mwaka 2007/2008 hadi lita 20,000 mwaka 2008/2009. *(Makofi)*

Mhe. Spika, idadi ya mbolea imeongezeka kwa mwaka ambapo kwa sasa wizara imefikia kununua kiasi cha tani 160 za mbolea badala ya tani 22 zilizonunuliwa mwaka 2006, mbolea hiyo serikali inaiuza kwa bei ya ruzuku.

Aidha kuimarika kwa Chuo cha Kilimo Kizimbani kutasaidia kupatikana kwa wingi wataalamu, ambapo kwa mwaka 2009/2010 chuo kimechukua wanafunzi 89 badala ya lengo la wanafunzi 40. Mipango iko mbioni kuanzisha ngazi ya diploma.

Kwa upande wa matreka mwaka 2007/2008 wizara imenunua matrekta kumi na mbili (12) mapya, mwaka 2009/2010 wizara ina malengo ya kununua matrekta kumi na moja (11) mapya.

Vile vile, hivi sasa wizara imeunda mkakati mpya ujulikanao kama Mageuzi ya Kilimo sambamba na ule wa Tanzania Bara Kilimo Kwanza. Katika mpango huu mkazo zaidi ni kutoa mafunzo kwa wakulima kupitia vikundi vyao na skuli za wakulima juu ya mbinu bora za kuongeza uzalishaji.

Miongoni mwa mbinu hizo ni matumizi ya mbegu bora, mbolea za kilimo pamoja na kulima kwa wakati. Baadhi ya pembejeo kama vile mbolea na mbegu zimefunguzwa bei maradufu, ili wakulima wengi waweze kumudu kununua na kuzitumia. *(Makofi)*

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba niuliza swali kama ifuatavyo.

Pamoja na matrekta ambayo serikali inanunua kwa lengo la kuwasaidia wananchi, lakini bado mwananchi anapochimbuliwa konde yake lazima alipe na anapoburugiwa pia.

- (a) Je, hivi sasa nadhani umefika wakati mwananchi kuburugiwa bure, kwa ajili ya kuendeleza kilimo.
- (b) Hivi sasa wakulima wengi wa mpunga wanapata tatizo la kunguni mgunda, je hilo analijua na kama analijua dawa za kunguni mgunda zipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza naomba nianzie na lile swali la kifungu (b) kuhusu kunguni mgunda. Ninachoelewa kuwa kipindi hiki kilichojitokeza zaidi ni viwavi jeshi na wizara yangu inalifanyia kazi suala hilo, kwa sababu hao ndio maadui wakubwa wa mpunga hivi sasa.

Kifungu (a) mpaka sasa swali lake tunalibeba, lakini wizara au serikali kwa jumla haijatoa taarifa kwamba, wakulima waanze kulimiwa bure, kwa sababu hatuna bajeti ya kuweza kuwalimia bure. Isipokuwa hali itakaporuhusu tunaweza kufanya hivyo, lakini kwa hivi sasa wakulima tutawalimia kwa fedha.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa msimu uliopita baadhi ya wakulima walikosa mavuno mazuri kutokana na ukosefu wa wataalamu pamoja na kuharibika kwa mazao na hivi sasa kilimo cha mpunga ndio kinaanza.

Je, Mhe. Waziri, unao mpango gani wa kuwaandaa wataalamu pamoja na wewe mwenyewe kuwatembelea wananchi hawa, kwa ajili ya kuwapa maelekezo mapema.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza ombi lake tunalipokea. Lakini namuomba kama ninavyomuomba mara zote wakati tunapotembelea katika maeneo ya kule kisiwani Waheshimiwa Wajumbe hatuwapati.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe kupitia kwako Mhe. Spika, wakati tunapotembelea katika maeneo yake basi na yeye tumpate rasmi, ili tuweze kuona yale maeneo ambayo yanayokabiliwa na matatizo zaidi. (*Makofi*)

Kuhusu suala tunao mpango gani katika kuongeza wataalamu. Kwa kweli wataalamu tunao kama nilivyosema mwanzo, yaani tunazo mpaka zile skuli ambazo tayari zinafundisha suala la kilimo. Kwa hivyo, wakulima wanapata kujifunza na wataalamu wetu watazidi kusaidia.

Vile vile, wakati tulipotembelea kule Pemba tuliwataka wataalamu wetu, ili wakulima wetu waweze kuwaamini zaidi, basi kila pahala ambapo wapo wakulima kiasi 60 au 70 na wao waweze kulima, ili wawe mfano mzuri. Hivyo, hilo tutaendelea kulisisitiza na mkazo zaidi wakati tutakapotembelea narejea kusema kwamba, Waheshimiwa Wajumbe wote tuwe tunawapata katika maeneo yao, kwa ajili ya kuondoa haya matatizo.

Kutokana na hali hiyo, isiwe sisi tunatembea na siku ya pili tunaulizwa swali la nyongeza, kuwa eneo fulani hamjatembelea kumbe na Mhe. Mjumbe mwenyewe hakuwepo katika eneo lile.

Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kuniona pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Katika jibu lake wakati alipokuwa akijibu swali la msingi alikubali kwamba wizara inakabiliwa na tatizo la wataalamu.

- (a) Hivi Mhe. Naibu Waziri, anaweza kutuambia hapa Baraza, hii wizara yake inahitaji wataalamu wangapi, ili ikidhi haja ya wataalamu katika nchi yetu.
- (b) Vile vile, anaweza kutuambia Mhe. Waziri, pamoja na elimu kubwa wanayowapa wakulima wetu. Tatizo gani hasa linalowakabili wakulima hawa wakati wanaporejea katika maeneo yao, kwa ajili ya kutekeleza shughuli zao za kilimo. Lakini atakubaliana na mimi kwamba pamoja na atakayoyasema ni gharama kubwa za uzalishaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, kwanza nataka nikubaliane naye katika kifungu (b) kwamba miongoni mwa matatizo yanayowakabili wakulima ni changamoto ya kuwepo kwa hawa wadudu, kwa sababu kila aina ya kilimo basi kunakuwa na maradhi. Pamoja na nilivyojibu na kuwepo kwa matatizo mengi ya wadudu, lakini wataalamu wetu wamekuwa wakiwasaidia sana wakulima, maana yake hawawaachii kwenda peke yao.

Kuhusu wataalamu wangapi ambao wanahitajika na wizara. Kwa kweli kila siku imekuwa ikizaliwa miradi mbali mbali. Kwa hivyo, inapoongezeka miradi basi na wataalamu wanahitajika kuongezeka.

Kutokana na hali hiyo, swali hili tutalichukua na tutamjibu kwa maandishi kwamba wataalamu wangapi wanatakiwa wapatikane, kwa ajili ya kilimo pamoja na shughuli nyengine.

Nam. 100

Utalii Micheweni

Mhe. Ame Ussi Juma – Aliuliza:-

Serikali imeruhusu uwekezaji katika Sekta ya Utalii kwa lengo la kuongeza pato la wananchi na hatimaye kupunguza umasikini. Pamoja na juhudi hizo, Micheweni bado ni miongoni mwa maeneo yenye umasikini mkubwa Zanzibar.

- (a) Mhe. Waziri, unafahamu kwamba wananchi wa Micheweni hawafaidiki sana na utalii uliopo maeneo hayo.
- (b) Kuna sababu zipi zinazopelekea utalii wa maeneo hayo kutowafaidisha wenyeji wa sehemu hiyo.
- (c) Je, wizara imeandaa mikakati ipi ya kuhakikisha kwamba, wananchi wa Micheweni wanakuwa wa mwanzo kufaidika na utalii katika eneo lao.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 100 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba wananchi wa Micheweni hawajafaidika sana na utalii uliopo katika maeneo hayo. Hii ni kutokana na kuwa na ushiriki mdogo wa wananchi wa Micheweni katika Sekta ya Utalii, licha ya kuwa Wilaya ya Micheweni ni moja kati ya Wilaya iliyobarikiwa kuwa na vivutio vingi vya utalii.

Hata hivyo, hali imeanza kubadilika na hasa katika eneo la Makangale, ambalo lipo karibu na Hoteli ya Manta. Kwa kweli hoteli hii sasa imeanza kuwafaidisha wananchi kwa kuwashirikisha kwenye shughuli za maendeleo pamoja na shughuli za michezo.

- (b) Sababu zinazopelekea wananchi wa Micheweni kutoshiriki katika Sekta ya Utalii kikamilifu ni pamoja na hizi zifuatazo:-
 - (i) Muamko hafifu wa wananchi juu ya kufahamu mchango wa Sekta ya Utalii katika kuleta maendeleo kwa jamii na taifa kwa jumla.

- (ii) Ufahamu mbaya juu ya Biashara ya Utalii, yaani imehusishwa kuambatana na maadili yasiyokubalika katika jamii.
- (c) Wizara kwa kushirikiana na sekta nyengine imeona hali hiyo na kwa kushirikiana na taasisi nyengine imechukua hatua zifuatazo:-
- (i) Kuwapatia mafunzo vijana wawili kutoka Micheweni katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii ngazi ya cheti, ili waweze kujiajiri au kuajiriwa kwenye Sekta ya Utalii. Vijana hao tayari wameshatoka chuoni na wanajishughulisha katika sekta hiyo. (*Makofi*)
 - (ii) Wizara imefanya jumla ya semina nne katika Wilaya ya Micheweni kwa lengo la kutoa mafunzo juu ya umuhimu wa utalii kwa maendeleo endelevu. Semina hizo zilizungumzia mchango wa utalii katika maendeleo ya jamii.
 - (iii) Kuendesha mafunzo ya vitendo kwa kutoa fursa kwa wananchi wa Wilaya ya Micheweni, kutembelea maeneo kadhaa Unguja na Pemba yenye vivutio vya utalii na kuona jinsi gani vivutio vya utalii vinaweza kuchangia pato la wananchi kupitia Biashara ya Utalii. Kiasi cha wananchi 60 na wajasiria mali wanane walishiriki katika mafunzo hayo ya vitendo.
 - (iv) Kuanzishwa kwa vikundi viwili vya akinamama katika kijiji cha Makangale chini ya ufadhili wa *MANCEMP*. Vikundi hivyo vinajishughulisha na uzalishaji wa viungo na ushonaji wa vikoi kwa lengo la kuuza katika Sekta ya Utalii.
 - (v) Wizara kwa mara mbili mfululizo mwaka 2008/2009 imeadhimisha Siku ya Utalii Duniani katika Wilaya ya Micheweni. Lengo ni kuamsha ari ya kuenza michezo ya jadi, kama vile mchezo wa ng'ombe na resi za ngalawa. Nia ni kufanya michezo hii kuwa ni vivutio vya watalii na hivyo kuongeza idadi ya vivutio vilioko Wilaya ya Micheweni, kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa sehemu hiyo.

Mwisho Mhe. Spika, ningeomba sana viongozi wa Wilaya ya Micheweni wa vyama vya siasa na serikali wakasaidia na juhudi za wizara katika kubadilisha muamko wa wananchi wa Wilaya ya Micheweni. Hivyo, wakubaliane na sekta hii na watumie yale ambayo yanaendana na maadili yao, basi wayatumie kama vyanzo vyao vya mapato.

Mhe. Ame Ussi Juma: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri.

Wizara imejipanga vipi kuondoa tatizo la umasikini hasa ukizingatia kuwa wananchi wa Micheweni bado wanahitaji kupewa elimu zaidi, ili kukuza huo utalii wenyewe.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, tatizo la umasikini Wilaya ya Micheweni halitoondoshwa na wizara moja peke yake. Hata hivyo, serikali kwa ujumla imeona suala hilo na imeamua kuifanya Micheweni kwamba ni Kijiji cha *Millennium*. Kutokana na hali hiyo, sekta zote zinahitajika kutoa mchango wake katika kijiji kile kwa ajili ya kukuza maendeleo au kuwatoa wananchi wale kwenye unyonge na umasikini.

Isipokuwa kikubwa kilichofanywa cha kuendeleza elimu ni kuanzishwa Radio Jamii, ambayo itakuwa inatoa elimu katika eneo lile kupitia nyanja tofauti za maendeleo ya kijamii, kisiasa pamoja na kiuchumi. (*Makofi*)

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri, wakati alipokuwa akijibu swali lake mama ametueleza kwamba wamechukua juhudi mbali mbali kwa Wilaya ya Micheweni, kwa ajili ya kutoa elimu au taaluma tofauti kama vile mafunzo, semina, mafunzo ya watu 60, vikundi viwili vya akina mama na hata siku ya utalii Duniani ilisherekewa Wilaya ya Micheweni, ili kuhakikisha wanahamasisha kuhusu utalii.

Je, Mhe. Waziri, kwa kuwa bado pahala hapa kuna giza, yaani watu hawajaamka wamelala pamoja na juhudi zote hizo. Hivi kuna hatua gani ya kuridhisha ambayo inaonesha kuwa wito huo wameitikia vizuri, ili kuweza kujikwamua na umasikini huo na kuwa na maisha mazuri.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kufanya masahihisho kidogo kwamba watu wa Micheweni hawakulala. Isipokuwa wanalinda kile wanachokiamini katika mazingira yao kidini na kijamii na wala sio kama wamelala.

Vile vile, kama nilivyosema katika majibu yangu kwamba kufanywa Micheweni kuwa Kijiji cha *Millennium* na kwamba sekta tofauti zitachangia pale, basi zitasaidia kuwapa mwelekeo au muamko wa kimaendeleo wananchi wale.

Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba tusaaidiane kama nilivyosema kwenye jibu mama katika kuwafanya wananchi wetu wa Micheweni kuamka na kwenda kwenye maendeleo ambayo wanatarishiwa, ili kuyapa nguvu na wao wenyewe kuyakubali. (*Makofi*)

Lakini maendeleo sio chumvi kama utaweka leo siku moja na itakolea hapo hapo, isipokuwa itakwenda kidogo kidogo kulingana na mwamko wao kutoka walipo na kuelekea kule wanakotaka kuelekea.

Nam. 24

Vitendea Kazi katika Bandari ya Mkokotoni

Mhe. Haji Mkema Haji – Aliuliza:-

Bandari ya Mkokotoni imeruhusiwa rasmi kufanya shughuli za kibandari. Hivi sasa vyombo vinapakia na kuteremsha bidhaa kupitia bandari hiyo, lakini hakuna vifaa vya kibandari vya kupakilia na kushushia mizigo.

- (a) Mhe. Waziri, kwa nini bandari hiyo haina vitendea kazi vya aina hiyo.
- (b) Je, kwa nini bandari hiyo inatumika kwa kuteremsha abiria, lakini hairuhusu kupakia abiria.
- (c) Je, wizara ina mpango gani wa kujenga banda la abiria ambalo kwa sasa halipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia kuwa wazima na kuweza kuhudhuria kikao cha Baraza na kuweza kutekeleza majukumu ambayo tumepangiwa.

Kwa ruhusu yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Na. 24 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) kweli kuwa Bandari ya Mkokotoni imeruhusiwa rasmi kufanya shughuli za kibandari kwa mujibu wa sheria. Wizara yangu kupitia

Shirika la Bandari inao wajibu wa kuiendesha na kuendeleza bandari hiyo kama zilivyo bandari nyengine za Zanzibari.

Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari inao mpango gati ndogo (*Jetty*), kwa ajili ya kuhudumia vyombo vya abiria wanaovuka na kwenda kisiwa cha Tumbatu. Mpango huo umeingizwa kwenye bajeti ya miaka mitatu ya shirika na utaendelezwa mara tu pale hali ya fedha itakaporuhusu. Uwekaji wa vitendea kazi vya bandari kutafuata mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa *Jetty* hiyo.

- (b) Bandari ya Mkokotoni inatumiwa na vyombo vya kienyeji, vikiwemo majahazi, mashua na maboti madogo. Hivyo, hivi sasa hakuna chombo chochote cha abiria kutoka nje ya Zanzibar kinachotumia bandari hiyo ambacho kina leseni ya kuchukua abiria. Kwa hivyo, vyombo vyote vinavyotumia Bandari ya Mkokotoni kisheria haviruhusiwi kubeba abiria.

Isipokuwa vyombo vinavyoingia bandarini hapo kutoka Tanga ni vile vya mizigo tu. Lakini baadhi ya vyombo hivyo huchukua abiria kutoka bandari zisizo rasmi huko Tanga kinyume na sheria. Wakati vyombo kama hivyo vinapofika Bandarini Mkokotoni vikiwa na abiria, basi inakuwa vigumu kuvirejesha vinakotoka na badala yake wizara yangu kupitia Shirika la Bandari hutoa taarifa kwa vyombo vya usalama hapo Mkokotoni, ili hatua za kufaa zichukuliwe.

Kwa hivi sasa wizara yangu haina mpango wa kujenga jengo la abiria katika Bandari ya Mkokotoni hadi hapo tutakapofanya marekebisho ya kujenga gati.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, bandari ni sehemu ya kutoa huduma kwa mizigo na abiria. Hivyo, Bandari ya Mkokotoni abiria muhimu wale wanaotokea Tumbatu, yaani wao wanalazimika waje ng'ambo Mkokotoni, kwa ajili ya huduma za kiutawala pamoja na kilimo.

- (a) Je, kwa nini bado hawajaimarisha bandari hiyo, ili hawa wananchi wa Tumbatu wakaweza kuteremka na kupanda pale vyombo vyao katika hali ya usalama kwenye karne hii ya 22.

- (b) Bandari hiyo ipo karibu na Afisi ya Mkuu wa Mkoa. Kwa kweli Mkuu wa Mkoa hana raha ya kufanyakazi kutokana na zogo la wachukuzi pia kuna Mahakama ya Wilaya. Je, Mhe. Waziri, haoni hivi sasa kuna haja ya jengo lile wakachukua wao Shirika la Bandari na kumjengea Mkuu wa Mkoa nyumba nyengine, ambapo ataweza kufanyakazi kwa nafasi pamoja na Mahakama, ili Hakimku awe na nafasi kusikiliza kesi vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza Mhe. Mwakilishi anataka aelewe kuwa bandari ya Mkokotoni kwa usafiri wa Tumbatu inakidhi haja hivi sasa isipokuwa kinachotakiwa ni kujenga hiyo *jetty* ili kuboreka zaidi.

Mhe. Spika, ni kwamba nataka akumbuke Mhe. Mwakilishi, kwamba Afisi ya Mkoa sasa hivi inajengwa katika Chuo cha Amali na ya kisasa zaidi na itakuwa na Afisi mbali mbali. Kwa hivyo, naomba kama hajatembelea huko atembelee ataona maendeleo yaliyofanywa na Mkoa wa Kaskazini – Uguja.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, katika jibu lake mama alisema kuwa katika gati ile sio sheria. Kwa kuwa Mheshimiwa ameshakiri kwamba sio sheria kwa vyombo kushusha abiria pale.

Je, vyombo vingapi vimefikishwa mbele ya sheria.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, katika jibu mama Mhe. Naibu Waziri, amesema kwamba sisi wajibu wetu ni kwamba chombo kikija na abiria tunawaita taasisi husika ambazo zinahusika na usalama wa wananchi. Kwa hivyo, sisi tunawakabidhi wao ili wafuate taratibu zinazotakiwa.

Mhe. Spika, wajibu wetu mkubwa ni kushughulikia mizigo katika bandari ya Mkokotoni. Kwa mfano mwaka uliopita tumepokea karibu vyombo 464 na tuliondoa vyombo karibu 439 na kuingiza mzigo na kutoa karibu tani 667. Pia, shirika limejiingiza mapato karibu ya shilingi milioni 4.4.

Mhe. Spika, kwa upande wa taratibu kwa sababu kuingiza abiria kuna taratibu nyingi sana, lakini sisi bado hatujaruhusu kwamba bandari ya Mkokotoni kutumika rasmi, kuingiza na kutoa abiria isipokuwa abiria wa kisiwa cha Tumbatu ambao wana haki safi ya kushuka katika bandari ya Mkokotoni.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, nimefarajika sana kusikia kwamba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi itajenga *jetty* katika bandari ya Mkokotoni ili kupunguza tatizo. Lakini mimi ningependa kumuuliza Mhe. Waziri, kuwa ni lini *jetty* hiyo itajengwa na kama itajengwa hivi karibuni je, tayari michoro imeshatengenezwa. Kama imekwishatengenezwa lini nitaiona michoro hiyo ili niamini ndani ya nafsi yangu kwamba hiyo nia ipo.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba bandari ya Mkokotoni ni pana sana na yako maeneo maalum ambayo yatachukuliwa kama bandari. Je, mipaka ya bandari hiyo inajulikana kwa Mkoa wa Kusini imemalizia wapi, Kaskazini wapi na uchejua ni wapi katika mipaka ya bandari ya Mkokotoni.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, katika adhema na mipango kazi ya Shirika la Bandari, lengo la kwanza ni kujenga *jetty* katika kisiwa cha Tumbatu katika eneo la Gombani, ndiko ambako tutaanza kujenga *jetty* hiyo ili kuwasaidia wananchi wa Tumbatu kwa sababu kutoka kule kuja Mkokotoni ni tatizo kubwa kuliko Mkokotoni kwenda Tumbatu.

Mhe. Spika, la pili kuhusu mipaka ya bandari hapa siwezi kumwambia Kaskazini imefika wapi, maana yake hata hiyo Kaskazini wenyewe nitakuwa sijui imeelekea wapi na Kusini wapi. Lakini Shirika la Bandari imeshajiandaa kwa bandari zetu zote tumeshirikiana vizuri na Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kuweka mipaka ya bandari zetu kuanzia bandari kuu ya Malindi na bandari nyengine. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi, jambo hili akaturuhusu Mhe. Spika, tunaweza tukakuletea baadae kwamba mipaka ya bandari ya Mkokotoni ikoje, lakini tuna mashirikiano mazuri na watu wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi katika uwekaji wa mipaka ya bandari.

Nam. 13

Matengenezo ya MV. Maendeleo

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:-

Shirika la Meli Zanzibar limeipeleka Meli ya MV. Maendeleo Chelezoni Mombasa Kenya miezi kadhaa iliyopita, lakini hadi leo meli hiyo haijarudi kutoka huko Mombasa.

(a) Mhe. Waziri, ni tatizo gani linaloikabili meli hiyo hadi leo.

(b) Ni kiasi gani cha fedha kinachohitajika katika matengenezo ya meli hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 13 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Ni kweli kuwa Meli ya MV. Maendeleo imepelekwa Mombasa kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo na hadi sasa haijarudi kutokana na kuwa meli hiyo imo katika kumaliziwa matengenezo madogo madogo. Aidha, wizara yangu kupitia Shirika la Meli Zanzibar linafanya matayarisho ya kumpeleka mkaguzi (*Surveyor*) kwenda kuifanyia ukaguzi meli hiyo kutokana na matengenezo yaliyofanywa. Jumla ya *USD* 240.000 zilitumika katika matengenezo hayo, gharama hizi zilijumuisha pamoja na uingizaji wa vifaa (*Spear parts*) za meli hiyo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Mwakilishi, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, visiwa vyetu vya Unguja na Pemba tunategemea kuwa na meli madhubuti hasa meli ya serikali na sababu ya msingi ni kwamba meli hiyo iwe ni meli itakayoweza kuchukua karafuu, watu siku za sherehe na mambo mbali mbali, tuwe na chombo cha uhakika kwa ajili ya watu wetu.

Lakini meli hii hivi sasa pamoja na matengenezo makubwa ya *USD* 240.000 sio nyingi kwa matengenezo ya meli, lakini sio kidogo. Hivyo, wizara kwa makusudi kupitia Shirika la Meli lina mpango gani wa kutafuta meli ya uhakika ili meli hii tuliyokuwa nayo na meli ya MV. Mapinduzi zikauzwa ili kupata meli moja ya uhakika kwa ajili ya huduma za Wazanzibari.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, kwanza ni kweli kuwa na meli mpya ni vizuri, lakini hali inakuwa ni ngumu. Mhe. Spika, meli hii ya MV. Maendeleo kwa kawaida sisi meli zetu tunatengeneza katika *Africa Marine*, lakini kwa bahati mbaya katika kipindi hiki kulikuwa kuna matatizo katika uongozi na *Management* ya *Africa Marine* kulikuwa kuna kama ususiaji wa kazi. Kwa hivyo, meli yetu tuliipeleka katika Kampuni ya *SECCO* wameitengeneza na kwa kazi ambayo tumewapa wao karibu imemalizika.

Walihitaji walipwe fedha zao zile wamalizie ili wairuhusu meli na wameshapelekewa nafikiri kama *USD* 50,000 na wameiruhusu. Hivi sasa meli hiyo tunaipoleka kwenye Chelezo chengine cha *Africa Marine* kwenda kupara mwani na kutia rangi kwenye *botton plate*, ikimaliza hapo meli itakuwa tayari

kuja Zanzibar. Mhe. Spika, bahati nzuri wewe mwenyewe uliruhusu ujumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenda Mombasa kuikagua na ripoti yao nimeiona wameridhika na kazi ambayo imefanywa.

Mhe. Spika, kuhusu mpango gani wa serikali wa kuziua meli ya MV. Mapinduzi na MV. Maendeleo na kununua meli mpya. Mhe. Spika, ni kwamba serikali inajitahidi sana na inafanya kila linalowezekana kuziua meli hizi. Tumekusudia kuziua kwa awamu, hivi sasa meli ya MV. Mapinduzi iko sokoni inauzwa.

Siku ile Waheshimiwa wengine walitushauri kwamba tuuze meli tu tusiueze jina, lakini tunaiua leo baadae nitazungumza na Waziri wa Fedha kwa sababu kuna habari njema katika mwenendo wa kuitafutia soko meli hii, lakini bado serikali inaendelea kutafuta mbinu ya kupata meli nyengine ili iweze kutoa huduma kwa wananchi. Kwa sababu tunajua kwamba Zanzibar ni nchi ya visiwa na bila ya kuwa na meli ya uhakika wananchi wetu watapata tabu sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru ni kwamba tunavyoelewa meli hiyo iko chini ya mkataba na Kampuni ya *Hamid Distributors*, ninachotaka kujua ni nani aliyehusika kupeleka meli hiyo Chelezoni ni Shirika la Meli au ni kampuni.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, mkataba wa Shirika la Meli na *Hamid Distributors* umemalizika na meli hii imepelekwa na Shirika la Meli lenyewe kwa fedha zao wenyewe hawakupewa ruzuku, lakini ikirudi baada ya matengenezo uongozi na Bodi ya Shirika la Meli watakaa kuangalia wafanye nini katika uendeshaji wa meli hii.

Nam. 46

Kukua kwa Kiwango cha Mpira wa Miguu Zanzibar

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Sababu moja inayochangia kukua kwa viwango vya mpira wa miguu kwa timu na mataifa mbali mbali duniani ni upendo na ushirikiano wa wadau mbali mbali wa mchezo huo. Ili kufikia malengo hayo nidhamu kwa wachezaji, vilabu na hata waamuzi ni muhimu na kwamba suala la adhabu kali kama kuwafungia wachezaji na wahusika wengine wa mchezo huo kwa muda mrefu halina nafasi ulimwenguni.

(a) Ikiwa Zanzibar ni sehemu ya dunia, suala hili tunaliangalia vipi.

- (b) Ni sababu zipi za msingi zilizosababisha makocha Ali Bushiri na Seif Bausi kufungiwa muda usiopungua miaka mitano.
- (c) Kwa kuwa Rais wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo wa Zanzibar pamoja wa wadau wengine wa michezo walikemea sana tabia za *TFF* na *ZFA* kuwa na maamuzi ya jazba pale wanapotoa adhabu hususan kwa makocha na wachezaji. Kwa sasa kauli ya Serikali juu ya tabia hiyo ni ipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 46 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa katika swali la msingi alilouliza Mhe. Mwakilishi naomba nimjibu kwamba adhabu hizo hazina nafasi ulimwenguni hivi sasa kwa sababu tayari indhari na matokeo mbali mbali ya adhabu kwa muda uliopita yameshaweza kuweka sawa mengi miongoni mwa wachezaji, waamuzi na makocha.

Mhe. Spika, mizizi imara ya mchezo wa mpira inatokana na nidhamu mchezoni. Nidhamu inahitajika kwa wachezaji, walimu, waamuzi pamoja na wapenzi wa mchezo kwa jumla. Kwa kuwa mchezo wa mpira hapa nchini haujawa wa kulipwa, yaani "*Full Professional*". Hata hivyo, bado wachezaji, viongozi, waamuzi na wananchi wanapaswa kufuata Sheria za *FIFA* kwani malengo yetu ni kuelekea huko kwenye *professional football* na pia kushiriki mashindano mbali mbali ya kimataifa ambayo hivi sasa tayari tunafanya hivyo. Hiyo itasaidia pia kutunza nidhamu za mchezo huu ambao ni maarufu hapa nchini.

Mhe. Spika, wizara na taasisi husika zitaendelea kutoa taaluma kwa wadau wote ili kurudisha hali ya nidhamu nchini mwetu hususan katika mchezo wa mpira wa miguu hapa nchini na katika viwanja vyote vinavyochezwa mjini na njje ya mjini.

- (a) Mhe. Spika, ni kweli Zanzibar ni sehemu ya dunia na suala la nidhamu mchezoni linaangaliwa kwa upeo mkubwa hapa nchini kwani limo kwenye kanuni zetu za kuendesha mashindano ya mchezo wa mpira wa miguu zinazolindwa na sheria zake na adhabu hutolewa pale panapohusika.
- (b) Mhe. Spika, naomba nimkatalie Mhe. Mwakilishi na pia niliombe Baraza lako tukufu wakati tunauliza maswali tuwe makini kuwataja

majina kwa sababu hao tunaowataja majina wengine hawana nafasi ya kuja kujitetea hapa na wakati swali linaulizwa huwa kama ameshapewa ile adhabu wakati sio kweli.

Mhe. Spika, kocha Ali Bushiri hajawahi kufungiwa kufundisha mpira hapa nchini. Kocha Ali Bushiri amefungiwa na *CECafa* na kufungiwa kwake kumemkataza kushiriki kama kocha au kiongozi kwenye mashindano yanayosimamiwa na kuendeshwa na *CECafa*. Kocha aliyetajwa katika swali ni kocha Seif Bausi naye huyu hajafungiwa na *ZFA*, kwani hajafanya utovu wa nidhamu wowote kama kocha wa mpira wa miguu hapa Zanzibar.

Hivi sasa Seif Bausi anafundisha timu ya Malindi ya Zanzibar, lakini kwa kuliweka sawa hili, nadhani Mhe. Mwakilishi alikusudia kocha Salum Bausi aliwahi kufungiwa na *ZFA* na kifungo chake kilikuwa mpaka *league* ya Zanzibar itakapomalizika na faini ya shilingi 200,000 na alifungiwa siku ya mechi ya JKU na Miembeni walipocheza wakati yeye akiwa kocha wa JKU na Miembeni kushinda siku hiyo mabao mawili kwa moja.

Mhe. Spika, kocha huyu hivi sasa anafundisha timu ya *Oceans View* hapa Zanzibar na tayari faini ile ameshalipiwa na kwa msimu ule uliopita wa *league*. Kwa hivyo, Seif Bausi hana kosa lolote wala hakuwahi kufungiwa.

- (c) Mhe. Spika, adhabu zote zinazotolewa na *ZFA* zinatokana na Kanuni za kuendesha mchezo wa mpira hapa nchini na hazitolewi kwa maamuzi ya jazba. Mhe. Spika, kwa sasa serikali itaishauri *ZFA* kuzipitia kanuni zake pamoja na kuhusiana na sheria za nchi pale wanapohusika washabiki moja kwa moja ili ziendane na maendeleo ya mchezo wa mpira wa miguu duniani na kuzingatia zile kanuni mpya za *FIFA* kila tunapotelewa.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika michezo mingi duniani inayopendwa moja wapo ni mpira wa miguu na mchezo huu hivi sasa umekuwa mali na vijana wetu wengi wamepata ajira katika nchi yetu au nje ya nchi. Pia, tunao wachezaji wengi kutoka vilabu mbali hapa Tanzania kwa mfano Timu ya Simba, Yanga, Mtibwa, Maji Maji na wengineo.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba tatizo letu la kinidhamu ni tatizo ambalo linarudisha nyuma wachezaji wetu wa Zanzibar kuongeza vipaji vyao hasa

tukilinganisha kwamba waamuzi ndio chanzo cha matatizo na ndio chanzo cha kushusha kiwango hapa kwetu Zanzibar.

- a) Je, wizara kupitia Baraza la Michezo na *ZFA* limejipanga vipi kuhakikisha kwamba waamuzi wanapatiwa taaluma nzuri ya kutokunyooosha mkono kwa njia ya uhadaa ili kutoa kauli thabiti katika mashindano ya mechi zozote wanazochezesha.
- b) Kwa kuwa Kocha Ali Bushiri amefungiwa na Shirikisho la Soka la Afrika ya Mashariki na Kati (*CECAFA*) na kwa kuwa Chama cha Soka cha Zanzibar ni mwanachama halali wa Shirikisho hilo. Hivyo, chama chetu hiki cha Soka cha Zanzibar kimechukua hatua gani angalau ya kumuomba msamaha ili kocha huyo aachiwe kushiriki katika mashindano hayo ya Afrika Mashariki.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwa bahati nzuri Mhe. Mwakilishi ni mwanamichezo maarufu hapa Zanzibar na pia ni mshabiki wa hizo timu alizozitaja hususan Timu ya Simba pia ni Mjumbe wa Baraza letu la Michezo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, tumeligundua hilo na tumelifanyia utafiti wa kutosha, lakini pia kulikuwa na makosa yanafanyika wakati pale marifarii wanapoachwa kwenye maposho yao ya mechi ndipo unaleta mwanya wa mambo mengine kupenya katikati. Kwa hivyo, hilo limezingatiwa na hivi sasa kuna kanuni zimewekwa za refarii kucheza michezo hiyo na viwango vyao vya maposho vimeongezeka na hilo tutalihakikisha na sasa hivi kuna utafiti ambao unafanyika katika hili Kombe la Marehemu Mzee Thabit Kombo ambalo linaendelea hivi sasa ni kwamba marifarii wameekewa viwango vyao maalum na mpaka sasa bado hakujatokea malalamiko yoyote.

Kwa hivyo, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kweli kulikuwa kuna kasoro na tumezifanyia utafiti na hivi sasa kutokana na huo mpango nilioutaja, basi naweza kusema tayari hizo kasoro zimeshaanza kupungua.

Mhe. Spika, pia ameuliza kuhusiana na sheria za *CECAFA* na kwa kuwa *ZFA* ni mjumbe halali wa *CECAFA*, lakini katika sheria za *CECAFA* wakishatoa uamuzi ni vigumu sana kuomba msamaha ukakubaliwa lazima uamuzi ule uliotolewa ufuatwe. Lakini tunashukuru sana kwenye masuala ya faini inapotolewa kwa timu pale huwa tunakaa nao na kukubaliana watupunguzie kwa zile faini. Lakini kwa sheria hii ya kumzuia, basi kwa kweli ni ngumu sana wao mara nyingi wanakataa na kwa kuwa amezuiliwa kwenye mechi za

CECFA tu sio katika timu zetu hapa nchini, basi tumeona tusilisukume sana aendelee kufanya kazi yake hapa, lakini pangelikwa na faini, basi tungeomba afueni hizo faini tupunguziwe.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, wenzetu Tanzania Bara Kocha Maximo huwa anafuatilia *league* na kuchagua wachezaji wa kimataifa na kuunda timu ya taifa.

Je, huyu kocha wetu Mmisri simuoni kufuatilia *league* hizo zinazochezwa, je, hawa wachezaji wao huwapataje wa timu ya taifa ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli wenzetu katika timu ya taifa ya Tanzania Bara, kocha wao hupata nafasi ya kuwapeleka sehemu mbali mbali, lakini na sisi tunashukuru pia Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutupatia nafasi kama hizo. Nakumbuka Kocha Maximo alikwishawahi kuipeleka timu ya taifa katika nchi za Denmark, Sweden pamoja na kule nchini kwake Brazil. Kwa hii timu yetu ya hapa Zanzibar pia imeshabahatika mara kadhaa kwenda Ujerumani, Misri pamoja na nchi nyenginezo ambazo hualikwa na marafiki wa huko kwa kushirikiana na bajeti ambayo inatoka serikalini.

Mhe. Spika, chakufanya hivi sasa kwa kuwa tumepata kocha mpya tayari kocha huyu ameshaanza kuitayarisha safari maalum ya timu yetu ya taifa ambayo atafuatana nayo kwenda Misri na hivi sasa ameazimwa na timu ya Miembeni kwa ajili ya mashindano ya huko huko nchini Misri ambapo itacheza na timu ya Petro Jety baada ya kuja hapa Tanzania. Kwa hivyo, hilo linaendelea namuomba Mhe. Mwakilishi atukubalie kwamba jitihada zaidi zitaongezeka hapo baadae.

Nam. 63

Uwekezaji katika Elimu

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

- (a) Je, Mhe. Waziri, vigezo gani vinatumia kuruhusu mwekezaji kuanzisha skuli ya binafsi.
- (b) Ni mtaji kiasi gani unaohitajika kuwekeza katika elimu kwa kuanzisha skuli.

- (c) Kwa nini wawekezaji binafsi wanaruhusiwa kuanzisha skuli zenye majengo duni ambazo hazina hadhi ya kuitwa skuli, zikiwemo nyumba zilizokusudiwa kutumika kwa makaazi ya kifamilia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- a) Mhe. Spika, vigezo vinavyotumiwa kumruhusu mwekezaji kuanzisha skuli binafsi ni kuwa na jengo ambalo lina nafasi ya kutosha kwa shughuli za kiskuli au kuwa na hati ya kumiliki eneo la kujenga skuli, kuwa na walimu wenye sifa za kielimu na maadili, kuwa tayari kuweka viwango vya ada ambavyo vitakubaliwa na Wizara ya Elimu na kuwa tayari kufundisha kwa kufuata mitaala inayoruhusiwa na Wizara ya Elimu.
- b) Mhe. Spika, kiwango cha mtaji wa kuanzisha skuli kinatofautiana kutegemea aina na ukubwa wa skuli inayoanzishwa.
- c) Mhe. Spika, ni kweli kwamba baadhi ya skuli za binafsi hasa za maandalizi zimeanzishwa katika majengo ya nyumba za kuishi. Skuli hizi zimepewa vibali vya muda na vinaweza kuamriwa kufungwa mara moja kama mazingira ya maeneo wanayofundishia yataonekana hayaridhishi na yanahatarisha maisha ya wanafunzi na walimu. Mhe. Spika, hata hivyo, baadhi ya skuli hizo zimeweza kujiimarisha kwa kuhamia maeneo mengine baada ya kuanzisha majengo yake ya kudumu. Katika siku za karibuni, kumekuwa na ongezeko la ujenzi wa skuli za binafsi zenye majengo ya kisasa ambayo yamevutia wanafunzi wengi kujiunga na skuli hizo. Ni azma ya wizara kuona kwamba skuli hazipatiwi usajili wa kudumu mpaka hapo zitakapokuwa na majengo yanayofikia viwango vinavyokubalika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri, amekiri kwamba katika skuli zinazofunguliwa zina tofauti kiuwezo. Je, katika skuli za serikali huwa kuna wakaguzi maalum kupita kuangalia maendeleo ya wanafunzi na ya walimu kwa ujumla.

- a) Je, katika skuli hizi za watu binafsi uko utaratibu huo.

- b) Kwa kuwa skuli zina tofauti kiuwezo kiwanafunzi, kimajengo na kimapato kwa mfano Skuli ya *High View* na *Laurent*, pia skuli za chini kama Mbarali na Chuwini Sekondari ya *private*. Je, kwa nini hawa wote wanakatishwa leseni ya aina moja wakati uwezo ni tofauti.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama alivyoeleza kwamba katika skuli za serikali kuna wakaguzi ambao wanapitia skuli hizo na kuona maendeleo ya skuli pamoja na mwenendo mzima wa uendeshaji wa skuli. Katika skuli za binafsi pia kuna utaratibu kama huo wakaguzi wetu huwa wanapitia mara kwa mara ndio maana kwamba skuli haiwezi kupata kibali kama haijakaguliwa na kuridhisha kwamba imefuata vigezo vinavyotakiwa.

Mhe. Spika, pia ni kwamba skuli inatozwa leseni kutegemeana na aina ya skuli ambayo inaanzishwa kama ni sekondari au *primary*.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba niongeze kidogo tu kuhusu suala la wakaguzi katika skuli za binafsi.

Mhe. Spika, hili tunaliangalia kwa makini sana na labda mmeshasikia Waheshimiwa Wajumbe kwamba ripoti za ukaguzi pamoja na matokeo mbali mbali yanayotokea katika skuli ya binafsi ya *Stanet* ni kwamba tumeshatoa hati rasmi kwamba ile skuli kuanzia tarehe 1 Januari, 2010 itakuwa imefutwa.

Tumeifuta kutokana na matokeo mbali mbali yaliyotendeka huku nyuma, lakini pia, tumegundua kwamba aina ya majengo ambayo walikuwa wanatumia si ya kawaida (yaani ni nyumba za kuishi). Kwa hivyo, tumechukua uamuzi huo na mwenye mamlaka ya kufanya hivyo sio waziri ni Baraza la Elimu ambalo Mwenyekiti wake ndiye anayetia saini hati ile na kuipeleka kwenye vyombo vinavyohusika.

Mhe. Spika, napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi, kwamba leseni hupewa walimu na skuli huwa zinafanyiwa *registration*. Kwa hivyo, huwa wanapata hati ya usajili, lakini leseni walimu wote ambao wamekidhi mahitaji ya kusomea na wamefikia viwango huwa tunawapa leseni zao.

Mhe. Mohamed Ali Salim: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri, swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri, ametoa mfano wa skuli iliyokaguliwa na kuonekana matatizo yake.

- a) Je, ukaguzi huu uliofanywa katika skuli hiyo ya binafsi na yakaonekana matatizo ulikuwa ni ukaguzi wa kawaida tu unaopangwa au ulikuwa ni ukaguzi uliopangwa kutokana na haja maalum.
- b) Mhe. Spika, skuli nyingi za binafsi zinapoanzishwa huanza vizuri zikatoa matokeo mazuri, lakini baada ya muda kuendelea huanza kuporomoka matokeo yake. Ni sababu zipi za msingi zinazopelekea skuli hizi kwenda katika mwendo huo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, skuli hii na nyenginezo ukishapanga utaratibu wako wa ukaguzi wa kawaida, lakini inapotokea haja ndipo pale ambapo tunapeleka wakaguzi maalum. Nashukuru sana kwamba masuala haya ya Skuli ya *Stanet* katika Baraza hili tukufu lilijadiliwa sana, kutokana na hilo tukafikia hatua ya kupeleka kamati maalum ya kwenda kuchunguza na mimi mwenyewe niliteuwa, kamati ile kwa kupitia Baraza la Elimu na wengineo nje ya Baraza lile.

Kwa hivyo, inapotokea haja ya kwenda kufanya ukaguzi wa aina maalum huwa tunapeleka wakaguzi wetu, lakini kwenda kuchunguza zaidi ya ukaguzi, kwa sababu ukaguzi wa mambo ya *academic* na mambo mengine ya *administration* ya kiskuli, lakini kuna mambo mengine ndani ya skuli ambayo inabidi lazima utumie utaratibu wa kutuma kamati maalum.

Swali lake la pili, naomba kidogo alirejee kwa sababu sikulipata vizuri.

Mhe. Spika: Kuanzishwa kwa skuli hizi binafsi maendeleo huwa mazuri, lakini baadaye huporomoka. Ni sababu zipi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: *Wallahi* sababu itakuwa wanazielewa zaidi wao Mhe. Spika, lakini tatizo kubwa biashara yoyote hata dukani mwanzo duka linapambwa vizuri kila kitu pale, baadaye kidogo mkoba nadhani huwa unakauka na mambo yanakuwa si mazuri. Lakini tatizo la maskuli ni la *academic* zaidi.

Utaratibu uliyopo wanajisahau kama ile ni *service oriented* kuliko *business oriented*. Kwa hivyo, wao pengine wanaingia zaidi kwenye mambo ya kibiashara zaidi wakati mwengine ndio tunakosa ile *quality* yenyewe. Lakini zaidi ya hivyo, kutokana na mwamko mkubwa wa skuli binafsi kumejitokeza kwamba sasa hivi zinaanzishwa skuli za kila aina katika kila maeneo. Wananchi wanayo ruhusa ya kuanzisha skuli hizo, kuna skuli za jamii, *private schools, community schools* na kuna hizi *public or Government Schools*.

Sisi kwa upande wetu ni kuweka vigezo ambavyo vinakidhi mahitaji ya skuli ile, wakishafikia viwango vile, basi tunaruhusu, lakini suala la ubora wa elimu Mhe. Spika, tunaliangalia na tunahakikisha pale ambapo matokeo yanakuwa si mazuri ndio pale tunapofanya tafiti zetu na kuunda kamati mbali mbali kufanya utafiti huo. Tunashukuru mambo yanakwenda vizuri na matokeo yetu yanaelekea kuwa mazuri. Ahsante.

HOJA YA MJUMBE INAYOHUSU MAPENDEKEZO YA UANZISHWAJI WA MFUMO WA SERIKALI YA UMOJA WA KITAIFA

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii na kuikubali hoja yangu ili niweze kuiwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu.

Pili, Mhe. Spika, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai sote tukiwa wazima na kufika hii leo kuniwezesha mimi kuiwasilisha hoja hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwa kutumia uwezo niliyopewa chini ya vifungu 49(1) na 50(1)(2) na (3) za Kanuni za Baraza la Wawakilishi, naomba kuleta hoja binafsi inayofuata.

Kwanza kwamba kuna haja ya Baraza la Wawakilishi likiwa ndio chombo cha juu cha wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar waliyotokana na ridhaa za Wazanzibari kupitia Uchaguzi Mkuu kuyapa nguvu maridhiano ya kitaifa ya Wazanzibari yaliyotokana na mazungumzo kati ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi *CUF*, Maalim Seif Sharif Hamad yaliyofanyika tarehe 5 Novemba, 2009.

Pili, kwamba katika kuyapa nguvu maridhiano hayo na kwa lengo la kustawisha umoja na mshikamano miongoni mwa Wazanzibari na kujenga misingi imara ya amani na utulivu wa kudumu hapa Zanziabar, basi uanzishwe Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayohusisha vyama vya siasa vyenye wajumbe katika Baraza la Wawakilishi.

Tatu, kwamba mfumo huo wa serikali ya pamoja ya kitaifa uzingatie uwiyoano kwa mujibu wa kura za uchaguzi wa Rais.

Nne, kwamba Baraza hili tukufu lifanye marekebisha ya vifungu vya 39,42 na 61 vya Katiba ya Zanzibar kwa madhumuni ya kuweka utaratibu utakaowezesha kuanzishwa kwa Mfumo huo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Tano, kwamba Baraza hili tukufu liweke utaratibu utakaowezesha wananchi wa Zanzibar kutoa ridhaa yao kuunga mkono mfumo huo mpya ninaoupendekeza kwa njia ya kura ya maoni au kwa njia nyengine yoyote ambayo wananchi hao kwa kupitia wawakilishi wao waliowachagua wataamua.

Mhe. Spika, sasa naomba kutoa maelezo ya hoja yenyewe. Mhe. Spika, sote tuliyo ndani ya Baraza lako tukufu na wananchi kwa ujumla, tunaolewa hali ya kisiasa iliyokuwa ya wasi wasi, ngumu na isiyo na utulivu iliyokuwepo Zanzibar kabla ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi CUF, Maalim Seif Sharif Hamad kukutana na kufanya mazungumzo hapo tarehe 5 Novemba, 2009.

Hali ambayo ilikuwa na kila dalili ya uwezekano wa kuleta uvunjifu wa amani na kuweza kusababisha Wazanzibari kupoteza maisha yao, mali zao na hata utu wao.

Mhe. Spika, kwa maana hii, sisi Wazanzibari kwa pamoja bila ya kujali nafasi ya mtu, chama cha siasa anachotoka au itikadi aliyonayo, hatuna budi kuwashukuru na kuwapongeza viongozi hao kwa hatua yao hiyo ya kijasiri na ya kizalendo na tuungane nao kwa pamoja kama ni Wazanzibari tunaoipenda nchi yetu kwa maslahi ya Zanzibar na watu wake, kwa maendeleo ya Zanzibar yetu na Tanzania kwa ujumla.

Kuna haja pia sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu tukiwa ni wawakilishi halali wa wananchi wa Zanzibar kuchukua hatua madhubuti na kihistoria kwa lengo la kuyapa nguvu maridhiano hayo na kwa lengo la kustawisha umoja na mshikamano miongoni mwa Wazanzibari na kujenga misingi imara ya amani na utulivu wa kudumu hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, naamini kwa dhati kwamba tukiwacha fursa hii ya kihistoria bila ya kuchukua hatua ya kutilia nguvu na kujenga misingi madhubuti, upo uwezekano mkubwa wa hali ya kisiasa kurejea kule tulikotoka na hivyo, kuendelea kuiathiri nchi yetu kijamii, kiuchumi, kisiasa au hata watu kupoteza maisha yao pamoja na mali zao au vyenginevyo hali ya Zanzibar kiamani kuvurugika. Umoja kukosekana, uzalendo kupotea na hivyo, kuwapa mwanya maadui zetu kutugawa, kututawala na kufanya watakavyo katika nchi yetu wenyewe.

Mhe. Spika, naamini pia kwamba njia pekee madhubuti itakayoweza kuyatilia nguvu maridhiano hayo na kujenga Zanzibar na watu wake kwa misingi imara ya umoja, mshikamano, amani na utulivu wa kudumu ni kwa kuanzisha Mfumo

wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayohusisha vyama vya siasa vyenye wajumbe wake katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naamini vile vile kwamba wananchi wa Zanzibar ambao kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ndio wenye maamuzi ya mwisho ya kuamua jinsi gani Zanzibar inafaa kuongozwa. Panapaswa kushirikishwa moja kwa moja kupitia kura ya maoni au kwa njia nyengine yoyote ambayo wananchi hao kupitia wawakilishi wao waliowachagua ambao ndio Wajumbe wa Baraza lako tukufu wataamua kutoa ridhaa yao kwa Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa unaopendekezwa ili uwe msingi madhubuti wa kidemokrasia.

Mhe. Spika, sasa naomba nitoe hoja yenyewe.

Basi kwa kuwa nchi yetu inakabiliwa na uchaguzi mkuu hapo mwezi wa Oktoba, 2010 wa kumchagua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

Na kwa kuwa uchaguzi katika Zanzibar mara zote umeambatana na hali ya mivutano mikubwa ya kisiasa ambayo mara nyingi imepelekea kugawanyika kwa jamii ya Wazanzibari na hivyo, kuathiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Na kwa kuwa uchaguzi unaotukabili upo karibu sana na kuna haja ya kuchukua hatua zitakazowezesha Wazanzibari kuendelea kuwa wamoja kabla na baada ya uchaguzi na hivyo, kuendelelea kushirikiana katika kuleta maendeleo yao na nchi yao.

Na kwa kuwa hatua ya kukutana na kufanya mazungumzo baina ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi *CUF* Maalim Seif Sharif Hamad, imeleta hali ya amani, umoja, mshikamano na maelewano makubwa miongoni mwa Wazanzibari.

Na kwa kuwa Wazanzibari kwa ujumla wao bila ya kujali itikadi zao za kisiasa na kupitia jumuiya na taasisi zao mbali mbali, wameonekana kuunga mkono na kufurahia hatua na matokeo ya viongozi hao wawili kukutana.

Na kwa kuwa Jumuiya ya Kimataifa kupitia taarifa na kauli za nchi, jumuiya na taasisi mbali mbali imetangaza kuwapongeza viongozi hao kwa hatua kubwa na ya kihistoria waliyoichukua na kutaka waungwe mkono katika juhudi zao hizo huku ikiahidi kutoa msukumo na misaada zaidi katika kusaidia Zanzibar ipige hatua kubwa zaidi za maendeleo.

Na kwa kuwa kuna haja ya kuinusuru Zanzibar yetu kwa Wazanzibari wote kuungana kwa pamoja bila ya kujali chama, itikadi, kabila, rangi, dini na kadhalika. Hivyo basi, ili kuwapa moyo wananchi na kuona serikali yao inawajali, inawatetea, inataka kila mtu apate haki yake kikatiba na kwamba iko tayari kuwahifadhi wao na mali zao, mimi Abubakar Khamis Bakary, Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni, Wilaya ya Micheweni Pemba naomba kutoa hoja binafsi ya kulitaka Baraza hili tukufu lifanye mambo yafuatayo:-

1. Lifanye marekebisho ya vifungu vya 9(3), 39, 42 na 61 vya Katiba ya Zanzibar.
2. Litamke kwamba, muundo wa serikali Zanzibar uwe ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayohusisha vyama vyote vya siasa vilivyomo katika Baraza la Wawakilishi na kwamba viongozi wa serikali watokane na uwiano wa kura za Rais katika uchaguzi mkuu.
3. Litamke kwamba, serikali hiyo ya Umoja wa Kitaifa itakayoundwa itaendelea kuheshimu na kuthamini misingi mikuu ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964 kama ilivyotangazwa na Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume hapo tarehe 8 Machi, 1964.
4. Liweke utaratibu utakaowawezesha wananchi wa Zanzibar kushiriki kwa njia ya moja kwa moja kutoa ridhaa yao kuunga mkono mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa njia ya kura ya maoni, na kwamba kura hiyo ya maoni iwe imeandaliwa na kufanyika si zaidi ya mwezi wa Mei, 2010 au liweke utaratibu mwengine kwa njia ambayo Wazanzibari wenyewe kwa kupitia wawakilishi wao waliyowachagua wataona inafaa.
5. Liagize serikali ndani ya siku saba kuandaa na kuufikisha mbele ya Baraza hili tukufu Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 kwa madhumuni ya kuweka utaratibu, masharti na namna ya uendeshaji wa kura ya maoni na pia kuipa mamlaka Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar mbali ya majukumu yake iliyonayo sasa. Pia, kusimamia na kuendesha kura ya maoni kwa yale masuala mazito yanayohitaji maamuzi ya wananchi moja kwa moja.
6. Liagize serikali kufanya mawasiliano na nchi rafiki, washirika wa maendeleo na jumuiya za kimataifa kwa lengo la kuona

uwezekano wakusaidiwa gharama za uendeshaji wa kura hiyo ya maoni ili kupata ridhaa ya wananchi katika suala hilo zito.

7. Pale litakaporidhia hoja hii, basi livitake vyama vyote vya siasa vyenye wajumbe katika Baraza hili tukufu kujikubalisha kuunga mkono hoja itakayopelekwa kwa wananchi ya kuomba kuidhinisha uanzishwaji wa Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.
8. Chini ya Kanuni ya 48(6) na 78(3) ya Baraza hili, Baraza lijadili rasimu ya Mswada wa Marekebisho ya Katiba ya Zanzibar kwa vifungu vilivyohusika, ambavyo kwayo vimeambatanishwa na hoja hii na ambavyo ni sehemu ya hoja yenyewe na baadaye upelekwe serikalini kama ni Mswada wa Serikali ambapo serikali baadaye kwa kutumia utaratibu uliowekwa kikatiba na kwa mujibu wa Kanuni za Baraza utapelekwa katika Baraza lako tukufu chini ya Kanuni ya 80 ya Kanuni za Baraza kuhusu miswada inayopelekwa Barazani kwa hati ya dharura.
9. Liunde kamati ya Wajumbe sita, watatu kutoka upande wa serikali na watatu kutoka upande wa upinzani, kwa madhumuni ya kusimamia hatua zote zinazopendekezwa kwa hoja hii hadi kukamilika kwake.

Mhe. Spika, hapa haya maneno yaliyoanzia ‘kama mpaka hoja hii’ nimeyafuta kwa mujibu wa *notice* niliyoitoa katika barua niliyompelekea katibu ya tarehe 25, na hii haikuharibu hoja yoyote.

Mhe. Spika, baada ya hapo katika ukurasa unaoendelea wa sita kuna mapendekezo hayo ya marekebisho ya katiba ambayo ninayafikiria yafanywe. Kwamba kifungu cha 9(3) cha katiba kirekebishwe ili kuwe na muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utakaokuwa wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo utendaji wa kazi zake utafanywa katika utaratibu utakaohakikisha kuendelezwa kwa umoja nchini na lengo la kufikia demokrasia chini ya misingi mikuu iliyowekwa na Mapinduzi ya 1964 ambayo ilikuwa ni:-

- (a) Kutaifishwa kwa ardhi na kugawiwa kwa wananchi.
- (b) Kutaifishwa kwa majumba na kupewa wananchi wasio na uwezo.
- (c) Kutolewa kwa elimu bure kwa wote.
- (d) Kutolewa kwa matibabu bure kwa wote.
- (e) Kupigwa marufuku uwekaji poni na rehani.
- (f) Kupigwa marufuku kwa vyama, jumuiya na klabu za kikabila na kuondoa ubaguzi wa aina yoyote ile.

Kifungu cha 39 pia kirekebishwe ni kwamba kiwekwe kifungu kidogo kama ifuatavyo:-

Bila ya kuathiri masharti mengine ya katiba hii, Waziri Kiongozi atapatikana kwa kuteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na chama cha siasa kilichoshika nafasi ya pili katika uchaguzi wa Rais na vifungu vyengine vyote vitabakia kama vilivyo.

Kifungu cha 42 pia Mhe. Spika, ninaomba kirekebishwe ambacho tunaweka kifungu cha 42(3) kwa mfumo ufuatao:-

Mawaziri wote watateuliwa kwa kuzingatia uwiyo wa kura za Rais walizopata vyama vilivyomo ndani ya Baraza katika uchaguzi wa Rais na vifungu vyengine vyote vitabakia kama vilivyo.

Mwisho ni kifungu cha 61 ambacho pia ningeomba kirekebishwe kwa kuweka kifungu cha 61(4) kama ifuatavyo:-

Kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya watateuliwa kwa kuzingatia uwiyo wa kura za Rais walizopata vyama vilivyomo ndani ya Baraza katika uchaguzi wa Rais uliopita.

Mhe. Spika, haya ndio mapendekezo yangu na kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Spika: Hoja imeungwa mkono kuashiria kwamba sasa hoja hii ni ruhusa kuweza kujadiliwa. Napenda niwajulishe, Waheshimiwa Wajumbe wenyewe mnajua, lakini wageni na waandishi wetu hawaelewi, nikisema hoja imeungwa mkono msije mkasema Spika alisema kwamba hoja ishaungwa mkono aa, uungwaji wa mkono huu ni utaratibu tuliojiwekea kwa mujibu wa kanuni kwamba hoja inayotolewa ionekane kwamba je, kuna wajumbe wowote au yeyote aliyeunga mkono? Kwa maana kwamba inaruhusika hoja hiyo ijadiliwe? Ndio kauli ile kwamba hoja imeungwa mkono na nikasema hiyo inaashiria kwamba sasa hoja hiyo ijadiliwe.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha leo katika Baraza letu hili tukufu kuwa na afya na tukapokea hoja hii na kwamba sasa hivi tuwe tayari kwa ajili ya kuijadili.

Pili, napenda kuchukua nafasi hii Mhe. Spika, kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kwanza katika kushiriki kujadili hoja hii.

Mhe. Spika, hoja hii ina mambo mazito sana na lazima tuijadili. Mimi najua hii hoja iligawiwa tangu juzi na niliisoma na nikaona kwamba wajibu wa kujadiliwa tuwe nao tutoe maoni yetu. Ndani ya hoja hii Mhe. spika, yamo mambo ambayo tunaweza tukayakubali, lakini kwa mawazo yangu mimi na hasa mimi yako mambo napenda kutoa hoja ya kuyakataa. Nitayaeleza moja baada ya moja na nitatoa sababu zake.

Mhe. Spika, hoja ya Mhe. Mjumbe, imezungumza juu ya kuyapa nguvu maridhiano ya viongozi wetu Mhe. Amani Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad. Katika kipindi chote hiki tangu wamekutana kwenye mazungumzo na ufafanuzi tulioupata katika sehemu mbali mbali juu ya mazungumzo yao imedhihirika kwamba maridhiano yao yalikuwa na nia ya kujenga umoja, maelewano, mshikamano katika ujenzi wa nchi yetu na kuweka utulivu wa kudumu.

Mhe. Spika, bila ya kujali itikadi ya chama, lakini mimi chama changu ni Chama cha Mapinduzi. Mimi chama changu nachukulia kwamba mambo haya yaliyomo katika maridhiano yakuleta amani, umoja na utulivu ni mambo ambayo yamo katika sera ya chama changu na nia na dhamiri ya kuendelezwa na chama changu.

Kwa sababu hiyo Mhe. Spika, hili mimi limokatika orodha ya mambo ambayo ninayakubali kwa sababu najua ninatekeleza sera ya Chama changu cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, jengine ambalo limo katika hoja hii ni suala la kujenga au kuunda serikali shirikishi au Serikali ya Umoja wa Kitaifa kama ilivyoitwa ndani ya hoja hii. Chama changu mimi siwezi kukaa nisikitaje Mhe. Spika, Chama changu cha Mapinduzi kilifikiria zamani kwamba katika kujenga maelewano na maridhiano mazuri na kama tuna nia ya kutaka kujenga Serikali ya Umoja wa Kimataifa, basi wananchi washirikishwe na waulizwe. Watoe maoni yao juu ya suala hili, hili ni suala ambalo chama changu kiliamua zamani na kimeliamua hilo kwa nia ya kutaka kuleta umoja na mshikamano na kufikia katika maelewano na amani ya kudumu.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, suala la njia nyengine ya kufanya maamuzi juu ya suala hili ambalo litakuwa tofauti na hili la kuwashirikisha wananchi hiyo mimi siungi mkono. Mimi naunga mkono kama tunataka kufanya hiyo serikali ya umoja wa kitaifa, basi tuwaulize wananchi kwa njia ya kura ya maoni. Nakubali Mhe. Spika, kwamba sisi ni wawakilishi wa wananchi na

wametukabidhi kazi ya kuwaendeshea hii nchi, lakini unapokabidhiwa kitu likitokea suala zito ni vizuri urudi kwa yule aliyekukabidhi, usichukulie tu kwamba nimekabidhiwa pamoja na masuala mazito yote ukasema unayabeba wewe, kuna tatizo lake Mhe. Spika. lazima nitoe mfano mdogo tu ambao pengine watu wanaweza wakafahamu kwa nini nasema hivi.

Mifano iko mingi, kuna mifano mikubwa mikubwa, lakini mimi nitazungumza mifano ambayo inaweza ikaeleweka na watu wengi wa kawaida.

Mhe. Spika, umepewa nyumba, umeruhusiwa nyumba ile kuitunza, ipake rangi bati ikatoboka pale, utafute jengine, shata ya mlango ikibomoka utie nyengine na kama njia ile inakusudia kutia mapato, basi iwe inaleta mapato na ufanye jitihada ya kuona kwamba inaleta mapato. Nyumba ile kama kuna waharibifu wanataka kuja kuidhuru, basi uilinde ili wasiidhuru.

Lakini Mhe. Spika, likakupitikia wazo, nyumba mlango wake umeelekea upande wa urejua na kawaida ya mlango yetu ya mbele huwa inafuatana na ukumbi mkubwa. Sasa mimi niliyepewa ile nyumba kuitunza nimefikiria kwamba mlango wa nyumba ile sasa niubadilishe na niuelekeze kaskazi na kaskazi kuna chumba, itabidi kile chumba ndio nikigeuze ukumbi na mlango mkubwa niweke kule.

Sasa sidhani kama hili nitaliamua bila ya kurudi kwa mwenye nyumba ee bwana wee, ile nyumba uliyonikabidhi naona tufanye mabadiliko makubwa ambayo yataingiza gharama, sasa tufanye mabadiliko haya. Lazima nirudi kwa mwenyewe, lakini kwa yale mambo ya kawaida tu ya kupata rangi, kutengeneza shata kama imevunjika, waya wa mbu na mengineyo, yale naweza kufanya mimi, kuilinda isiharibiwe yale naweza kufanya, kutia kiraka kama anavyonambia Mheshimiwa pia naweza kufanya.

Lakini suala la kuibadilisha nyumba *shape* yake sasa kwa sababu kuunda serikali shirikishi ina maana tunabadilisha *shape* ya serikali. Mhe. Spika, ndio maana nikasema tusijitwike mzigo wa sisi kufanya marekebisho haya, lakini tuwaulize wananchi wenyewe wanasemaje.

Mhe. Spika, mtoa hoja amezungumza mambo mazuri sana, lakini ndio nasema mengine pamoja na uzuri wake inalazimika kutoa ushauri na kwamba siyaungi mkono na mengine nimeshaeleza mwanzo kwamba nayaunga mkono.

Kwenye ukurasa wa 4, hapa mtoa hoja ameeleza mambo ambayo Baraza hili anataka liyafanye akayaorodhesha pale tangu nambari moja mpaka nambari tisa. La kwanza anasema lifanye marekebisho vifungu vya 9(3) 39, 42 na 61

vya Katiba ya Zanzibar. kifungu cha 9 cha katiba kinazungumzia muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba iwe inayojenga umoja na kidemokrasia.

Kifungu cha 39 kinazungumzia nafasi ya Waziri Kiongozi. Mhe. Spika, kama tulivyosema mwanzo kama tunataka kuingia kwenye marekebisha makubwa kama haya ya sasa hivi, nadhani huu muundo wa serikali ni vizuri sasa hivi tuabadilishe ili tupate serikali inayo-*fit* yale mabadiliko inayotaka.

Mhe. Spika, tunapochagua Rais na mtu akafanikiwa akaupata Urais wananchi wanamtegemea atawahudumia tena bila ya kujali wanatoka chama gani, atawaletea maendeleo na atawashughulikia maisha yao siku kwa siku na atatekeleza hata ile ilani ya kile chama ambacho kimempendekeza kuja kugombea.

Mhe. Spika, Rais huyu lazima aekewe mazingira ambayo yatamuondoshea kikwazo cha kutekeleza hayo, maana hayo ndio muhimu. Sasa kama tunataka kujenga Serikali ya Umoja wa Kitaifa, basi tutakuwa na Rais mtendaji kama tulivyokuwa tunaendelea kuwa nae. Lakini sasa tunakwenda kwenye Umoja wa Kitaifa, nadhani tumuwekee Ma-naibu Rais wawili huyu au kama tutawaita Makamu tutakavyoamua, Wajumbe wa Baraza wapo na Rais wa kwanza atatoka katika hicho chama cha pili kilichotokea wa pili katika kura hizo za Rais.

Lakini kuna zile kazi za siku kwa siku za kila siku pamoja na utekelezaji wa sera na ahadi za uchaguzi. Maana wakati wa uchaguzi Mhe.Spika, kunatoka ahadi nyingi tu, utekelezaji wake, basi huyu Naibu wa pili atoke kwenye chama cha huyu Rais. Maana huyu ndiye atakayesimamia utendaji wa siku kwa siku na kuhakikisha kwamba sera ile iliopo na ahadi zile ziliopo zinatekelezwa.

Mhe. Spika, silisemi hilo kwa nia mbaya nalisema hilo kwa kukimbia shetani. Shetani anaweza akatokezea kukatoka migomo migomo hivi na akapata tabu Rais wetu katika utekelezaji. Kwa hivyo, nasema hilo kwa kukimbia yule ya shetani.

Lakini ikiwa huyu Rais na Naibu wa pili wanatoka chama kimoja, nasema chama chochote kitakachoshinda Mheshimiwa, kwa kweli itasaidia kumuwezesha huyu Rais kutekeleza majukumu yake na kuwa naye huyu siku kwa siku pamoja na yule mwengine atampangia kazi. Lakini huyu atakuwa ndie kiongozi katika Baraza la Wawakilishi na likitokea tatizo ambalo tuombe Mwenyezi Mungu lisitokee, tusiloweza kuliepuka huyu awe ndiye mrithi wake.

Mimi nalipendekeza hilo. Kwa hivyo, marekebisho hayo ya kifungu 39 tukasema tuende tu kidogo hiyo, mimi naona tusiende moja kwa moja, tunaingia katika mfumo mpya sasa hivi.

Kifungu cha 42 kinazungumzia wizara. Katika ile hati ambayo Mheshimiwa ameisoma katika hii nyongeza alioweka huku nyuma kifungu cha 42 (3) juu ya suala la mawaziri. Hapa Mhe. Spika, mimi nina pendekezo langu humu ndani na hii hoja imesema wazi kwamba katika Wajumbe waliomo katika Baraza.

Mtu anayeteuliwa kuwa waziri kwa mujibu wa Katiba yetu na kifungu hicho hatujakigusa kwamba tutakifanyia mabadiliko atatoka ndani ya Baraza la Wawakilishi. Sasa unapokuwa unavyama vinne vyote vimegombea U-rais kimoja kimetokea wa kwanza, chengine kimetokea cha pili, kile cha kwanza kimepata ushindi wa Rais pamoja na viti na kile cha pili kimepata kura. Lakini hazikumshinda yule wa mwanzo pamoja na viti. Lakini cha tatu kimepata asilimia kumi na tano, lakini hakikupata kiti hata kimoja. Mhe. Spika, huyu waziri wa chama hiki utamtoaje kama unatizama uwiano wa kura za Rais na hayumo katika Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, mimi natoa pendekezo hapa tutizame vipi uwiano wa viti katika Baraza la Wawakilishi ndio tugawane hizo nafasi za uwaziri. Lakini Mhe. Spika hayo yanakuja wakati gani? Kama wananchi wameshakubali tuende na hiyo serikali yenyewe ndio yatakuja haya.

Mhe. Spika, kuna kifungu chengine cha 61 ambacho nacho tumeshauriwa katika Baraza hili kwamba nacho tukifanyie marekebisho. Kifungu hiki Mhe. Spika, kinahusu Wakuu wa Mikoa. Lakini humu imezungumzwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya katika hii hoja. Mhe. Spika, Wakuu wa Mikoa ni wanasiasa. Tunaweza tukasema kwamba wanasiasa twendeni basi, lakini Wakuu wa Wilaya tuwaache Rais ndiye anayeamua. Lakini haya tugawane kama walivyosema kwa mujibu wa wilaya.

Mhe. Spika, narejea tena, maana sina hakika pengine wananchi wananisikiliza huko nje. Haya yafanywe baada ya kukubali wananchi kwamba tuwe nayo hiyo serikali ya pamoja au tusiwe nayo. Yaani tuwe tumeshapiga hiyo kura ya maoni ndio tuende kwenye haya marekebisho tusije kwenda kwenye marekebisho hata wananchi hawajaamua. Mhe. Spika, mimi mawazo yangu itakuwa si barabara waamue kwanza.

Katika ukurasa ule ule wa 4 tunasema Baraza litamke kwamba muda wa Serikali ya Zanzibar uwe ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa itayayohusisha vyama vyote vya siasa vilivyomo katika Baraza la Wawakilishi na kwamba viongozi wa serikali watokane na kura za Rais katika Uchaguzi Mkuu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo akubali kwamba Rais na Makamu wake watumie kura za Rais, lakini mawaziri hawa watumie idadi ya viti ndani ya Baraza. Mhe. Spika, Baraza litamke kwamba Serikali hiyo ya Umoja wa Kitaifa itakayoundwa itaendelea kuheshimu na kuthamini misingi mikuu ya Mapinduzi ya tarehe 12 Jan 1964, kama ilivyotangazwa na Rais wa kwanza wa Jamhuri wa watu wa Zanzibar Marehemu Mzee Abeid Aman Karume tarehe 8 Machi 1964.

Mhe. Spika, hili si baya isipokuwa tu Baraza litake indhari kwamba kuna mengine katika hili yameshabadilika. Kwa hivyo, kutengeneza ile *thrust* ya Mapinduzi ni kitu muhimu sana. Lakini kwa kadiri siku zinazoendelea na mabadiliko yanatokea, basi tuzingatie yale mabadiko ambayo yametokea.

Mhe. Spika, nne Baraza liwekwe utaratibu utakaowezesha wananchi wa Zanzibar kushiriki kwa njia ya moja kwa moja kutoa ridhaa yao kuunga mkono mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa njia ya kura za maoni hapa haswa. Haya yaliozidi huko mwisho Mhe. Spika, mimi nayakataa.

Halafu Baraza liagize serikali ya siku saba kuandaa kufikisha mbele ya Baraza hili tukufu mswada wa marekebisho ya sheria ya Uchaguzi Zanzibar kwa madhumuni wa kuweka utaratibu wa masharti na uendeshaji wa kura za maoni na pia, kuipa mikakati Tume ya Uchaguzi mbali ya majukumu yake iliyonayo sasa. Hii Mheshimiwa, itabidi ifanywe hatuwezi kuingia kwenye kura ya maoni kabla hatujafanya sheria. Lazima kwanza utangulize hiyo sheria yenyewe itakayotwezesha kufanya hiyo kura ya maoni.

Baraza liagize serikali kufanya mawasiliano na nchi rafiki washirika wa maendeleo ya Jumuiya za kimataifa kwa lengo la kuwa na uwezekanao wa kusaidia gharama za uendeshaji kwa kura hiyo ya maoni ili kupata ridhaa ya wananchi. Hili ni suala la kuwategemea wakati mwengine kuwapa wafadhili ni jambo la kawaida hili, mimi sina tatizo nalo. Lakini pale itakapotokea ridhaa hoja hii Mhe. Spika, itabidi kwanza tukubaliane juu ya ile hoja yenyewe kama nilivyona mimi mapendekezo na wenzangu kama wanaipenda wataunga mkono na kama hawaipendi basi.

Lakini mimi ndio nimeshazungumza, kwamba hiyo hoja yenyewe iwe na mfumo ule tuwe na serikali itakayokuwa na Rais mtendaji, tuwe na serikali iliyokuwa na Ma-naibu Rais wawili, mmoja ni yule aliyepata nafasi ya pili katika uchaguzi, watatu katika kile chama ambacho kimeshinda cha yule Rais na mawaziri wateuliwe kwa mujibu wa uwiano wa viti Barazani hiyo sawa sawa nakubalia kabisa. Sasa wananchi unapokwenda kuwaeleza suala hili

tuwaeleze hilo jambo lenyewe linalotaka kufanywa wajue hayo mabadiliko yenyewe kabla hawajapiga hiyo kura ya maoni.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba mimi nashauri kwamba Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa ambayo imeombwa kama tunakubaliana au kama wananchi wanakubali iwepo, basi ipewe nafasi ya kufanyiwa *review* baada ya kipindi fulani. Maana yake wakati mwengine Mhe. Spika, unaweza kuihitaji kuwanayo maisha, lakini mazingira yakibadilika ikawa hata huna haja ya kuwa na kitu kama hicho.

Hivi sasa Mhe. Spika, hakuna umeme lazima tuwe na majenereta kwa wananchi wenye uwezo nayo. Lakini umeme ukishakuja majenereta ya nini gharama, kwanza majenereta utayasahau utayaweka pahala yatakwishwa kwanza. Kwa hivyo, tuweke kipindi cha ku-*review* Mhe. Spika, je, baada ya miaka mitano au baada ya mitatu au minne tunaweza kwenda nao mfumo huu tena. Maana pengine wakati huo wananchi tumeshawajengea umoja wote washaelewana vizuri kuwa mambo yanakwenda vizuri tena ya nini kwenda kwenye mambo hayo pengine chama kikipiga kura kinapata kura zote maana watu wameshakuwa wanaelewana eti kitu kimoja katika nchi ya nini tena kwenda kwenye mambo hayo. Kwa hivyo, tuweke *review*.

Lakini pia, Mhe. Spika, kuna yule shetani ninayemuogopa miye. Huyu Rais ambaye ana majukumu ya kuwatumikia wananchi huyu na anaongoza serikali hii ya umoja wa kitaifa awekewe utaratibu wa kikatiba utakaomuwezesha kumdhibiti mtu yeyote katika serikali yake atakaonekana kwamba anavuruga utekelezaji ule. Uwepo utaratibu wa kikatiba uwekwe utakaomdhibiti mtu yeyote ambaye yumo ndani ya serikali, lakini ana mipango yake anafanya fanya mambo na nini uwekwe utaratibu kabisa wakikatiba.

Mhe. Spika, mambo haya ya kura ya maoni haya itakuwa ni vizuri tuyafanye kabla ya Oktoba mwaka 2010 na mambo yatakayofatia baada ya watu kupiga kura ya maoni, yaani kubadikisha hayo marekebisho. Tunaweza kuitisha vikao vya dharura tukafanya mambo haya hilo si tatizo maana yake ukitaka uzuri udhurike, itabidi ule gharama. Lakini serikali shirikishi iundwe baada ya matokeo ya Uchaguzi wa mwaka 2010.

Mhe. Spika, mimi nimeusoma huu waraka nimeona haya mambo yaliomo humu ni mazito sana na nikasema basi bora na mimi leo angalau niombe nafasi wa mwanzo nitoe mawazo yangu niliyonayo haya leo nitalala uzuri Mhe. Spika. Ahsante sana nimeshayataja niliyoyakubali na nimeshayataja niliyoyakataa nakushukuru Mhe. Spika. (*Makofi*).

tuende turudi, tuende turudi. Kwa hiyo naomba ruhusa yako nisome ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 124..

Mhe. Spika: Waheshimiwa kidogo nitasema moja kuhusiana na hili. Tusije kusema CCM oye aa hiyo isije, au Haki Sawa aa hiyo isije.

Lakini kwa sababu maudhui ya mitizamo juu ya hoja hii utaweza kunukuu hata *reference* ya kitabu chochote endelea Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Utalii Biashara na Uwekezaji: Sawa sawa Mhe. Spika, hata mimi nilikuwa na wasi wasi huo na niliwaambia Wajumbe wa upande huu mwambie Mwenyekiti wa Chama Wilaya kule isijetoka *point* nzuri hapa akasema CCM oye maana yupo kule.

Mhe. Spika, naomba ninukuu sera ya 2005 kwenda 2010 kwa upande wa chama cha CCM inasema: Sera ya kuunganisha na kuwashirikisha wananchi wa Zanzibar katika harakati za ujenzi wa Taifa lao kwa amani na utlivu. Zilipewa umuhimu mkubwa katika kipindi kilichipita yaani 2000/2005, na kufikiwa Mwafaka tarehe 10 Oktoba 2001 kati ya CCM na CUF ni utihabitisho tosha ya sera sahihi ya sera za CCM.

- (a) Mhe. Spika, ili kuunganisha mafanikio hayo ya kujivunia CCM katika kipindi kijacho 2005/2010 itatekeleza yafutayo moja kuendeleza matunda ya mwafaka kwa faida ya maslahi ya Wanzanzibari wote mwafaka ule uliomalizika.
- (b) kuendeleza kupiga vita kwa nguvu zote ubaguzi wa dini kabla jinsia au asili ya mtu katika utoaji wa huduma na fursa mbali mbali za kiuchumi na kijamii.
- (c) Kuendeleza umoja mshikamano Amani na Utulivu miongoni mwa wananchi wote na kuimarisha jumua mbali mbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii na nataka niseme kwamba Mhe. Spika, kwamba hili kwa upande wa CCM limetekelezeka.

Sasa kutokana na haya baada ya uchaguzi kuliundwa tume ya makatibu wakuu kuendeleza mwafaka huu na Tume ya Makatibu Wakuu ilifanyakazi nzuri sana Mhe. Spika, naomba nipongeze Wajumbe wote walioko katika Tume ile na nina mambo ambayo yalizungumzwa na kufikiwa makubaliano katika Tume ile ya Makatibu wakuu na yalipelekwa katika Vyama CCM na CUF ili kupata maoni ya vyama na baadaye wakae kumalizia shughuli ile. Kwa bahati mbaya hapa ndio alipoingia yule shetani aliyemuoana mwezangu Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora.

Lakini makubaliano yale Mhe. Spika, naomba ninukuu yanasema hivi: “Timu ya mazungumzo ya CCM na CUF zimefikia kwa pamoja maelewano kuhusu ajenda namba moja hadi nne ambazo zilikuweko”.

Katika kuzungumza pande mbili maelewano juu ya haja ya kuundwa Serikali shirikishi ya Zanzibar ilikubalika katika hiyo. Baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010. Kwa hiyo hili halitaki kutiliwa mkazo sana. Kwamba pande zote mbili tulikubaliana kuwa na Serikali Shirikishi lakini iundwe baada ya mwaka 2010. Na inasema kwamba na taswira ya serikali hiyo Shirikishi nikama ifuatavyo.

Hii kazi tumeifanya pande zote mbili moja mshindi wa uchaguzi wa Urais awe Rais mtendaji na chama cha pili kwa kura za Rais kitatoa makamo wa kwanza wa Rais na tatu makamo wa pili wa Rais atateuliwa na Rais kutoka chama chake atakuwa kiongozi wa shughuli za serikali katika Baraza la Wawakilishi na mrithi wa Rais likitokea lisilotarajiwa. Mhe. Spika, nne Rais atachagua mawaziri kwa uwiano na hapa mimi binafsi kama Samia Suluhu lakini nataka nilisome kama lilivyokuja halafu nitajaza langu. Rais atachagua makamo wa Marais kwa uwiano baada ya kushauriana na wakuu wa vyama husika.

Mhe. Spika, la tano linatasema vyama vitashiriki katika Baraza la Mawaziri vikipata zaidi ya asilimia tano za kura za Rais. Lakini hili nataka niseme kabla kwamba kwa upande wa chama chetu sisi tulilifanyia marekebisho hatukuridhiana na hili na ndio tuliyoyarudisha warudi wakayajadili tena.

Jengine kutakuwa na Baraza la usuluhisi, zikitokea tofauti kati ya Rais na Makamo wa Rais na hili pia nalo tulilifanyia marekebisho. Mhe. Spika, nasema hayo kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati kuu ya Chama cha Mapinduzi kwa hayo tuliyajadili pale.

Namba saba inasema Serikali Shirikishi ya Zanzibar itapatikana na Uchaguzi Mkuu ulio huru na haki ili washiriki wawe na uhalali wa kidemokrasia.

Namba nane Serikali Shirikishi ya Kitaifa itaanza mara baada ya matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.

Haya mambo Mhe. Spika, tulishayazungumza pande zote mbili kwa umoja wetu tumepoteza pesa na tumepoteza muda na nguvu za watu wote tumeyajadili. Kwa hiyo wazungu wanasema *tusi-reinvent the wheel* tuangalie yale yaliokubalika na yale ambayo nimesema yatizamwe upya halafu twende mbele tusirudi nyuma kuanzisha hoja nyengine.

Sasa mimi nasema kwa sababu hili lipo na hatua zimechukuliwa lakini zikilikwama basi muungozi tayari tulishaupata ambao uliufanyiwa kazi na pande zote mbili na wala si upande mmoja peke yake na kuleta hapa kujadiliwa.

Mhe. Spika, napenda haya niseme tu kwamba kwa hiyo hoja hii ukiitizama kwa undani ni hoja ya CCM. Lakini nimshukuru sana Mhe. Abubakar Khamis kuleta hoja hii baada ile *stalemate* wakaona bora walete hoja hii. Lakini namshukuru zaidi kwamba hoja hii imetoka upande ule kwa sababu labda kama ingetoka upande huu isingepata mwafaka mzuri. Kwa sababu nakumbuka kabisa mwafaka ambao upande huu wa serikali ulitayarisha hoja na ikaletwa Barazani lakini ulikataliwa kutoka herufi ya kwanza mpaka herufi ya mwisho. Kwa hiyo ni vizuri sana kwamba imetoka kule tutapata kujadili na sisi hatutakataa bali tutajadili na kuonesha sehemu tunayokubali na sehemu ambazo tunazikataa.

Mhe. Spika, sasa niingie kwenye hoja yenyewe. Mhe. Spika, nimeiangalia hoja iliyowasilishwa na mimi kama alivyotangulia kusema Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwamba kuna vipengele ambavyo binafsi navikubali na kuna vipengele ambavyo sikubaliani navyo au nitatoa rai tu tuvibadilishe au tufanye venginevyo.

Kwanza nataka nichukue nafasi hii nikubali kabisa kipengele cha kwanza kilicho ukurasa wa kwanza, kinasema kwamba kuna haja Baraza la Wawakilishi likiwa ndio chombo cha juu cha wananchi wa Zanzibar kuyapa nguvu maridhiano ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Aman Abeid Karume na katibu Mkuu wa Chama cha CUF Mwalim Seif Sharif Hamad. Kwa hivyo hii nakubaliana nayo kabisa.

Pili inasema kwamba katika kuyapa nguvu maridhiano hayo kwa lengo ya kustawisha umoja na mshikamano miongoni mwa Wazanzibari na kujenga misingi imara ya amani ya utulivu wa kudumu hapa Zanzibar kama ilivyoelezwa kwenye ilani ya CCM basi uanzishwe mfumo wa serikali ya umoja wa kitaifa itakayohusisha vyama vya siasa vyema Wajumbe katika Baraza la Wawakilishi. Hili na mimi nasema si baya baada ya kupata ridhaa ya wananchi tuwapelekee wananchi ambao ni wadau wakubwa wa jambo hili na wenyewe waamue, wananchi wakitoa ridhaa ni jambo zuri sana katika kuleta amani na utulivu ndani ya nchi yetu.

La tatu kwamba mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa uzingatie uwiano kwa mujibu wa kura za uchaguzi kidogo Mhe. Spika, mimi hapa niko *mixedup*. Hii ya juu inasema kwa kuangalia vyama vyenye uwakilishi Barazani ina maana vyama vilivyopata viti vikaingia Barazani. Lakini ya tatu inasema

mfumo huo wa serikali wa Umoja wa Kitaifa uzingatie Uwiano kwa mujibu wa kura za uchaguzi wa Rais, kidogo inanichanganya lakini ninaufahamu na namba mbili inasema kuundwe na kuanzishwe mfumo wa kiserikali ya Umoja wa Kitaifa itakayohusisha vyama vya siasa vyenye Wajumbe katika Baraza la Wawakilishi, ina maana vyenye viti.

Lakini ya tatu inasema kwa kura za Rais hapa hebu tupaangalieni vizuri. Mimi ningependekeza kwamba hii sehemu ya tatu isomeke kama ya pili kwamba vyama vyenye viti katika Baraza la Wawakilishi au vyenye Wajumbe kama alivyoifafanua vizuri Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora.

Mhe. Spika, ya nne inasema kwamba Baraza hili tukufu lifanye marekebisho ya vifungu vya 39 na 42 si vibaya kama ilivyochambuliwa na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora lakini na mimi nataka nisistize kama itakavyotoka ridhaa ya wananchi baada ya *referendum* kufanywa.

Namba 5 kwamba Baraza hili tukufu liweke utaratibu utakaowawezesha wananchi wa Zanzibar kutoa ridhaa yao ya kuunga mkono mfumo huo mpya unaopendekezwa kwa njia ya kura za maoni, sasa hii itakuwa ni kazi ya vyama vyenyewe.

Halafu Mhe. Spika, nitilie mkazo tu ukurasa wa pili ile hoja yangu niliyosema kwamba mimi ningeungana na hoja kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayofanywa iendane na vyama vya siasa vyenye wajumbe katika Baraza la Wawakilishi. Ina maana iende kwa viti.

Hoja ya Mheshimiwa aliyewakilisha inathibitisha hivyo katika ukusara wa pili *paragraph* ya pili kutoka chini inayosema kwamba “Naamini pia kwamba njia pekee madhubuti itakayoweza kuyatilia nguvu maridhiano haya na kujenga Zanzibar na watu wake misingi imara ya umoja, mshikamano, amani na utulivu wa kudumu ni kwa kuanzisha mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayohusisha vyama vya siasa vyenye Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, huu uwe ndio mfumo wa kutengeneza serikali yote”.

Mhe. Spika, ukurasa wa 3 kwenye hoja yenyewe, mimi nimefurahishwa sana na *paragraph* ya kwanza inayosema “Basi kwa kuwa nchi yetu inakabiliwa na Uchaguzi Mkuu hapo mwezi Oktoba, 2010 wa kumchagua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani”.

Mhe. Spika, mimi nimefurahishwa na *paragraph* kwa sababu sasa inanipa utulivu wa moyo na ile hoja ya Rais Amani Abeid Karume aendele, serikali ya mpito na uchaguzi uahirishwe, kwa hiyo hii imenipa faraja kwamba wote

tunakubaliana kuwa mwaka 2010 tuingie kwenye uchaguzi halafu tuendeleo na mambo yetu.

Mhe. Spika, ukurasa wa 4 kifungu cha kwanza kinazungumza Baraza lifanye marekebisha ya vifungu cha 9 (3) kama vilivyotajwa. Mimi naomba nianze na kifungu cha 9 (3) kinachozungumza muundo wa serikali. Hapa naomba nifanye *reference* kwenye *document* hii iliyowasilishwa na mjumbe lakini ukurasa wa 6 na nitaangalia kifungu hivyo hivyo cha 9 (3) cha ukurasa ule wa 6 kifungu cha kwanza.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana sana na kifungu cha kwanza 9 (3) aliyoundika Mhe. Mjumbe kwenye hoja inayosomeka “Muundo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar utakuwa wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo utendaji wa kazi zake utafanywa katika utaratibu utakaohakikisha kuendelezwa kwa umoja nchini na lengo la kufikia demokrasia chini ya misingi mikuu iliyowekwa na Mapinduzi ya 1964”. Mhe. Spika, *full stop* iwe pale.

Mhe. Spika, “ambayo ni kuwa” hii ya chini mimi nakataa haikuwa misingi mikuu ya Mapinduzi. Misingi mikuu ya Mapinduzi ilikuwa ni kuwatoa Wazanzibari wanyonge kwenye makucha ya wadhalimu na kuwaweka huru, lakini pia kuwajengea hadhi kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hiyo ndio ilikuwa misingi mikuu ya Mapinduzi. Yaliyoorodheshwa hapa Mhe. Spika, ni mbinu zilizotumika kwa wakati ule na kwa hali ya kisiasa, kimaendeleo, kiuchumi kwa wakati ule, zilitumika mbinu hizi kutimiza hiyo misingi mikuu ya Mapinduzi.

Lakini hii iliyoorodheshwa kifungu (a) mpaka (f) haikuwa misingi mikuu ya Mapinduzi. *In fact*, kufikia leo hatuwezi kuiendeleza kwa sababu imepitwa na wakati.

Masuala ya kutaifisha sasa hivi hayapo na sera zetu zinasema wazi kwamba hakuna kwa sababu tumeingia katika *area* nyengine ya kiuchumi. Kwa hiyo, hii haikuwa misingi mikuu lakini ni mbinu za kufikia hiyo misingi mikuu na kwa wakati ule, haziwezi kutumika tena sasa hivi baadhi yao, baadhi zinaweza kuendelea.

Unaposema tunatoa elimu bure hata kama watu wanachangia sawa, matibabu bure watu wanachangia sawa. Kuna mabadiliko mengi yametokea, kwa hiyo hii hatuwezi tena kuiendeleza.

Mhe. Spika, naomba nirudi tena kwenye hoja ukurasa wa 4 nizungumzie kifungu cha 2 kinachosema “litamke kwamba muundo wa serikali Zanzibar uwe ni wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayohusisha vyama vyote vya siasa

vilivyomo katika Baraza, kama nilivyosema kabla kwamba hii itategemea ridhaa ya wananchi.

Lakini kifungu cha 3 “litamke kwamba Serikali hiyo ya Umoja wa Kitaifa itakayoundwa itaendelea kuheshimu na kuthamini misingi”. Hii nimeshaizungumza ndio ile ambayo nimeizungumza kabla.

Kifungu cha 4 “liweke utaratibu utakaowawezesha wananchi wa Zanzibar kushiriki kwa njia ya moja kwa moja kutoa ridhaa yao kuunga mkono mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa njia ya kura ya maoni (*referendum*)”. Yaliyobakia hapa ya kuweka *target* ya muda ni imani yangu kwamba kazi hii tutakaposema hapa tunakubaliana twende kwa wananchi kama tunavyokubaliana pande zote. Kazi hii tutaikabidhi nadhani kwa Tume ya Uchaguzi au taasisi yoyote itakayokabidhiwa.

Sasa taasisi itakayokabidhiwa yenyewe itajipangia program yake ilimradi tu jambo hili litimie kabla uchaguzi wa 2010. Baada ya uchaguzi tuendeleo na huo mfumo kama ridhaa ya wananchi itasema sawa, kama sio tutaangalia mengine.

Lakini mimi ningeomba hizi tarehe zilizopangwa kwamba serikali iagizwe Baraza liseme mpaka mwezi Mei haya yangeachiwa taasisi ambayo tutaikabidhi kazi hiyo kuendelea nayo.

Hivyo hivyo, kifungu cha 5 na 6 kwa sababu taasisi tutakayoiachia yenyewe itajua wapi ipate pesa za kufanyia hivyo, kama kutoka serikalini, itaomba kwa wafadhili, mimi nahisi tungewaachia wenyewe.

Mhe. Spika, nizungumzie kifungu cha 7 ambacho kinasema “pale litakaporidhia hoja hii”. Hii nimesema ni kazi ya vyama vyenyewe kwenda kwa wananchi na kuwaambia aidha kubalini au vyengevyo vyovyote.

Halafu kifungu cha 8 chini ya kanuni hiyo na hiyo kwamba “marekebisho ya katiba ya vifungu vilivyohusika ambavyo vimeambatishwa na hoja hii”.

Mhe. Spika, naomba nizungumzie sasa vifungu vile vya katiba ambavyo vimeambatishwa na hoja hii.

Mhe. Spika, nikienda kwenye hivyo vifungu vilivyoambatishwa ambao ni ukurasa wa 6 kifungu cha 39 cha katiba kimependekezwa kurekebishwa na kisomeke kwamba “bila ya kuathiri maslahi mengine ya katiba hii Waziri Kiongozi atapatikana kwa kuteuliwa na Rais, kupendekezwa na chama cha siasa kilichoshika nafasi ya pili katika uchaguzi wa Rais”.

Hii ndio ile nilisema tusi-*reinvent the wheel*. Tulikwisha kuzungumza, tulikwisha kubaliana kuwe na Makamo wa Rais wawili, kamati ile ya Makatibu Wakuu imefanya kazi nzuri, basi nadhani tunge-*stick* na ile kuliko kifungu hiki ambacho kimependekezwa.

Halafu kifungu cha 42 cha katiba kinarekebishwa, hiki ni kile cha mawaziri ambao Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban amekieleza vizuri kwamba mawaziri watokane na idadi ya vyama na viti vyao kwenye Baraza la Wawakilishi kuliko kwa *percentage* ya kura.

Hili niliwekea *question mark* kule mbele nikasema wakati tunajadili Kamati Kuu ya CCM tulilikataa kwa wasi wasi ule ambao Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban ameueleza. Kwamba je, ikitokea chama kimepata asilimia 7 ya kura itabidi kiwe na waziri lakini hakina uwakilishi ndani ya Baraza. Nadhani itakuwa si mfumo mzuri.

Mhe. Spika, nizungumzie kifungu cha 61 cha katiba ambacho kinazungumzia uteuzi wa Wakuu wa Mikoa. Mhe. Spika, nimemsikiliza vizuri Mhe. Waziri kwenye suala la Wakuu wa Mikoa. Yeye alisema Wakuu wa Mikoa ni wanasiasa kwa hiyo tunaweza kufika mpaka hapo.

Lakini kumekuwa kuna mawazo tofauti nyuma na hayatoki kwenye vyama ni mawazo tu yanayofikiriwa kwamba kwa sababu Wakuu wa Mikoa wanasimamia Serikali za Mitaa, ndio wanatakiwa kuwa wanasiasa lakini wanatakiwa kuwa *neutral* zaidi. Wanatakiwa kusimamia haki za watu zaidi kuliko mambo ya kisiasa na kwa sababu wakuu wa Wilaya wako chini yao. Kwa hivyo tunaweza tukaendelea kulijadili wanaweza kuwa wanasiasa lakini *my own opinion* tunaweza hata na wao tusiwafanye wanasiasa tukawapa kazi nyengine za kufanya na kwa maana hiyo tukajadili vipi tunaweza tukaenda nao.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na niseme nilikuwa na mchango huo wa kutoa na kwa mjadala huu ulivyo Mhe. Spika, unaweza kusikiliza wengine wanasema nini ukapata *point* baadaye ya kuja kusema. Kwa hivyo tukinyoosha mikono baadaye uturuhusu Mhe. Spika. Ahsnate sana.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: *Bismillah Rahman Rahim*, Mhe. Spika, kwanza ninakushukuru sana kunipatia nafasi hii baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kukaa hapa leo kujadili jambo kubwa lenye mustakbali wa nchi yetu.

Mhe. Spika, mchango wangu mimi leo utakuwa ni wa jumla jumla sana na napenda sana nigusiegusie mambo yaliyopita ingawa si kwa madhumuni ya kuharibu mazingira mazuri ambayo yamejengeka katika mjadala huu.

Mhe. Spika, kwa maana hiyo basi nianze kwa kusema kwamba sehemu kubwa ya historia ya nchi yetu imekuwa ni ya unyanyasaji, ukandamizaji na maonevu na tabaka dhidi ya tabaka. Harakati za kudai uhuru zilisindikizwa na chaguzi kwa maana ya kufikiria tu kwamba chaguzi ndizo njia za kistaarabu za kuweza kuelekea katika Serikali na jamii itakayokuwa huru.

Mhe. Spika, hili halikuwa wazo baya lakini uzoefu wetu wa kihistoria umeonesha namna ambavyo chaguzi zilizofikiwa kwamba zitajenga jamii mpya yenye umoja, yenye nguvu namna ambavyo vile vile zimegeuka kuwa chanzo cha historia mbaya vile vile katika nchi yetu.

Mhe. Spika, maneno haya ninayoyazungumza, ninayazungumza kwa ushahidi kwa kuwanukuu watu wazito ambao ni muhimu sana kuwataja, maana yake kama tungekuwa katika mkutano wa kidini hapa, tungetaja Masahaba, tukamtaja Mtume (SAW). Tukiwa katika jukwaa hili la kisiasa la historia ya nchi yetu si vibaya kuwataja Marehemu Thabit Kombo, Marehemu Abeid Amani Karume, Sheikh Mohamed Shamte na wengineo.

Sasa naomba kidogo tu uniruhusu niyataje maneno ya Sheikh Thabit Kombo katika kitabu chake hiki ambacho ...

Mhe. Spika: Huyu anaitwa Ami.

Mhe. Abass Juma Muhunzi: Mhe. Spika, masimulizi ya Sheikh Thabit Kombo kwenye ukurasa wa 131 alisema maneno haya. "Ilikuwepo vile vile dharau ya Serikali ya Mkoloni kugeuza kauli na kuwanyima Afro-Shirazi haki ya kutawala baada ya kushinda sana katika uchaguzi wa kwanza wa mwaka 1957, ingawa wenyewe wamekwisha kutoa ahadi kuwa atakayeshinda atapewa fursa ya kuunda Serikali. Halafu zile mbinu za wakoloni zilizotumiwa katika kugawa majimbo zilipangwa kuwapa Hizbu majimbo mengi ya uchaguzi na ASP majimbo machache tu lakini yenye watu wengi zaidi. Lengo lilikuwa ni kuelekeza matokeo ya uchaguzi ili Hizbu wapate viti vingi kusudi iwezekane kuwakabidhi wao na Sultan serikali kwa kusingizio cha demokrasia". Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Spika, nimeyataja maneno haya kwa sababu ni funzo kubwa sana katika historia yetu ya kisiasa. Maneno haya leo kwetu sisi yanazusha hofu na kila mara tunapokuwa tunafanya chaguzi zetu, maneno kama haya ambayo yalitamkwa na Sheikh Thabit Kombo, yanatamkwa katika majukwaa yetu ya

kisiasa, ingawa sasa sio yeye Sheikh Thabit Kombo tena. Kwa hivyo humu yametajwa mambo ambayo ya kugawa majimbo, kufikiria kwamba uchaguzi unakuwa unaelekezwa na kwa hivyo lolote tutakalolipanga katika kujenga mustakabali wa taifa hili, ni lazima kwanza akili zetu na fikra zetu zote zielekee katika uchaguzi ambao hauwezi kuturejeshea haya.

Kwa hivyo Mhe. Spika, hofu ya majimbo iliyokuwepo hapo mwanzo, ndio maana tukafikiria kwamba ili kuondosha hili basi kura za Rais ndio msingi. Lakini hoja zilizotolewa ni hoja nzito sana na mara nyengine unaweza ukafikiri jambo, ukafikiri umemaliza kumbe mwenzako akisema ndio anasema kakutanabahisha. Ni kweli kama huna majimbo humu ndani ya Baraza la Wawakilishi, maana yake huna Mawaziri wa kuwapa nafasi kwa sababu Katiba yetu inatueleza Waziri atoke ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, msingi wa kupata majimbo yawe ndio chanzo cha kujenga serikali yetu. Mimi naomba sasa niseme kwamba si wazo baya kwa sababu ndio msingi, lakini lazima Mhe. Spika, mazingira ya uchaguzi huo wa kupata Wawakilishi hao, ni lazima yawe ni mazingira ya kuweka uchaguzi wa haki na huru.

Mhe. Spika, kura ya maoni ni kura kama kura nyengine. Watu watajipanga watapiga kura. Baada ya matokeo, inategemea ni namna gani kura ile iliendeshwa. Kama itakuwa inakwenda varange-varange, jambo hili zuri ambalo sote tunakubaliana nalo ya kura ya maoni. Inaelekea kwamba inaweza ikawa chanzo chengine kippa cha migogoro na kikubwa sana katika nchi hii.

Hivyo si suala la kura tu au kura ya maoni, lakini ni suala la misingi halisi ya kufanya uchaguzi ambao baadaye hauwezi kuturudisha katika migogoro.

Mhe. Spika, hata hivyo niseme kwamba kila inapokuwa ikijitokeza migogoro baada ya chaguzi, viongozi wa vyama, wazee wetu waliokwisha kututangulia hawakununiana lakini walifanya kila aina ya juhudi ya kukaa pamoja kuendesha nchi yao.

Ninapenda nitanabahishe kwamba inawezekana kuwa mtu mmoja alifikiria kwamba tuunde Serikali ya pamoja kama sisi tunavyofikiria hapa, na ikawa jamii huko nje, wapo baadhi ya watu hawataki hata kuisikia lugha hii, na kwa hivyo tukafikiria kwamba kura ya maoni ndio ambayo itaweka mustakabali huru.

Hata katika Chama cha Afro-Shirazi wakati ule. Kuna nukuu hapa ya Mwanamapinduzi mmoja naomba nimnukuu tena John Okello. *After the 1963 election when the ASP had won 54% of the total vote and 63% of the votes cast*

on Zanzibar Island, I remember discussing with Othman Shariff than leader of ASP Parliamentary Opposition the crucial need to form a National Government before independence.

Lakini huyu ni John Okello. Ninakumbuka Mhe. Spika, utanivumilia tena huyu ni Martin Meredis mwaka 2006, anasema hivi, *“In the last election before independence, the ASP gained a majority of total vote cast taking some 54%. But won only a minority of 46%. The result intensified deep routed racial animosity between Arabs and Africans inhabitants. Culminating in Revolution and the emergency of Karume as head of Revolutionary Council”.*

Mhe. Spika, nimejaribu kuyanukuu haya ya kihistoria ili tuyatumie vizuri yatuamshe, yatutanabahishe tuondokane na mambo yote ambayo tunayaona ni matamu yanaweza yakaleta ama utashi wetu wa kisiasa au yanaweza kuwa ni matamu kwa sababu ya kujenga maslahi yetu ya kibinafsi. Nasema sote tuna maslahi humu si upande mmoja tu, kila mmoja ana maslahi, tuyaweke mbali ili tuone kwamba msingi tunaoutaka kuujenga ili tuwe na serikali makini ya watu wanaopendana, ya watu wanaosaidiana, ya watu wanaoshirikiana katika masuala makubwa na mazito ya kijamii na kiuchumi ni uchaguzi ulio huru na ulio haki.

Mhe. Spika, lakini niseme kama nilivyosema mwanzo pamoja na maelezo haya ya John Okello na nilisema mwanzo kwamba sio kila mtu katika ASP alikubaliana na hilo wazo la kuwa na serikali ya pamoja. Sheikh Thabit Kombo Jecha alikataa katakata. Ukurasa wa 29 anasema kwa maneno machache tu “Lakini wazo la Serikali ya Mseto na Afro Shirazi kushiriki tulilikataa tena kata kata”.

Kwa hivyo, nina maana ya kusema kwamba mawazo tunayoyajenga ni mawazo ambayo pamoja na kwamba jamii yetu hatuko pamoja nao hatujawasikiliza, hatujakaa pamoja nao kuwauliza, lakini ni masuala ambayo unaweza wewe ukakubali ndani ya chama kimoja na mtu mwingine akaona silo. Au chama kimoja kikakubali hivi na chama chengine kikaona sivyo.

Mhe. Spika, napenda niwashukuru sana wasemaji wa mwanzo waliotangulia wameonekana dhahiri kwamba wanakubaliana na wazo, yaliyokuwa yana tofauti ni namna ya kujenga. Maana Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban alikubaliana kimsingi kuwa ana nyumba, lakini yeye anasema namna ile ya matengenezo tu, inabidi tumwambie mwenyewe, tufanye hivi, si vibaya.

Lakini Mhe. Spika, tuangalie namna hiyo ambayo tunakwenda kuwaambia watu wetu kwamba iwe ni njia ambayo tukishawaambia basi tujiridhishe kuwa namna tunavyowaambia hivyo ndivyo vilivyo safi kabisa na haitatuletea matatizo baadaye.

Mimi nasema tusijifunge sana tukafikiri kwamba tatizo la serikali ya pamoja hapa ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu kiasi ambacho lazima tunahitaji kura ya maoni. Mimi nafikiri hapa tulitaka kugeuza mfumo wa vyama vingi, mfumo wa chama kimoja ulitawala na ndio uliokuwa ukiendesha mapinduzi. Lakini tuliabadilisha kwa kutafuta tu maoni ya baadhi ya Watanzania, hatukujipanga tukasema tunataka kupiga kura ya maoni. Tukaiondosha nafasi ya Makamo wa Rais ambaye ndiye aliyekuwa kiongozi, mwanamapinduzi na mkombozi wa nchi hii, tukasema sasa asiwe tena Makamo wa Rais awe ni Makamo wa Pili wa Rais na kazi yake nadhani kule sasa hivi ni kushughulikia mazingira.

Tunaweza tukafikiria kwamba hilo maana yake ni jambo lililo kubwa na tumeli-*achieve* katika nchi yetu. Lakini tukiiangalia historia na misingi halisi ambayo aliileta Mzee Abeid Amani Karume, kama angelikuwa yuko hai asingekubaliana na wazo hilo hata siku moja. Sio kwamba asingekubaliana kwa maslahi yake binafsi, lakini asingekubaliana kwa namna ambavyo Zanzibar kwa ujumla na watu wake kwa kweli ingekuwa kidogo imerudi nyuma.

Mhe. Spika, niseme kwamba Makamo wa Kwanza wa Rais Zanzibar na Makamo wa Pili wa Rais si tatizo. Lakini ukishasema una Makamo wa Kwanza wa Rais maana yake huyo ndie mtu wa pili wa Rais. Dunia itataka tuwaeleze sababu nzito za kwamba huyu aliye wa pili asiwe ndie mrithi wa Rais lakini aje awe huyu ambaye sasa ni wa tatu. Ni suala ambalo itabidi tukae tena kitako ni kwa nini, maana yake tunapendekeza vitu kama hivi.

Mhe. Spika, inaonesha dhahiri kwamba wazo juu ya mustakabali wa nchi halitarajiwi kupata na kuungwa mkono na chama kimoja husika licha ya jamii kubwa inayowakilisha mtazamo tofauti wa siasa. Kwa hivyo, tuikubali kura ya maoni katika msingi kwamba inapanua demokrasia, si kwa jambo hili tu lakini kwa mambo mengine yote mazito ambayo yatafuata. Lakini tusije tukajifunga kwamba katika nchi hii katiba yetu, busara za viongozi wetu hasa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba sasa hawezi kufanya jambo lolote mpaka tutenge kura ya maoni.

Mifano niliyoitoa ni hiyo kwamba yapo maamuzi mazito tumekwishayafanya hapa tena mazito sana. Sikulitaja suala la Muungano ambalo lilikuwa ni mazungumzo tu baina ya Rais Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume na Muungano ukafanywa hadi leo upo.

Nilipokuwa nasoma kitabu cha Sheikh Aboud Jumbe anasema “Nilikuwepo Pemba siku hiyo, niliporudi Sheikh Abeid Amani Karume akaniita akasema, Aboud tumekwishaunganisha nchi”. Maneno yake yamo katika kitabu chake cha Mawimbi Makali.

Mhe. Spika, nimeyataja hayo ya kihistoria ili yatusaidie yasiturudishe nyuma, lakini yatuelekeze kwamba bado tunayo nafasi sisi kama watumishi wa watu, watumwa wa watu, tunaosema kwa niaba ya watu, tukitaka kulifanya jambo hili ni kubwa ni fikra zetu tu tunalifanya kuwa kubwa. Lakini kama hili tunalolifanya kwamba la kuwa na serikali ya pamoja ni jambo lililo dogo linaweza likafanywa kwa wakati mmoja na nchi ikatulua safi kabisa.

Hakuna jambo ambalo lilikuwa linaonekana kubwa kama kiongozi wa CUF kwenda akakaa pamoja na Rais Amani Abeid Karume. Wengine lilitaka kututoa roho, ndio haya si limekuwa, kuna kitu gani katika nchi kilichokuwa kimeharibika. Kwa hivyo, mengine tunayofikiria haya kwamba ni mazito tunataka kauli za watu ni fikra zetu tulizozijengea *perceptions*.

Mhe. Spika, katiba yetu hii tuliyonayo ya vyama vingi, kama Rais angetaka hata asishauriane na mtu yeyote akasema mimi nataka kumteua huyu kutoka CUF huyu ni waziri, hatuna pahala pa kumshtaki kwa nini umefanya hivi. Hii ndani ya katiba tuliyonayo sijakiona mimi kifungu kilichomfunga. Lakini ni busara yake anaona twende hivyo kwa sababu ndio tunavyokwenda, ndio utamaduni tuliokuwa tumejijengea. Sasa kama kutatokea busara zikazidi *practise* ambayo tunakwenda, hili tusije tukaliona kwamba ni jambo lililo gumu.

Mhe. Spika, nilisema kwamba ndani ya chaguzi na mambo yaliyojitokeza baada ya chaguzi, yaliyotufahamisha, mafunzo tuliyoyapata ni namna ambavyo nchi yetu ilikuwa imegawika kijamii. Harakati za kiuchumi zilivyodorora sana. Ilifika wakati hapa Mhe. Spika, tunakuja katika Baraza tunadai tunataka hichi tupelekeke katika jimbo, lakini akija waziri anamtafuta Muhunzi yuko wapi hamuoni. Ndio, mnadai kwa kutumia sheria lakini siasa inakwambia bwana hapana.

Mhe. Spika, watu wetu wametabahi kwenye *grass root*, kutanabahi huku wao wenyewe wanatuelekeza kwamba wanasiasa mnakokwenda siko, ndio. Leo wanashirikiana katika mambo chungu nzima ya kimaendeleo, hakuna mtu aliyekaa katika jukwaa akasema kwamba sasa tunakuruhusu shirikianeni, *material condition*.

Mhe. Spika, mtu wa mwisho nataka kumnukuu ni huyu Camila anasema hivi “*The central point of the a say is that democratic government means democracy in administration, as well as in the original legislation. Lakini anasema anamnukuu Levitan, “suggest that administrative technics must not only be consistant with political philosophy on which a government is best but also with the contemporary social and economic conditions”.*

Ni maneno mazito haya. Sisi kwa muda mkubwa tumeichukulia mifumo yetu na falsafa na itikadi za kisiasa ndio za kujengea serikali tu na za kujengea utawala tu, bila ya kuona kwamba mabadiliko ya kijamii na ya kiuchumi yanatufahamisha kwamba tunacho kitu chengine cha kutumia cha kurekebisha mfumo tukenda vizuri.

Leo Mhe. Spika, Zanzibar hapa tuna *crisis* ya umeme na maji, ni *crisis* moja kubwa katika karne hii hatujaiona katika kipindi hiki. Lakini kama isingekuwa ni viongozi wetu wawili, wala hatujui walichokizungumza, kiasi wamekwenda tu na kuonana. Leo ingekuwa suala hili vijasho vinatutoka tumepangiwa majukwaa kila mmoja anakwenda kumpiga madongo mwenzake.

Shida hii Mhe. Spika, ya watu kukaa wakastahamili, wakavumiliana na kuona kwamba aah! Hili si la Mhe. Mansour peke yake ni letu, maana yake kama isingekuwa ni hivyo, basi mazingira haya sasa hivi kila mmoja angekuwa anasema ndio, tayari tungeshaanza kuandika zile *manifest* za uchaguzi, uchaguzi huo wa 2010 kutokana na shida hizi. Lakini watu wametulia, utulivu huu Mhe. Spika, uliopatikana kwa juhudi za viongozi wetu, wamekwishakufanya kazi kubwa sana, wanasubiri sisi ambapo na sisi tumepata ridhaa ya watu kuja huku tutawasaidia vipi tuikwamue nchi hii.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwamba mimi siungi mkono, wala sioni sababu kubwa ya kwa nini lazima serikali hii iwe ni baada ya uchaguzi, sioni sababu. Ninachokiona ni zile zile hofu zilizotutawala tu. Iwapo itakuwa sasa hivi nani atakuwa waziri na nani atakosa, hiyo ndio ninayoiona.

Mhe. Spika, katika maafikiano yoyote kama hukukubali ku-*lose* na ku-*gain*, maafikiano ni *zero*, lazima uta-*lose* na lazima uta-*gain*. Mshindi mkubwa katika maafikiano ni mtu anaye-*lose* akaangalia maslahi ya nchi inavyokwenda, kuliko hata yule ambaye ana-*gain*.

Mhe. Spika, hebu leo tufikirie kuwa waziri amekaa kwa miaka minne sasa bado miezi kumi tu uchaguzi. Akiambiwa leo sio waziri tena. Labda nimwambie Mhe. Mugheiry ambaye ndio kanielekea hapa, kwamba leo sio Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii tena, Mwenyezi Mungu asikujaalie, atakachokikosa ni nini katika mwaka mmoja au miezi kumi, nini atakachokikosa, kama hajakipata katika miaka minne, lakini ni zile fikra tu.

Mhe. Spika, Baraza hili la Wawakilishi la kidemokrasia watu wanaliangalia, na wanalitofautisha sana na Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wameona sisi tumekuwa ni watu tunaowachezea chezea sana. Walikuwa mara nyengine wanakaa wanafikiria na kusema, hawa wawakilishi kukaa CCM huku

na CUF huku wakatazamana maana yake nini, mbona hatuyaoni katika Mabunge mengine. Nikawaambia aah! Ni muundo tu wa Baraza lilivyo, pengine baadae tukipata jengo jipya itaondoka.

Mhe. Spika, yalipokuwa yanaanza mazungumzo haya, watu walikuwa wanatoa maoni yao. Kwanza lilikuja hili la mafuta, nilipokwenda katika baraza zangu huko kwenye jimbo langu, walisema watu wa CUF na kama watakuwa wananisikiliza ni mashahidi. Wanasema tulikuwa katika migogoro mikubwa sana ya CUF na CCM, yaliyotokea ndio yametokea. Lakini sisi tunamsamehe Mhe. Rais wa Zanzibar yote kama kuna jambo alilotufanyia lililokuwa baya, kwa sababu moja tu. Kwa sababu ya hoja aliyoikalia kidete hii ya mafuta. Kwa hivyo, kitu kimoja tu unabadilika na watu wanasahau kila kitu, wanaondoka viongozi wa kidini, asilimia 95 ya nchi hii ni Waislamu, sio utawala wa Kiislamu, lakini ni nchi yenye Waislamu walio wengi. Wanatoka huko wanakwenda wanasema leo tukaeni na tuiombeeni nchi yetu (*Vicheko*).

Mhe. Spika, utakapo wa-*let down* watu kama hawa, tukakaa tunaangalia vyeo tu, nani atakuwa Rais na nani atakuwa waziri. Kwa kweli Mhe. Spika, tutakuwa hatujaitendea haki nchi hii hata kidogo kabisa, yanatoka katika moyo wangu. Nasema sikulishwa na ndani ya Baraza hili nina historia ya kusema mambo yanayotoka katika moyo wangu, kila mmoja anafahamu, hata kama yameniathiri vipi, kila mmoja ikiwa ni ukweli ataukubali huu. Lakini tufanye nini mpaka tuwaridhishe watu wetu kwamba wanataka tukae pamoja, kwa nini kila siku sisi tunapanga siku tu, tunapanga mambo tutafanya kesho na wakati hili jambo ni letu.

Mhe. Spika, Baraza hili hata demokrasia yake, naweza nikampinga waziri kwa sababu ya chama tu kinataka mimi nimpinge waziri, tumeshafanya hivyo. *Backbencher* atamkubalia waziri hata kama anakokwenda siko. Ndio chama kilivyomuelekeza hivyo, *efficiency* ya kutenda kazi katika Baraza hili imekuwa ni ndogo. Mawaziri wanaotoka sehemu zote wakakaa pale katikati, *backbenchers* wakachanganyika hakuna kukaa huku wala huku, hiyo serikali itaonja joto ya jiwe kuanzia leo mpaka 2010 Oktoba kabisa.

Mhe. Spika, *transition period* ni muhimu sana kwa mtu ambaye amelea mawazo yale kui-*observe*, haji kui-*observe* mtu mwengine ambaye hatumjui fikra zake ziko vipi, ni yue mwenye fikra nimeanzisha hapa nataka nione matokeo yako vipi.

Mhe. Spika, limetajwa neno, sijui kulikuwa kuna mambo ya kumuongezea Rais siku za kufanya hivi. Hata Balozi wa Norway nilisoma kwenye gazeti alikataa akasema hataki *engineering* ya *constitution*. Tunaheshimu sana mawazo ya kila mtu aliyefanya. Lakini kama kulikuwa kuna haja ya kusema kwamba tunataka tuione *transition* inakwenda vipi. Wananchi wayaone mafuta, aliyepigania

kidete mpaka akaleta *policy* na kila kitu, mafuta yanaanzishwa vipi. Kama hilo lingekuwa limo ndani ya hoja, basi mimi ningeunga mkono, hata kama ninge kuwa mbaya ndani ya nchi nzima. Kama angeongezewa mwaka mmoja, akiondoka yeye akaingia Mhe. Shamsi Vuai au Mhe. Mugheiry, Katiba inasema atakaa miaka mitano ile ile. Sio kwamba huyu akikaa miaka sita, basi atampunguzia huyu mwaka wake mmoja hamna, inakuwa ni ile ile. Lakini tunalifanya ni jambo kubwa mpaka watu wanasema kwamba jamani mnataka kuharibu katiba. Haichezewi tuliiunda sisi, tusiirekebishe sisi iwe tunataka nguvu nyengine.

Mhe. Spika, nimalizie kwa sababu wako wajumbe wengi ambao wanataka kuchangia, niseme tu kwamba ni vyema Baraza letu sasa, likae na tupevuke kweli kweli na tufanye maamuzi ya kweli kweli na yaonekane, tena maamuzi yakifanyika na yakaonekana yanafanyika pale pale, basi watu wataona namna ambavyo tumepevuka kisiasa. Utakapowaweka watu unangoja sijui Oktoba, unawaweka katika hali ile ile ya mtafaruku, kura ya maoni itakuwa vipi, huo uchaguzi unaokuja utakuwa vipi. Mhe. Spika, itakuwa kazi yote hii tuliyoifanya ni bure. Watu wataanza kusuguana huyu anapita huku na huyu anapita huku. Ni vyema tuanzishe mfumo leo na tuanzishe *machinery* ya kushughulikia uchaguzi ambao utakuwa haki na huru ili tuiokoe nchi hii katika majanga ya kusuguana na kugombana ambayo hayana maana.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, mimi ninakushukuru sana na kwa kweli nawashukuru wote ambao waliotoa maoni yao. Namshukuru sana Mhe. Abubakar Khamis ambaye alileta hoja hii. Lakini nakishukuru Chama cha CCM sana kwamba hii ilikuwa ni fikra wanayo ndani ya chama chao.

Mhe. Spika, tumeambiwa na mjumbe wa CCM walikuwa wanaizungumza na wameshakubaliana, suala liliopo silioni gumu sasa, maana yake kama mpaka ndani ya vikao vikubwa limekuwa *digested* tayari wala sioni ugumu kwa nini likae miezi 10 linasubiri tena. CCM nyengine mbili au tatu ziende zikakae tunafanya vipi, huyu kasema hili tunamngoja mmoja aje kaleta *input* hii. Mwisho tutaiwacha nchi hii hatufanyi jambo lolote.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana (*Makofi*).

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Abass Juma Muhunzi, leo umekuja na *library* yako ndani ya ukumbi huu. Sasa Waheshimiwa Wajumbe tuko wengi tunaohitaji kuchangia, sikutaka kukata katikati, najua inaondoa mustakabali mzuri ulimo ndani ya Baraza hili. Lakini tujaribu kurudi kupanga *points* zetu vizuri na twende moja kwa moja kwenye hoja. Kumbukumbu inaruhusika katika kulenga yale mazungumzo au mchango wa Mhe. Mjumbe. Lakini na muda unatutaka tena kwa mujibu wa kanuni twende kwa utaratibu huo.

Tujitahidi tutumie dakika 20 zilizotolewa na kanuni, tujitahidi hivyo. Spika, anaweza kuangalia pale ambapo pana maneno mawili yamebaki, lakini muda wa dakika 20 umekwisha ataangalia hivyo. Nashukuru.

Sasa ni zamu yake Mhe. Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na baada ya hapo tumsikilize, majina sasa nimeyapata *Alhamdulillah* itakwenda huku na huku. Baada ya hapo tumsikilize Mhe. Asaa Othman Hamad.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakushukuru, kabla sijaendelea, naomba niletewe glasi ya maji kidogo, kwa sababu nahisi sauti yangu imeanza kukauka.

Mhe. Spika: Ni kweli mheshimiwa. Nilitaka kusema mapema kwamba tunajadili jambo zito. Kwa hivyo, watendaji wangu muwe tayari kuwapa maji wajumbe wanaochangia ili asiye akakauka roho. Tengeneza maji na mpelekee.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa asubuhi ya leo kupata nafasi hii muhimu kujadili suala hili zito na muhimu kwa mustakabali wa nchi yetu.

Mhe. Abass Juma Muhunzi alianza kwa Bismillahi Rahman Rahim. Mimi naanza kwa *Audhubillahi Mina Sheytwani Rajim Bismillah Rahman Rahim*, Mwenyezi Mungu atusaidie Inshaallah kwa sababu tunazungumza suala zuri, lenye manufaa na maslahi kwa nchi yetu.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe Ramadhan Abdallah Shaaban kwa kuifanya kazi yetu sisi kuwa ni rahisi sana. Pia nimshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi alivyoweza kutoa ufafanuzi wa hapa na pale.

Mhe. Abass Juma Muhunzi alituchukua kabla ya Uhuru wa mwaka 1964. Mimi Mhe. Spika, sichukuwi kutoka mbali sana, mimi nachukua kutokea mwaka 1995 mpaka 2000 kwanza. Yeye keshapita kote huko kasema tumesikia. Kwa bahati mimi ni shuhuda mkubwa sana wa hali hii ya kisiasa ilivyokuwa. Waliokuwemo humu ndani wamo ambao walihusika kwa njia moja au nyengine katika matatizo hayo mbali mbali. Wakati ule mimi nilikuwa kama Naibu Katibu Mkuu katika Wizara ya Elimu wakati ule.

Mhe. Spika, nilipata bahati hiyo ya kuteuliwa na Dk. Salmini Amour nikawa Naibu Katibu Mkuu, namshukuru sana. Kipindi hiki cha baada ya uchaguzi yalitokea mambo mengi sana na hakuna aliyekuwa ameyafurahia.

Mhe. Spika, nakumbuka kuna kipindi nilikuwa nafanya ziara Pemba kama Naibu Katibu Mkuu nakwenda pale, naitisha vikao vya kamati za skuli, wazee

waje pale. Anabakia Mwalimu Mkuu anaheshimu kwamba anayekwenda ni kiongozi wake, lakini hakuna mwingine ambaye anaongezeka pale, itokezee nadra tu labda wawepo watu wawili au watatu. Hali ile ilikuwa sio nzuri kabisa wala haimpendezi mtu. Mimi sina maumbile ya kuwa ni mnene, ni hivi hivi na nilikuwa mwembamba zaidi kuliko hivi, makoti tu haya yasitie mashaka watu.

Mhe. Spika, katika kipindi kile cha mwaka 1995 mpaka 2000, nakumbuka Mhe. Mapuri ndiye alikuwa Waziri, tukenda skuli ya Mtambile kutoa msaada pale wa skuli. Mhe. Mapuri akatoa tamko, akasema huyu mwalimu Haroun sio mwili wake huu, lakini kutwa anakwenda mbio huku na huko na serikali inajitahidi kwenda mbio huku na huko kwa ajili ya kuwaleteeni maendeleo. Sasa ndio tunawaleteeni misaada hii na hampo wenyewe tunazungumza na walimu na wanafunzi tu, lakini ndio hali ya wakati ule ilivyokuwa. Kwa hivyo, haiwezekani masuala yale yaendeleo mpaka leo.

Mhe. Spika, tunashukuru sana baada ya Mhe. Rais Karume kupata ushindi na imani ya wananchi yeye akachaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, basi tukaanza kujipanga. Tulipata misukosuko mingi, pamoja na yeye Rais, kwa kuanzia pale mwaka 2000. Lakini kadri siku zilivyokuwa zinakwenda kwa imani na uwezo mkubwa ambao Mwenyezi Mungu alimjaalia Rais wetu, akatandika misingi ya kujenga Zanzibar. Misingi ya kuimarisha wananchi na uchumi wetu hadi leo tunavyozungumza hapa mwaka 2010.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mimi nilikuwemo kwenye serikali kwa muda mrefu kwa kiasi. Miradi ya maendeleo katika kipindi hiki cha mwaka 1995 mpaka 2000 haikupatiwa fedha, kwa sababu washirika wa maendeleo na mabalazi hawakutaka kutusaidia kutokana na hali ilivyokuwa. Mimi ni shahidi niko afisini nikiwa Naibu Katibu Mkuu, Balozi wa Sweden amekuja afisini kumwambia waziri tumeamua tusikusaidieni, hivi hivi, kwa sababu hali ya nchi haiko katika hali inayoridhisha.

Mhe. Spika, tutizame baada ya Mhe. Rais Karume baada ya kupata madaraka kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na wananchi. Mhe. Spika, washirika wa maendeleo kuanzia mwaka 2001 hadi leo wameisaidia sana Zanzibar, na maendeleo yamepatikana. Haya yamethibitishwa hata chama cha upinzani kwamba Rais Karume amefanya kazi nzuri na anastahili kupongezwa.

Mhe. Abass Juma Muhunzi kazungumza hapa kwamba tulipinga hata lile ambalo lilikuwa zuri ambalo wewe mwenyewe unaliamini ndani ya moyo wako, lakini kwa sababu ya msimamo tu wa itikadi ya chama. Mhe. Spika, mimi hapa hata sera yangu ya elimu haikuungwa mkono hapa. Nikawatizama jamani waheshimiwa sera hii ni kwa ajili yetu sote. Lakini juzi tumekwenda

Micheweni Alhamdulillah Rais wangu anazungumza pale, nikamuona Sheikh Suleiman yuko pale mwakilishi na Bwana Ali Tara - Mbunge yuko pale alihudhuria kwenye sherehe ile, basi nikamshukuru Mwenyezi Mungu. (*Vicheko*).

Mhe. Spika, niruhusu kidogo pamoja na muda. Kuna watu wawili walipotewa hapa mjini washamba kama mimi. Walikuwa maeneo ya Shangani wametoka Makunduchi, nitasema Kimakunduchi ikifika wakati vile alivyomwambia mwenzake, kwa ruhusa yako Mhe. Spika, nadhani unakifahamu. Katika kupotea watu wale, mmoja akawa analia kwa makelele, nikisema kwa makelele ndio kama vile Mhe. Abass alivyofanya. Akamwambia mwenziwe, “nakwambiaje usilie nami nalia hea kati kwa kati?”. Kumbe yule anayelia kati kwa kati ndiye anayelia zaidi, maana hata pumzi hazipati, angalau yule mwengine akilia anatoa sauti.

Mhe. Spika: Nadhani haihitaji niwe mtapta wa hayo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Hata Mhe. Juma Duni kafahamu, maana naona kacheka, ni mshamba mwenzangu. Kwa hivyo, na sisi yale yalikuwa yanatusononesha jamani kabisa Mhe. Spika, hatuwezi kabisa kurudi. *That error has gone.*

Wallah, siwasifu watu tu kwamba nawasifu. Mhe. Hamad Masoud nisamehe nitakayoyasema, alikuwa mtu mmoja ambaye alikuwa hajanielewa. Lakini tumekwenda mpaka tumefahamiana na kuelewana. Mhe. Haji Faki Shaali ni *very scientific* kwa ku-*criticize*. Lakini Mhe. Haji Faki huyu na aseme aje anisute mimi, kama hatujawahi kushirikiana pamoja tukatembea kwenye jimbo lake lote la Mkanyageni, katika skuli zote za jimboni kwake mguu kwa mguu tulikwenda kutembea, kwa sababu gani tulishirikiana vizuri. Sasa kama yale yalikuwa yanatendeka si kwa jina lako kificho ficho hapana. Leo yamejitokeza dhahiri yanatendeka haya na waheshimiwa wengi hivyo tupo. Mimi nafurahi sana.

Mhe. Abass Juma Muhunzi alisema hapa, hudai mambo hapa tufanyeni hivi na hivi, tunapanga basi tukutane jimboni. Ukenda kule Mhe. Abass humkuti, pengine yupo. Aah! Nilikuwa na dharura kubwa, tena mtu akishakuambia hivyo, humwambia basi haya. Kwa hivyo, tumefika mahali ambapo Rais Karume ametengeneza mazingira mazuri ya nchi yetu. Wapinzani, Kiongozi wa Upinzani, Katibu Mkuu wa CUF wakasema aah! Jamani tena hapana, twendeni wamemtambua Rais wetu. Tunawapongeza sana kwa hatua hiyo ambayo wameichukua. (*Makofi*).

Mhe. Spika, yakakubalika yaliyokubalika. Tarehe 05 Novemba, 2009 tumefungua historia ya nchi yetu. Kama nilivyosema hatuwezi wala hatuwezi.

Nakumbuka kama leo Mhe. Spika, nilipangiwa nikafunguwa Skuli ya Shungi kama leo nakumbuka niko Pemba. Siku ya pili nakwenda kuifungua Skuli ya Shungi, Mhe. Spika, nafika karibu ya kupinda kuingia pale kuelekea Skuli ya Shungi imeshachezea moto, imepigwa moto na ilikuwa ni ya makuti tu, imechomwa moto. Hee! Watoto wakanikamata mkono, nilikwenda. Mhe. Waziri sisi tutasoma wapi skuli imeshachomwa moto, maskini watoto wadogo. Nikajipiga mwaka 2000 sikuwa na pesa kwa wakati ule za kutosha, nikahangaika hivyo hivyo tukawajengea madarasa 4 mapya. Leo ninafuraha kusema kwamba jana tulipokuwa tunapitisha matokeo ya mihani. Afisa Mdamini anasema kwamba tunaomba kufungua *form three* Skuli ya Shungi, sio jambo dogo jamani hili. Sio darasa la tatu hapana *form three* ifunguliwe Skuli ya Shungi leo. Tumeongeza kule Birikao, Mzambaru takao *form three* zinaongezeka tu. Sasa wanafunzi wanapasi kwa nini tusiwapeleke.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hali imekwenda mpaka juzi yamefanyika mazungumzo haya. Sote tuna wajibu wa kuyaangalia kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. Lazima hili tuliweke mbele kabisa. Wenzangu waliotangulia wamesema hivyo. Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban nakushukuru sana umetoa ufafanuzi na wewe ni hodari sana wa kutoa ufafanuzi. Ndio maana nadhani ukapewa Wizara ya Katiba na Utawala Bora, ulitulia. Hata na mimi najitahidi nitulie. Maana yake haya maji nimeletewa sijayanywa kwanza, lakini Mhe. Spika, nitakunywa.

Sasa Mhe. Spika, kuna masuala haya yamejitokeza hapa. Lakini kama alivyosema Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, kwamba yote haya tunayoyazungumza hapa. Kwa sababu sisi tulipokwenda majimboni tuliwaambia wananchi wetu tuchaguweni tutafanya hili na hili ili kuwaleteeni maendeleo kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu na kwa maendeleo ya wananchi wetu, tuna mikataba nao. Sasa kama kuna jambo zito ambalo na sisi limetukwaza au tunalo na liko kwenye vifua vyetu, hatuwezi tukakaa nalo hapa tu tukaliamua. Jambo hili zito la marekebisho yoyote ambayo yatakuja hapa hapa ni lazima tulirejeshe kwa wananchi wenyewe. Yote hayo yatakuja (*Makofi*).

Mhe. Spika, suala la kura ya maoni ambalo mhesimiwa mwenzangu aliyetangulia aliona kwamba halina haja, tuwe na kitu kama *transition government*. Mimi nasema suala hili lifanyiike kama lilivyopangwa kwa utaratibu wa kwamba marekebisho haya yote, mabadiliko yote yatakuja baada ya uchaguzi wa mwaka 2010. Nasema tena uchaguzi umepangwa Oktoba utafanyika, marekebisho haya mengine, sisemi haya ya *transition government*.

Ninachozungumzia hapa tutafanya utaratibu kwamba kuna marekebisho ya Katiba ya mambo fulani fulani hapa, lazima hayo mengine yafanyike kwa ajili ya kuandaa mustakabali wa baadae.

Kinachofanyika hapa Mhe. Spika, ni kwamba CCM na Rais mwenyewe keshatamka kwamba Katiba hairuhusu vipindi vitatu, lakini Katiba sio msahafu vile vile inaweza kurekebishwa, chochote ambacho kinahitaji kurekebishwa kinaweza kurekebishwa. Haya yote ambayo tumezungumza, na mwenzangu kazungumza hapa niyataje.

Mhe. Spika, bila shaka mimi nakubaliana na lile la mwanzo alilosema Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban kwamba, atakuwepo Rais, haya ndio makubaliano ya CCM na kweli tuliyasema na tulikubaliana. Mimi ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa vile vile. Tunachofanya ni nini, ni kwamba Rais atakuwa ni yule ambaye ameshinda katika uchaguzi mkuu na atakuwa Rais mtendaji. Sasa tulikubaliana kwamba vyama vyote viwili vilikubaliana kwamba kutakuwa na Makamo wa Rais wa kwanza na wa pili.

Mhe. Abass Juma Muhunzi katika *point* yake aliposema kwamba huyo wa kwanza kwa nini asiwe yeye. *This is very clear*, kwa nini asiwe yeye kwa sababu gani chama kilichoshinda kilikuwa ni cha yule Rais aliyekuwepo madarakani. Kwa hivyo, yule Makamo wa pili ambaye yuko ana-*belong* na chama kile ndiye atakayeweza kuendelea kumrithi Rais aliyekuwa madarakani. *What I understanding* ndivyo ilivyo, kwa sababu yule wa kwanza ha-*belong* na chama kile, anaye-*belong* na chama kile ni yule Rais wa pili. Kwa hivyo, suala la msingi hapa Mhe. Spika, tujitahidini katika suala hili kuyaangalia yale ambayo ni muhimu kuyazingatia.

Suala la pili ambalo amelizungumza Mhe. Samia Suluhu na mimi namuafiki sana, katika vile vipengele ambavyo vimeelezwa cha pili. Nitamke kwamba

Kipengele cha (ii). Litamke kwamba Muundo wa Serikali ya Zanzibar uwe na Serikali ya Umoja wa Kitaifa na inayohusisha vyama vyote vya siasa vilivyomo katika Baraza la Wawakilishi na kwamba viongozi wa serikali watokane na uwiano wa kura za Rais katika uchaguzi mkuu”.

Mhe. Spika, suala hili waamuzi ni wananchi.

Kipengele cha (iii). Litamke kwamba Serikali hiyo ya Umoja wa Kitaifa itakayoundwa itaendelea kuheshimu na kuthamini misingi mikuu ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964 kama ilivyotangazwa na Rais wa kwanza wa

Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Marehemu Mzee Abeid Aman Karume hapo tarehe 8 Machi, 1964”.

Mhe. Spika, hili ni muhimu sana.

Kipengele cha (iv). Liweke utaratibu utakaowezesha wananchi wa Zanzibar kushiriki kwa njia ya moja kwa moja kutoa ridhaa yao kuunga mkono mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa njia ya kura ya maoni *referendum*, na kwamba kura hiyo ya maoni iwe imeandaliwa na kufanyika si zaidi ya mwezi Mei 2010, au liweke utaratibu mwingine kwa njia ambayo Wazanzibari wenyewe kwa kupitia wawakilishi wao waliowachagua wataona inafaa”.

Mhe. Spika, ni lazima twende kwa wananchi tukawasikilize na watupe maoni yao wananchi, halafu tutarudi tutakuja kupanga hayo mengine.

Kwa hivyo, ninachosema Mhe. Spika, sina haja ya kurejea wenzangu yote waliyoyazungumza. Lakini ninachosema ni kwamba suala hili ni zuri, tushirikiane vizuri la msingi ni kwamba kila pale ambapo tutahitajia kutoa maamuzi mazito kama haya ni lazima turudi kwa wananchi. Mimi nakubaliana na Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban yale yote ambayo ameyazungumza tuendelee kuyaunga mkono kwa sababu yana mustakabali mzuri.

Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Nilitangulia mapema kumtaja Mhe. Asaa Othman Hamad na baada ya yeye kama muda utakuwepo tumsikilize Mhe. Haji Mkema Haji. Nafanya hivi kwa sababu majina yaliyoletwa maombi mapema kwa kweli mengi yalikuwa ni ya viongozi kutoka serikalini, sitaki ije ionekane kwamba ala, mbona anawapa wa serikali watupu. Kwa hivyo, baada ya yeye atakuwa ni Mhe. Haji Mkema Haji. Ahsante sana.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, na mimi naomba kutumia fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na huruma kutujaalia sisi sote Wajumbe wa Baraza lako tukufu uhai na uzima na kutufikisha leo kuja kujadili na hatimae kuridhia jambo kubwa la kihistoria ndani ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Kabla ya mchango wangu Mhe. Spika, mimi nitakuwa na mchango wa jumla jumla kwani waliotangulia nawapongeza sana kwani wamefanya kazi nzuri. Niseme

mimi Asaa Othman Hamad Mwakilishi wa Jimbo la Utaani kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wangu naiunga mkono hoja hii. Baada ya kusema hilo, Mhe. Spika, nije kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba siku ya leo ni siku inayosubiriwa kwa hamu na Wazanzibari wasiopungua milioni 1.2 walioko nje na ndani ya nchi yetu. Ni vipi wawakilishi wao ama watainyanyua Zanzibar ieleo kwenye neema ili iweze kuonekana kwenye kioo cha kiulimwengu kimaendeleo, kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mhe. Spika, mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa kutufanyia kazi nzuri na niseme hatuna cha kumlipa lakini yuko tajiri wa kumlipa ni Mwenyezi Mungu peke yake. Mhe. Spika, nasaha yangu kwa Waheshimiwa Wajumbe dhamana tuliopewa na wananchi wetu, dhima tuliyoikubali kwa Mola wetu isije ikatusuta siku ya siku. Ni kwamba tuna kila sababu ya kuilea nchi hii na wananchi wake kwa yote mema na kujitahidi kuyaepusha mambo mabaya.

Mhe. Spika, katika kufanya hilo nyenzo zetu kuu ni ukweli, haki, huruma na amani. Mhe. Spika, katika hili naomba sana tusitizamane nani atakuwa nani, hakuna sababu ya umimi kwani nchi ni nchi yetu, serikali ni serikali yetu kwa hivyo tuna wajibu wa kuijenga sote kwa mashirikiano ya pamoja. Vyama vitaendelea kuwepo, vitakuja vitapita na vitamalizika na Zanzibar itaendelea kuwepo milele na milele. Katika kutekeleza hili vyama tusivipe nafasi, ubinafsi wa aina nafasi tusiukaribishe Waheshimiwa Wajumbe kwani tukifanya hivyo hatutofika tulipokusudia kwa kuipata Zanzibar tuitakayo. Namwambia ndugu yangu Mhe. Mahmoud Thabit Kombo hufikirii kumuona Mhe. Asaa kuwa Naibu Waziri wa wizara yako, na nataka kusema Mhe. Haroun haoni tabu kuja kumuona Mhe. Rashid Seif Suleiman ni waziri badala yake yeye, ndio inawezekana kwani ilikuwaje yeye awe waziri asiwe yeye mwenzake. Mhe. Spika, ni kwamba hakuna mwenye hatimiliki ya hiki ama kile, tunahakimiliki ya sote kwa vyote.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba tuna dhima nzito na leo ni siku yetu ya kuandika historia mpya kwa nchi yetu, kazi waliyoifanya wazee wetu ya tarehe 12 Januari, 1964 matunda yake tunayafaidia sote leo. Kwa bahati mbaya tulivurugikiwa hapo kati kati, lakini kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu anavyowapenda Wazanzibari Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Mhe. Amani Abeid Karume, Mwalimu wetu Ndugu Seif Sharif Hamadi kwa mapenzi tu ya Mwenyezi Mungu walikutana wakazungumza tarehe 05/11/2009 matunda yake tunayashuhudia hadi sasa na inshaallah Mwenyezi Mungu ayajalie yadumu.

Mhe. Spika, wenzetu kwa maneno ya leo wameshakosha mikono, kazi imebaki kwetu. Mhe. Spika, ni imani yangu ya dhati kwamba hii kada yetu ya Wajumbe

wa Baraza lako tukufu hapa ndio kiini cha yote yale yaliyozungumzwa na viongozi wetu, ni vipi tutayashusha kwa wananchi huko waliko ili wayafahamu, wayaelewe na waweze kuyatekeleza. Hilo lipo mikononi mwetu Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, nitaendelea kurudia hili kwamba umimi tusahau katika hili kwani hatutofika pahali hivyo tunahitaji kwenda mbele kwani tumepitwa sana. Mhe. Spika, msokotano na mvutano wa siasa mbovu tulizozirithi, historia zetu za kisiasa zimefika pabaya sana hapa Zanzibar. Hii ni hidaya ya Mwenyezi Mungu ametuletea, nadhani Mwenyezi Mungu anajua bora, lakini nawafananisha Wajumbe wa Baraza hili na wale watu ambao huonekana na wao Makka wanahiji ilhali hawakufunga safari ya kwenda Makka.

Mhe. Spika, ulijipanga kwenda Hijja kwenye ibada kuu na umerudi salama inshaallah na sisi Mwenyezi Mungu atuite tuitike, lakini kuna watu hawakuwa na mpango kabisa wa maandalizi ya kwenda Hijja, lakini kutokana na nia yao njema, usafi wa nafsi zao na umchaji wao Mungu sio ajabu ulipata tabu kuwafananisha iwe yule siye mheshimiwa fulani. Hii ni hukumu ya Mwenyezi Mungu na yeye kumlipa faida ya Hijja ilhali hajenda Hijja. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu nasema tumepata nafasi hii ya upendeleo kwetu sisi binafsi na wale tunaowaongoza, tafadhalini nakuombeni sana nafasi tuitumieni kwa faida ya watu wetu na maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa nini Zanzibar leo tushindwe haiwi Rwanda, Burundi wameweza huko kuna halaiki ya watu walipotewa leo wanakunywa maji kwenye nyumba moja ya kutunga sheria, wanabadilishana mawazo, mabaraza yameundwa mpaka vijijini mtu kapoteza mume lakini bado anampa mkono mwenzake na wakati anajua kwamba amehusika kwenye mauaji hayo, anamwambia nimekusamehe. Hilo ni zito sana watu ambao wanazungumza lugha tofauti na wenye dini mbali mbali wanafahamiana ije iwe sisi Wazanzibari. Mhe. Spika, kwa kweli tutakuja kuchekwa sana, lakini sio cheko tu kwani litamalizia kwa watu Mwenyezi Mungu sijui tutakwenda kumwambia nini kesho. Mhe. Spika, hili ndio la msingi kuliko cheo cha aina yoyote ulichonacho leo.

Mhe. Spika, mimi nimesema naunga mkono sina haja ya uchambuzi wa kipi kizuri kwani kwangu mimi vyote ni vizuri nadhani kuna ya kuboresha ndani ya waraka huu. Yale yatakayoonekana na Waheshimiwa Wajumbe hayo ni ya kuongezwa nyama mimi nakubaliana nayo, haya ni ya kupunguzwa hakuna tatizo. Mimi ninachosisitiza ni ukweli juu ya hili, ubabaishaji juu ya hili mtu atajibabaisha mwenyewe. Mhe. Spika, maridhiano ni nyenzo ya kuponyesha mahusiano yaliyovunjika kwa kuondoa chuki, uadui na uhasama uliodumu kwa miaka mingi.

Mhe. Spika, tunahitaji mazingira bora juu ya utekelezwaji wa hili, serikali iandae mazingira ya kutekelezwa haya. Mhe. Spika, ndani ya waraka huu kuna kamati imetajwa juu ya hiyo taasisi itakayopewa dhamana hiyo ili tuweze kwenda salama kama tulivyokubaliana.

Mhe. Spika, mimi niseme wote kwa pamoja tunakubali kwa sababu ndio katiba yetu inavyozungumza. Mamlaka ya nchi hii ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa serikali kufuatana na katiba utatoka kwa wananchi wenyewe. Hili sina ugomvi nalo hata kidogo, tutapata kiini ya nyoyo hizi za Wazanzibari ambazo zimevurugika kwa muda mrefu basi isimamiwe kwa ukweli na msingi wa yote ni ukweli, uadilifu wa hali ya juu na kuitakia kheri na mema Zanzibar na Wazanzibari wake. Mhe. Spika, kadri nitakavyozungumza naogopa nisije nikalia.

Mhe. Spika, naomba ili na sisi tuandike historia mpya ya Zanzibar, leo Alhamis ya tarehe 28/01/2010 Zanzibar ya kimaendeleo leo iwekwe Makumbusho na wakumbukwe Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba tumeweka misingi hiyo ya kuipata Zanzibar ya kimaendeleo baada ya mvurugano wa miaka iliyopita, lakini wajumbe hawa walifanya kazi hii na tunawashukuru. Mhe. Spika, watoto wetu tujetuarithishe nchi ya kimaendeleo na nchi iliyojengwa mshikamano, maridhiano, maelewano ya nchi yao yaliyotukuta sisi yarabi usitujalie tena kuyarejesha. Mhe. Spika, ni kwamba tutie nia ya kuyakataa kwamba maovu hayastahiki kwa binadamu kuwa nayo na unafiki tujue ni maradhi donda ndungu litakalokupeleka motoni siku ya kيامa.

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa kusema kwamba walioko nje ya jingo hili, walioko nje ya nchi hii, masikio yao yote leo yako Zanzibar nakuombeni Waheshimiwa Wajumbe tofauti ndogo ndogo tuzifute ili Mwenyezi Mungu atujaze rehema zake njema, aijaze nchi hii amani na utulivu endelevu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Asaa alipokuwa anaanza kusema cheo cha Mhe. Mahmoud Thabit Kombo labda kiende kwake akawa anazunguka zunguka nilikuwa nafikiria ananyemelea na hiki kiti. Lakini Mhe. Abubakar alisema hiki kiti kina mambo eti kwa sababu siku moja Mhe. Ali Mzee Ali alipata homa. (*Kicheko*).

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunioreshesha kuchangia hoja hii. Mhe. Spika kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Koani

mimi Haji Mkema Haji Mwakilishi wa Jimbo la Koani nasema wazi siungu mkono hoja hii ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary kama hivi ilivyo.

Mhe. Spika, sasa nitachangia haraka haraka kwa sababu muda uliopo ni mchache na wengi wanahitaji kuchangia. Mhe. Spika, sababu ambazo zinanifanya hivyo kwanza katika ukurasa wa kwanza kifungu cha 1-2 chote hiki kinaelezea sababu zilizomfanya Mhe. Mwakilishi kuleta hoja hii ni maridhiano ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Maalim Seif Sharif Hamad. Maridhiano ambayo mimi siyajui kwa sababu baada ya kikao cha tarehe 05/11/2009 Maalim Seif Sharif alikwenda katika Kiwanja cha Demokrasia akahutubia lakini hayo maridhiano hakusema, alilosema ni kwamba amemtambua Rais Amani na atashiriki katika serikali hii kama mwananchi zaidi kwa kujenga nchi. Pia na Mhe. Rais naye alikuja akatueleza hivyo hivyo hakukuwa na zaidi.

Mhe. Spika, pengine mazungumzo yalikuwepo baina ya Rais Amani na Maalim Seif kwa sababu watu hao muda mwingi hawakukaa pamoja na walizungumzia hali ya karafuu, hali ya uchumi pengine wamezungumza waliyoafikiana huko sisi hatuyajui. Mjumbe anayeleta hapa hoja kwenye Baraza tuyazingatie maridhiano hayo rasmi basi angalau angekuwa na vielelezo kwamba maridhiano yenyewe yalikuwa ni haya nataka wajumbe muyape nguvu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, vipengele hivi mimi nashindwa kwa niaba ya wananchi kutoa nguvu hizo juu ya maridhiano hayo.

Mhe. Spika, bahati mbaya au nzuri viongozi hawa ni watu wakubwa, wazoefu, wana siasa na wenye nyadhifa kubwa. Maalim Seif amekuwa mwalimu kwa siku nyingi amefikia mpaka Waziri Kiongozi, Dk. Karume na yeye ni mwana siasa mkongwe ni Rais kwa muda wa miaka 10. Pia amepata *degree* za Falsafa mbili moja kwenye Chuo cha Kairuki cha Tanzania na chengine kule South Carolina. Chuo hiki ni kizuri na tunajua sifa yake kwa sababu na mimi nimesoma huko. Kwa hivyo, sifikiri Mhe. Rais awe na maridhiano mazuri wasijue njia za kufanya.

Kwa hivyo, hii ni hoja ambayo mimi siwezi kuwapa maridhiano kwa sababu wangeweza kuandika tumekubaliana hivi na wakaweza kuwaambia wananchi. Tulilokubaliana ni kuwa wamenitambua kwa hivyo kilichobakia basi zile nafasi zangu mbili nipe amepewa. Mhe. Spika, nashukuru ndugu yangu Mhe. Nassor Ahmed Mazrui yupo, ndugu yangu Juma Duni Haji yupo kutokana na matokeo hayo. Lakini suala la kujenga nchi hili ni wajibu kwa mwananchi Maalim Seif na sote madhali tumesharidhia kakubali kuwa alishindwa sasa hivi ni wajibu wake kujenga nchi, mwananchi yeyote ni wajibu wake, *fiydmatul-autwani fardhi alal-isani*, kujenga nchi ni wajibu wa mtu si lazima tena kuwe na mapatano mengine, kujenga nchi ni wajibu wa mtu Warabu wanazungumza.

Mhe. Spika, hili mimi nasema hiyo haijawa hoja kwangu, lakini pia inazungumzwa basi katika mazungumzo hayo hayo kuwoko na Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, si suluhu, penye mgogoro hiyo si suluhu. Tuna mfano mzuri wa Zimbabwe, Morgan Morgan Tsvangirai na Mugabe bado wanatafunana meno, Kenya hapo Raila Odinga na Kibaki wananyang'anyiana yule anataka madaraka kule na huku, lakini machafuko na amani hizo ndizo sifa za nchi hasa hii Zanzibar. Iko namna tukae tutafute njia mjarab kwa sababu hapa hata wakati wa ufalme palikuwa na vita hapa ugomvi Washihiri na Wamanga, Mshihiri akigusa tu kishakula panga au bunduki. Waarabu na Wamanga wametokezea hapa hapa wakati wa serikali ya wakati huo, vita vya ng'ombe.

Kwa hivyo, haya mambo baadae yanakuja tukatafuta njia ya suluhu ili tukayamaliza. Mhe. Spika, kutokana na historia nafikiri dawa yake tuwe na chama kimoja. Kwa sababu tulipokuwa katika chama kimoja tangu 1964 mpaka 1992 hapakutokezea matatizo yoyote Maalim Seif alikuwa mwalimu, akachaguliwa kuwa waziri hajjui, kuondoka pale alikuwa anataka kuchukua baiskeli akaambiwa wacha hiyo kuna gari hapa.

Kuna mchukuzi pwani mzee Sharif kule alibeba lakini alionekana na sifa na uwezo akaambiwa wacha gunia kuwa Naibu Waziri wa Bahari, Meli na Uvuvi. Pia jimboni kwangu nilikuwa ninaye ndugu Makame Simai alikuwa akipiga dawa majumbani, akachukuliwa akawa Waziri mdogo wa Majenzi na Nyumba. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tukenda namna hii tutakuwa na utaratibu mzuri wa kupata hivyo vyeo ambavyo tunavitaka. Kwa hivyo, mimi nafikiri ni bora twende kwenye chama kimoja.

Mhe. Spika, mheshimiwa mtoa hoja ni Mbunge wetu tumemchangia hapa. Hoja ya vyama ipo katika Jamhuri ya Muungano basi tunamuomba mheshimiwa akapeleke hoja kwanza. Huu utaratibu wa multipartism system kwa Zanzibar unatumiza na tangu kuja kwa mfumo huu ndio unaosababisha haya yote, maana tusitafute wapi tulipoangukia, tutafute wapi tumejikwaa.

Mhe. Spika, ninamuomba mtoa hoja tusitafute wapi tulipoangukia, tumejikwaa wapi? Tatizo hili tumelipata baada ya kuingia mfumo wa vyama vingi hapa kwetu. Ninafikiri dawa ni kurejesha ule mfumo wa chama kimoja ambao unatoa na huu hatutopata serikali ya umoja wa kitaifa. huu tutapata serikali ya kitaifa ambayo itakuwa madhubuti zaidi kuliko hii.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi mawazo yangu dawa moja ni hii lakini tunajizungusha huko. Mhe. Abubakar Khamis Bakary kama ni Mbunge wetu wa Baraza hili bado ana nafasi ya kutoa hoja kwenye Bunge la Muungano, kuiambia serikali kwamba huu mfumo wa vyama vingi sisi Zanzibar

unatumiza, tunagombana turejeshe mfumo wa chama kimoja tu. Hii itakuwa ndio dawa, watu wote watakwenda kwa mujibu wa sheria na wananchi watakwenda vizuri na kutakuwa hakuna ugomvi.

Serikali hii ya ushirikishi lakini itakuwa bado ya vyama vingi, mapande yapo na kila mmoja atataka ashinde. Shetani kama alivyozungumza Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora atakuwepo, mahala popote patakapokuwa na ushindani bado tatizo litakuwepo Mhe. Spika.

Kwa hivyo mimi hii serikali imetajwa na kuungwa mkono lakini mimi bado fikra zangu Serikali ya Kitaifa itakayojengwa chini ya mfumo wa chama kimoja ndio sahihi hasa kwa Wazanzibari na tutaondoa mashaka yote.

Mhe. Spika, mambo haya sitaki yafanywe haraka haraka kwa sababu siku zote haraka haraka haina baraka, wazee wamesema mambo mazuri hayataki mapapara, mwenye kufanya papara hadiriki kula tamu. Kwa hivyo, mambo yote haya inafaa tumalize hapa tuna shughuli nzito za uchaguzi, wacha tuendeleo tumalize uchaguzi wetu tushughulikie haya ili tufanye uchaguzi salama.

Mhe. Spika, eneo jengine bado mimi ninakubaliana na wazo kuwa sisi Baraza tusijitupe meno, tumepewa nyanda tukachukua shubiri. Hili jambo ni zito, kwa hivyo suala la kupelekwa kwa wananchi, mimi hili ninaliunga mkono asilimia 100.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe huyu kapitia hospitali na daktari hukutisha kwa maradhi uliyonayo ili utumie dawa vizuri. Endelea mheshimiwa.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, katika kifungu cha 3 ukurasa huo huo, basi pameelezwa hapa kwamba mfumo huu wa serikali ya kitaifa utazingatia uwiano kwa mujibu wa kura za uchaguzi wa Rais.

Mimi nimetoa mawazo yangu lakini kwenye kutoa mawazo kuna wengi huenda nikashindwa, basi kama nitashindwa wazo langu, hivyo mimi ninasema uzingatie uwiano wa viti katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, eneo jengine ni katika marekebisho ambayo ametaka yafanywe humu. Kifungu cha 3, 9, 1 haya yote ya kubadilisha Katiba basi yangojee ridhaa kutoka kwa wananchi. Haya yangojee kwa sababu tusikate mbeleko kabla mtoto hajazaliwa. Kwa hivyo ni vyema tuwape muda na tusifanye mambo kama ya kuweza kuwashawishi wananchi juu ya hili, wawe huru. Tukianza kufanya hivi, sijui iwe hivi tutakuwa kama ule uhuru na uwazi hatuwapi wananchi katika kupiga kura zao za maoni.

Mhe. Spika, katika marekebisho ya Katiba ambayo Mhe. Mjumbe ameyafafanua kwenye ukurasa wa 6, hasa katika muundo wa serikali. Lakini pale aka-*quote* maudhui na dhima ya kupata serikali yenye lengo ya kufikia demokrasia chini ya misingi mikuu iliyoekwa na mapinduzi ya 1964 ambayo ilikuwa kwanza ni kutaifishwa ardhi. Wajumbe hapa wamezungumza hapa kwamba hivi sasa serikali na wala hatufikirii, kwa sababu ndio kwanza tunawahifadhia watu waliopata wawe nayo na wanapewa hati.

Kutaifishwa nyumba, mimi sikubaliani nayo, waliopewa kwa wakati huo wameshakuwa nazo na sasa hivi iwalinde. Elimu kwa bure iendelee kwa Mhe. Haroun Ali Suleiman, matibabu bure Mhe. Sultan Mugheiry endelea. Kupigwa marufuku uwekaji wa bondi na rehani Mhe. Spika, hii imepitwa na wakati.

Hivi sasa kwa upande wa ardhi tunaweka reheni kwa sababu tumeweka sheria maalum ya *Land Tenure* ya utawala wa ardhi, mtu anaweza kuweka rehani miaka kumi, thalathini na idara imewekwa makusudi ili aweke ardhi yake aweze kufanya maendeleo yake. Kwa hivyo hii imepitwa na wakati katika serikali hiyo haimo.

Lakini (f) Mhe. Mjumbe hakuitazama kupigwa marufuku vyama. Kwa hivyo na chama chako kitakuwa hakipo mheshimiwa. Kwa hivyo kuanzia leo bora utoke, useme leo unaingia Chama cha Mapinduzi. Hiyo serikali inayokuja mheshimiwa anayoizungumza, inazungumza kupiga marufuku vyama. Kwa hivyo ajue kuanzia leo basi aseme mimi siko CUF ninaingia CCM.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo Mhe. Rama ameyazungumza mengi kuhusu marekebisho hayo. Mimi Mhe. Ramadhan Abdulla, mimi ninakubaliana nayo ninayaunga mkono yale marekebisho yakikubaliwa mimi hapo ndio mwisho nitaunga mkono.

Mhe. Spika, ninakushukuru. (Makofi).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninakushukurani sana Wajumbe wote, ni historia ambayo pengine ni mara ya kwanza kujadili jambo zito tunacheka na kufurahi. Inanivutia sana na kwa kweli itatuongozea shughuli zetu humu ndani, tutaongoza vizuri wananchi huko nje. Ninakushukurani tuendelee kuzungumzia hoja hii katika mazingira ya aina haya ili tufike pahala tuamue kitu ambacho kitakuwa kinafaa kwa madhumuni ya wananchi wetu na sisi wenyewe tuliomo humu ndani. Basi tukapumzike na tuje jioni, saa 11.00 jioni. Ninaahirisha kikao hadi saa hizo

(Saa 7.00 mchana Baraza l liahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, leo nimehimizwa kuingia humu ndani maana Wajumbe wako tayari, maana si kawaida wakati mwengine huwa niko na wachache tu. kwa hivyo, nakushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe (*Kicheko/Makofi*).

Mhe. Omar Ali Shehe: Bismilahi Rahmani Rahim. Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia jioni hii kuweza kukutana hapa na kunipa uwezo na mimi kutoa mchango wangu wa maneno katika kuiendesha nchi yetu.

Vile vile nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kukubali kwamba hoja hii ijadiliwe katika Baraza lako hili. Mhe. Spika, katika kukubali kwako, naomba huu uwe ni mchango pamoja na sadaka yako kwa Wazanzibari (*Makofi*).

Kutokana na sadaka hii basi nimuombe Mwenyezi Mungu kwa kitendo hiki akuingize katika pepo yake (*Makofi*).

Mhe. Spika, chimbuko na msingi wa hoja ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary nadhani inayo historia ndefu. Historia ambayo ilianza na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi aliyoitoa wakati akizindua Bunge la Jamhuri ya Muungano hili tulilionalo.

Katika kipindi kile alisema kwamba anatambua kwamba katika visiwa vyetu vya Zanzibar kuna mpasuko mkubwa wa kisiasa, yeye aliahidi kwamba atahakikisha ndani ya kipindi hiki anaufanyia kazi mpasuko huo na hatimaye kuumaliza.

Kwa hivyo, hilo ndilo chimbuko hasa la hoja ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Tunatambua kwamba baada ya kauli ile ya Rais wa Jamhuri ya Muungano nini kilichofuata. Kwa kweli kilichofuatia ni Kamati ya Makatibu Wakuu iliyoundwa baina ya Mzee Yussuf Makamba na Maalim Seif Sharif Hamad walifanya kama walivyofanya na kufika walipofikia, pia yalitokea yaliyotokea.

Lakini baadaye Mhe. Rais Dk. Amani Abeid Karume kwa kweli aliona haja na umuhimu wa kulishughulikia suala hili kabla ya kumaliza kipindi chake cha ongozi.

Kwa hivyo, Dk. Karume alimkaribisha Maalim Seif Ikulu na kwenda kuzungumza pamoja na kunywa maji kama alivyozungumza. Lakini kitendo chao cha kukaa watu wawili pamoja ndicho kilichozua umuhimu na kutoa tafsiri kwa Wazanzibari, kwa kweli pale Wazanzibari wote kufuatia wale viongozi wetu wawili baada ya kukaa pamoja, basi Wazanzibari na wao wakaamua kukaa pamoja (*Makofi*).

Kutokana na hali hiyo, sina haja ya kutaka kujua kwamba kwenye mazungumzo yao kuna nini. Isipokuwa walikubali kukaa pamoja, basi hiyo inatosha kuwa viongozi wetu wamekubaliana na mengine yatafuata baadaye.

Mhe. Spika, nataka nikubali kwamba hatua aliyofikia Mhe. Rais haikuja kirahisi bila ya shaka naamini kuwa msaidizi wake wa karibu sana Mhe. Waziri Kiongozi pamoja na Mhe. Naibu Waziri Kiongozi, walichukua nafasi kubwa katika kumshauri. Naamini kwamba viongozi hawa wawili walimshauri na hatimaye Mhe. Rais alifikia hatua ile.

Sasa naomba Mhe. Spika kupitia kwako niwaombe hawa viongozi wawili Mhe. Waziri Kiongozi pamoja na Mhe. Naibu Waziri Kiongozi ambao tunao hapa, kwa bahati mbaya katika chombo hiki cha Baraza hatunaye Mhe. Rais.

Lakini kuwepo kwao na ninaamini na nataka niwaombe kwamba kwa hekma ile walioichukua kumshauri Rais, pia wachukue hatua au hekma ile ya kusimamia mjadala huu, ingawa Mhe. Spika ndiye mkuu. Isipokuwa watumie ushawishi wao katika kuhakikisha kwamba aliyoaifikiana Mhe. Rais Karume hayaendi kombo (*Makofi*).

Mhe. Spika, leo Zanzibar tuko katika hali ambayo kila mmoja anaifahamu na wala haihitaji kuhadithiwa. Kwa kweli katika jamii yetu tunao mgawanyiko mkubwa sana wa kisiasa. Katika hali tuliyonayo Mhe. Spika, ndugu wamekuwa hawazikani, nani atakataa hilo. Vile vile katika hali tuliyonayo watu wanakaribia wanafika pahala na kuuana na halijui hilo, ndugu kwa ndugu hawafahamiani kwa sababu ya siasa.

Siku moja pale Chake Chake mzee wangu alikuwa ni dereva wa serikali alinipakia kwenye gari yake, lakini wakati ananiteremsha pale walikuwepo watu, baada ya kuteremka na kuondoka basi wale watu walimwita yule mzee na kumuuliza je yule uliyemchukua unamjua ni nani. Basi baba yangu aliwajibu na kuwaambia hivi kwa alivyoniambia mama yake yule mimi ni mwanangu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, turekebishe hilo tatizo.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, alisema hivi yule anaitwa Omar Ali Shehe na Ali Shehe mwenywe ndiye mimi (*Kicheko/Makofi*).

Mhe. Spika, hiyo ndiyo hali ya kisiasa tuliyonayo katika nchi yetu.

Lakini si hilo tu kwa sababu hilo linatokea mitaani. Tukiangalia katika mazingira ya Baraza lako kwa kweli Wajumbe wako tunapata tabu sana, labda kwa hili leo nikushtakie.

Wakati tunapofika pahala inakuwa ni tabu baina ya Wajumbe wa Upinzani na Chama Tawala, yaani wakati mwingine unapoonekana unazungumza na mjumbe wa upande wa CCM, basi wenzako hukuangalia kwa macho mawili. Vile vile na kwa upande wa mjumbe wa CCM anapozungumza na mjumbe kutoka upande wa Upinzani naye huambiwa vipi umeshageuka (*Kicheko/Makofi*).

Mhe. Spika, hayo ndiyo mazingira maana yake sio mitaani na kwenye majimbo, hata katika eneo hili hali inakuwa ni hiyo. Kwa kweli siasa inatulea katika misingi hiyo. Mimi binafsi nilisema nadhani kwenye kipaza sauti hichi, kuna siku nilisema kuwa Mhe. Spika kama inaonekana jamii yetu inagawiga au inauhasama mkubwa sana na kama ikiwa chanzo ni siasa za vyama vingi, ilisema hapa vyama vingi vipigwe marufuku.

Kwa sababu vyama vingi ndivyo vilivyotuletea balaa katika nchi hii nakumbuka nilisema hapa. Lakini leo sithubutu kusema kwa sababu huu ni mfumo ambao unakubalika na dunia, yaani tukitaka au tusitake kwenda hivi.

Mhe. Spika, katika mfumo huu tunacho cha kujifunza na pia kuna mambo ambayo lazima tukubali kujirekebisha. Kwa kweli tukubali kubadilika, ili kwenda na wakati au hali halisi na ustaarabu uliomo ndani ya mfumo wa vyama vingi.

Mfumo wa vyama vingi kigezo chake ni kuitishwa kwa chaguzi. Mhe. Spika, kwa kweli chaguzi katika nchi yetu inakuwa ni balaa kubwa sana. kwa sababu chaguzi ndicho chanzo cha matatizo, vurugu, yaani chaguzi zimekuwa ni balaa kubwa.

Wazee wetu waliotoka kwenye miaka ya 1950 na 1960 mnavyo vielelezo vikubwa sana, mnakumbuka vizuri sana chaguzi za miaka ya 1957, au ule wa mwaka 1961. Lakini kwa sisi ambao tumo kwenye mfumo huu mpya tunakumbuka matokeo yaliyotokana na uchaguzi wa mwaka 1995, pia mwaka 2000 pamoja na yale 2005 tulishuhudia. Sasa tunaangalia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.

Mhe. Spika, lazima kwa sababu matokeo ya chaguzi zote zilizopita zimetoa matokeo mabaya sana na kuleta mgawanyiko mkubwa sana. Kutokana na hali hiyo, kwa hatua hii tuliyonayo na maridhiano nadhani tukae tufikirie tena upya, vipi tutaweza kukabiliana na uchaguzi unaokuja, ili yale yaliyotokea yasiyekujirudia tena yanatosha, tuseme yanatosha. *(Makofi)*

Kwa kweli ustaarabu wetu Wazanzibari uonekane hapo na wala tusikubali kurejesha yaliyopita.

Mhe. Spika, fursa ya maridhiano tuliyonayo ambayo baada ya mchakato wote Mhe. Abubakar Khamis Bakary ametuletea katika Baraza hili kama hoja. Kwa hivyo, napenda kusema kwamba hoja hii si ya CCM wala CUF, isipokuwa hoja hii tunayojadili ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary ambaye ni Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mgogoni.

Kwa sababu wakati mwingine watu ambao hawatuombei mema hujaribu kutanguliza vyama, kwa kuwa katika nchi yetu unapotaja CCM, basi tayari umeshamuweka mtu wa CUF akataye. Vile vile unaposema hii ni hoja ya CUF basi unamfasha mtu wa CCM akataye.

Kwa kweli katika sakata hili ambalo tunaendelea nalo, nadhani kwanza ilikuwa ikizungumzwa kwamba Chama cha CUF kinapeleka hoja katika Baraza. Hivi kweli Chama cha CUF ndicho kilicholeta hoja katika Baraza? Maana kama Chama cha CUF basi angelikuja Katibu Mkuu.

Isipokuwa baada ya kuonekana hii si hoja ya CUF sasa watu wakaigeuza mpira na kusema ni hoja ya CCM, yaani lengo ni lile lile kwamba chama kikikaa mbele maana yake kutakuwa na upinzani. Kwa sababu watu wanatafuta namna walete upinzani katika suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani sasa tuko kwenye njia panda, yaani Waheshimiwa Wajumbe tuko kwenye njia panda ama tukubali kwende kwenye uchaguzi wa mwaka 2010 mwezi wa Oktoba. Kwa hivyo, tutakapokwenda kwenye uchaguzi wa mwaka 2010 tuangalie matokeo yake nini, ikiwa haya tunayoyazungumza matatizo yanatokana na chaguzi.

Sasa tunapozungumza uchaguzi wa mwaka 2010 matokeo yake nini, yaani baada ya uchaguzi matokeo yake ni kitu gani. Njia ya pili tukubali tuitumie nafasi au fursa hii katika kujenga misingi ya mustakbali wa taifa letu. *(Makofi)*

Nadhani tufanye vitu viwili tukubali na tuseme kuwa uchaguzi mwezi wa Oktoba mwaka 2010, kwa vile kuna wengine miongoni mwetu tayari tumeshakuwa na imani kwamba tutakuwa X marais, mawaziri, wawakilishi.

Jambo jengine tufike pahala na tuseme basi ikiwezekana na wala hakuna kisichowezekana chini ya jua.

Kwa hiyo, tuutumie muda huu kwa kusema tukaa kwa ajili ya kujenga misingi ya kuweka mustakbali wa taifa letu. Kutokana na hali hiyo, yeyote ambaye Mwenyezi Mungu amemuandikia kuwa rais basi tayari ameshamtangaza. Vile vile kama kuna yeyote ambaye Mwenyezi Mungu amemuandikia kuwa waziri, basi tayari mwenyewe Subuhanahu Wataala ameshamtangaza. (*Makofi*)

Kilichobakia hapa ni utashi tu, kwamba kuna watu ambao walichukua fomu na wengine waliteuliwa lakini hawakuwahi kugombea nafasi. Kwa mfano, kuna wenzetu ambao waliwahi kuingia kwenye vyombo hivi na matokeo yake hawakumaliza kipindi chao. Kwa hivyo, nadhani tufike pahala tuamue kipi kipaumbele chetu.

Mhe. Spika, kwa maoni yangu nafikiri kwa wakati tulionao tuache mbali matakwa ya vyama vyetu na tuweke mbele matakwa ya utaiifa. Kwa kweli watu wote wanaoingia kwenye hatua za mpito kama hizi tulizonazo huwa na agenda maalum za kitaifa. (*Makofi*)

Jambo la kwanza la msingi cha kuzingatia suala la amani ndiyo iwe ajenda yetu. Jambo la pili Mhe. Spika, tujenge mazingira ya kuaminiana, yaani Wazanzibari tunalo tatizo la kutokuaminiana, bila ya kuaminiana hakuna chochote kitakachofanyika itakuwa tunajidanganya tu. Isipokuwa lazima tufike pahala kila mmoja miongoni mwetu viongozi, kama walivyoaminiana Maalim Seif na Rais Karume na sisi viongozi katika ngazi hii tujenga hali ya kuaminiana. (*Makofi*)

Ili tuaminiane basi lazima tuseme tusameheane yale tuliyokosana. Kwa sababu hatuwezi kujenga nchi bila ya kuaminiana na wala ya kusameheana kwa yale tuliyokoseana.

Jambo jengine ambalo ndilo kubwa zaidi kuweke mbele utaiifa. Kwa kweli kila kitu tuseme kwamba Uanzibari ndio mwanzo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi naamini sana kuhusu vyama na kila mmoja kati yetu anapenda sana chama chake ni kweli. Lakini tukiendekeza vyama Mhe. Spika hatuwezi kwenda mbali na wala kufika pahala. Kutokana na hali hiyo, nadhani vyama hivi katika kati ya miaka ya 1950 tulikuwa na vyama ASP, Hizibu, ZPP, ZNP na mwisho vilifika mwaka 1964, yaani wazee wetu walivipenda sana na leo viko wapi, vilipofika mwaka 1964 vikaambiwa hapa ni marufuku.

Kwa hivyo, kutoka 1964 mpaka 1977 mama yetu *Afro Shirazi Part* ambaye tulimpenda sana tulimuaga. Kwa maana hiyo, waliokuwa wana-*Afro Shirazi Part* waliingia CCM na waliokuwa wana-*Afro Shirazi Part* leo tunao wengi sana. Kwa kweli *Afro Shirazi Part* tuliipenda sana na leo iko wapi?

Mhe. Spika, kuanzia mwaka 1977 mpaka 2010 tunacho Chama cha Mapinduzi na mimi naomba kiendeleo kudumu. Lakini nina hakika kwamba siku moja kitapotea katika sura hii. (*Makofi*)

Vile vile kuanzia mwaka 1992 mpaka 2010 tunacho Chama cha CUF. Lakini ninaamini kwamba kuna siku Chama cha CUF nacho kitapotea. Kwa sababu vyama vilikuwepo, viliondoka, vyama vipo na vitaondoka. Lakini Zanzibar *always* itakuwepo, yaani taifa letu litakuwepo. (*Makofi*)

Kwa mfano, tulikuwa na wazee wetu na leo hatunao tena, Mhe. Spika leo tupo sisi na kesho hatutakuwepo tena na Zanzibar itaendelea kuwepo daima milele, yaani ardhi hii itaendelea au visiwa hivi vitakuwepo. Hivyo, nchi yetu kama hatukufanya upumbavu sisi wenyewe basi itakuwepo.

Kwa hivyo, tusiweke mbele sana maslahi ya vyama, ingawa tuzungumze siasa, sera pamoja na mikakati mingine. Lakini katika masuala yanayohusu taifa letu hili la Zanzibar, basi tuweke mbele sana utaifa kuliko kitu chengine chochote. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hoja ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary inazungumzia suala la kuunda Serikali ya Kitaifa. Nadhani sote tunakubaliana kuwa suala hili ni muhimu na mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu tunaliunga mkono kwa dhati kabisa. Hivi itakuwaje hapa Zanzibar tusiwe na Serikali ya Kitaifa, kwa sababu mazingira ya visiwa vyetu ni Unguja na Pemba ndio Zanzibar itakuwaje ufanye serikali ya upande mmoja na ule mwengine usishiriki.

Lakini hata vyama vyetu vilivyogawika, yaani tunavyo CUF na CCM na matokeo yake yanaonekana itakuwaje uwe na serikali iliyoundwa na chama kimoja usikishirikishe chama chengine. Isipokuwa tutaona kufanya hivyo ni ushamba wa kisiasa na sisi hatutaki tuwe washamba wa kisiasa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, jitahidi muda unakimbia sana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, hoja hii naiunga mkono.

Jambo la pili ni kuhusu Kura ya Maoni. Kwa kweli nakubaliana twende kwenye kura ya maoni, maana ya kura ya maoni ni kuwa wananchi mamlaka na hilo sina tatizo nalo na twende kwa wananchi. (*Makofi*)

Isipokuwa nitahadhrishe kitu kimoja Mhe. Spika, ndani ya mwaka 2010 tunapanga tuwe na Uchaguzi Mkuu, lakini tunapanga tuwe na Kura ya Maoni. Hivi unapomwambia mwananchi wa kawaida leo kuna kura, basi mwananchi roho imeshamruka. Kwa hivyo, nasema kwamba Kura ya Maoni isiyeikageuka kuwa ni balaa jengine.

Kutokana na hali hiyo, nadhani tutafute muda na kuharakisha hakuna maana. Isipokuwa tutafute muda muafaka wa kuitisha Kura ya Maoni. Kwa kweli ikiwezekana basi tuifanye kama tulivyokubaliana kwamba iitishwe mwanzo, lakini kuna haja ya kupata matayarisho ya kutosha, ili kura hii iwe huru na kila mmoja ashiriki katika kuchangia suala hili.

Mhe. Spika, matumaini ya Wazanzibari wote hakika leo ilipofika milango ya saa 6:00 kulizizima hata kunguru walikuwa hawaonekani, yaani watu wote wanafuatilia suala hili. Hatima ya suala hili liko mikononi ya watu 78, kwa sababu wazee wetu wameshamaliza kazi yao na wameshanawa. Sasa wajumbe sisi ndio tuliobeba dhima kubwa kwa watu wetu walioko nje na ndani ya nchi yetu, yaani hata wazungu na leo tunao wageni kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika, hakika watu wote duniani wanayo haja ya kuona kuwa Zanzibar inatulia, mshikamano unakupo, yaani watu wote wanayo *entrest* hiyo. kwa hivyo, ni jukumu letu tuliomo kwenye chombo hiki Mhe. Spika tuweze kurejesha matumaini ya watu wetu. Kwa kweli tuitumieni vizuri sana fursa hii, kwani tukiikosa fursa hii tutakaa miaka mingi ijayo hatuwezi kuipata.

Kutokana na hali hiyo, nawanasihi wajumbe wenzangu kwamba tuache kila tulilionalo na tuangalie mustakbali na turejeshe matumaini mema kwa watu wetu waliotuamini katika kutumikia kwenye chombo hiki.

Mhe. Spika, kwa kuwa muda wako unakwenda mbio sana, basi naomba niseme kwamba Mwenyezi Mungu aibariki Zanzibar, Wazanzibari, Watanzania pamoja na Tanzania yao, pia avibariki vyama vyetu vya CUF na CCM. Vile vile Mwenyezi Mungu awabariki Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili kauli zao ziwe ni thabiti katika kuiweka nchi yetu kwenye ramani nzuri. (*Kicheko/Makofi*)

Mhe. Spika, nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru sana na mimi kunipatia nafasi hii adhim niweze kutoa mchango wangu. Kwa hivyo, nitajitahidi sana kuchangia kwa ufupi na uhakika. *(Makofi)*

Kwanza kabisa Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye pia ni Makamo wa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi upande wa Zanzibar pamoja na Katibu Mkuu wa CUF kwa kukutana, kujadili na hatimaye leo hii tupo hapa kwa ajili ya kufuatilia mazungumzo yao. *(Makofi)*

Pili nampongeza tena Mhe. Rais kwa kutambuliwa rasmi na Chama cha CUF, kwamba yeye ni Rais halali wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza nitaeleza kwa ufupi mambo ambayo ni muhimu katika nchi yetu ya amani na utulivu, mshikamano wa Wazanzibari, kuleta maendeleo ya ustawi wa jamii na uchumi katika nchi yetu. Kwa hivyo, hayo nitakayoyazungumza nitatumia hotuba za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alizozitoa hivi karibuni, katika kutimiza miaka ya 46 ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964.

Kwanza mkutano wa Vikunguni Pemba ilikuwa ni Sherehe ya Elimu Bila ya Malipo Mhe. Spika na wengi tulihudhuria na nitawataja. Mimi mwenyewe binafsi mwenyewe wetu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano, Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha, Mhe. Haji Omar Kheir, Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, Mhe. Waziri Kiongozi, Wakuu wa Mikoa yote miwili ya Pemba na bila ya kumsahau Mhe. Naibu Waziri wa Tanzania Bara wa Masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kadhalika.

Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Rais alisema hivi biashara ya ugomvi haiuzwi na wala hainunuliki. Kwa mfano, unalo duka lako kwa ajili ya kuuza ugomvi, basi hupata wateja na wote watakukimbieni, hayo nasema mimi hata nyumbani ukiingia ugomvi, ukitoka ugomvi kama hujakimbiwa basi utakimbia wewe. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, haya Mhe. Rais alikusudia kwamba tukae pamoja kwa ajili ya kujenga nchi yetu na tuache ugomvi, kwa sababu ugomvi hauna maana. Mhe. Spika, naomba kutoa siri niwaambie ndugu zangu wa Pemba. Hivi juzi zahma kidogo zilizotokea Pemba na wala hamjui kilichotokea basi mimi nitakwambieni leo.

Mhe. Spika, nilikaa ndani ya afisi yangu peke yangu pamoja na wazungu ambao ni madaktari bingwa kutoka nje na wala sitaji nchi gani, jumla yao ni kumi, wanakuja kila mwaka na kwenda Pemba, kwa ajili ya kuwachunguza pamoja na kuwapa dawa na mwisho wanapoondoka huwaachia madawa kila mwaka. Kwa mfano, wanakwenda Hospitali ya Chake Chake pamoja na vituo vyengine mbali mbali.

Safari hii Mhe. Spika, ndani ya afisi yangu na wala hajui mtu yoyote isipokuwa mimi tu ndiye ninayejua siri hiyo, basi waliniambia hatwendi Pemba. Sasa niliwauliza hamwendi Pemba, mtakwenda wapi na kila siku mnakwenda Pemba, waliniambia tutafutie popote, basi niliwapeleka Kivunge, Mahonda, Makunduchi na kufanyakazi zao mbali mbali za kuchunguza wagonjwa pamoja na kuwatibu na baadaye kuachiwa madawa. Faida ya biashara ya ugomvi watu wanakukimbieni.

Kwa hivyo, *alhamdulillah* tunashukuru kwamba huku salama, kama ingekuwa huko ndio hivyo, basi na huko tungekimbiwa. Kwa maana hiyo, tukubali kwamba ugomvi katika nchi yetu tuondoshe na sisi kitu kimoja na tukae pamoja, tufanye kazi kwa pamoja na tushirikiane kwa pamoja. (*Makofi*)

Mhe. Spika, masuala haya haya Mhe. Haji Omar Kheir alinipia simu na kuniuliza Mhe. Waziri upo wapi, nilimwambia niko shamba, kwa sababu mimi ni mkulima. Nipo hospitali na mtu wangu ambaye amepiga, basi nilimwambia nakuja mwenyewe, nilitoka na gari mpaka hospitali wakati wa laasiri kama hivi sasa, yaani mwanamke amelala kwenye sakafu amechukua kanga na kujifunga kwenye kichwa na ameroa damu.

Kutokana na hali hiyo niliondoka mwenyewe na kwenda kuwachukua madaktari timu nzima ya machina na kuwaleta pale. Baada ya kufika daktari bingwa wa china kumfungua ile kanga, basi hiki kidole changu ndio shimo kwenye kichwa, basi mchina alisema *Theater*. Hafla yule mchina ameshabadilisha nguo pamoja na wenzake haraka haraka, basi alishonwa nyuzi nyingi kwa kweli na tatizo nini, halijulikani, kinachogombaniwa nini, hakijulikani.

Kwa kweli masikini ya Mungu hana mbele wala nyuma Mchina aliniambia Wallahi angetoka roho yule, jicho nalo sijui vipi. Lakini zaidi tumuulize Mhe. Haji Omar Kheir.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nizungumzie kuhusu mkutano wa Mhe. Rais alioufanya hivi karibuni tarehe 3 mwezi wa Januari Kitengo cha Malaria Mwanakwerekwe. Katika mkutano huo ulihudhuriwa na Katibu Mkuu wa

Chama cha CUF Maalim Seif Sharif Hamad, pia na Naibu Katibu Mkuu wa CUF Mhe. Juma Duni Haji pamoja na Dk. Muchi.

Kwa upande wetu huku Mhe. Waziri Kiongozi, mimi mwenywe, Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora. Kwa kweli siku hiyo ilivyesha mvua kubwa sana tarehe 3 Januari mwaka huu. Mhe. Rais alisema hivi na Mhe. Mwakilishi wa Chake Chake na watu walifurahi, yaani aliisifu Zanzibar na watu walifura, basi aliwaambia mmefurahi ee! Na Mhe. Naibu Waziri wangu alikuwepo nilimsahau. (*Makofi*)

Alisema mmefurahi nilipoitaja Zanzibar, basi Zanzibar inaweza kupotea kwa dakika, kutokana na hali ile basi pale pakawa kimya isipokuwa mvua tu inanyesha, pamoja na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi naye alikuwepo.

Mhe. Spika, uwanja uliokuwa na sherehe basi ulikuwa kimya na kubakia mvua tu baada ya kusema kuwa Zanzibar inaweza kupotea kwa dakika moja tu, sababu ni haya mambo yasiyokwisha ya kutokufahamiana baina yetu. Hivi sasa Zanzibar duniani inajulikana naweza kusema hivyo.

Mhe. Spika, alikuja Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (*WHO*) na tulimpeleka kwa Mhe. Rais na kuzungumza naye pale vizuri sana, labda nizungumze kidogo yale waliyozungumza. Kwa kweli mazungumzo yalikuwa mengi na baadaye alimwambia Mhe. Rais nataka nikuombe kitu na hapa sicho nilichokusudia kusema imeingia katikati.

Kwa hivyo, nataka kukuomba kitu Mhe. Rais, alimwambia niombe, kwamba nataka kuleta Mkutano wa Kimataifa ya Malaria Duniani ufanyike Zanzibar. Mhe. Rais alimwambia nimekukubalia na kumuuliza lini, basi Mkurugenzi Mkuu alimwambia mwezi wa Oktoba mwaka 2010 na Mhe. Rais alicheka. Baadaye alimwambia hutonikuta hapa Ikulu, Mkurugenzi Mkuu alishtuka sana na kuuliza kwa nini, alimwambia mimi ndio namaliza wakati wangu. (*Makofi*)

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Spika amini usiamini mazungumzo ndipo yapoanza upya, yaani yale ya nyuma yote yalimalizika na kuanza upya, Mhe. Spika hapa nazuia kwa sababu sijapata ridhaa ya Mhe. Rais. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tulipotoka Ikulu na Mkurugenzi Mkuu tulimpeleka kijiji kimoja kinachoitwa Jendele na kumuonesha Kituo cha Afya pale na kuhusu masuala ya malaria pamoja na mambo mengine. Kwa hivyo, *protocol* ya Dr. Magret Chan. Wazungu wa kike wawili wakanijia wakaniuliza hivi, Unguja mna hospitali kubwa *referral* ngapi? Nikawaambia moja, pale pale Jendele. Inaitwa

nini? Nikawaambia Mnazi Mmoja Hospital. Wakaniambia kuna *beds* ngapi? Nikawaambia *four hundred beds*. Sisi tunataka kwenda huko na Dr. Magret Chan, nikawaambia haimo katika *program*, wakaniambia ndio maana tukakwambia ati, nikaona hii kasheshe. Naibu wangu ananisikia.

Nikawaita watu wa mambo ya nchi za nje kina Leluu pale nikawaambia bwana nina ombi hawa Wazungu wanasema Dr. Magret Chan apelekwe *Mnazi Mmoja Hospital*. Hee, ikabidi tukae kikao pale mwisho wakakubaliwa ikaambiwa gari ya polisi ielekeze *Mnazi Mmoja Hospital*. Nimo ndani ya gari Mhe. Spika, amini usiamini namuuliza Dr. Magret Chan unataka kuangalia nini *main hospital* yetu? Akanambia nataka kuona Wodi ya Watoto nione kesi za *severe malaria* Zanzibar. Sawa sawa twende. Tulipofika pale tukapanda wodi ya watoto, wodi nzima hamna mgonjwa hata mmoja kwenye kitanda, anaulizwa Dr. Ali Amour *surprise visit* wako wapi wagonjwa? Anasema Unguja hakuna malaria, zamani ilikuwa vipi? Akaambiwa kitanda kimoja wagonjwa wawili mpaka watatu wengine kwenye sakafu.

Tukenda chini tukakuta huyu ana *sickle cell anemia*, huyu kaungua uji umoto huyu maji ya moto, ananibia Dr. Magret Chan siamini, *news letter* ya *WHO* ya *Visit Magret Chan Tanzania* dunia nzima imeonesha picha za Hospitali ya Mnazi Mmoja Wodi ya Watoto tupu. Mhe. Spika, nitakuletea nitakuletea utizame. Yamepatikana vipi mambo haya? Yamepatikana mshikamano wetu baina ya nyinyi na sisi serikali Wizara ya Afya. Leo naipigia Pemba dawa ya malaria sasa hivi wiki nzima naifukiza, si mnajua waheshimiwa au hamjui?

Waheshimiwa Wajumbe: Tunajua.

Mwezi ujao nitaifukiza Zanzibar yote, basi mshikamano wa Wazanzibari, umoja wetu ndio tumeweza kupiga vita homa ya malaria. *Caroliscar Institute* imejenga maabara Kivunge yenye gharama mamilioni ya fedha nafikiri Mhe. Spika, ndiye aliyekuwa Mgeni Rasmi kufungu maabara ile. Wakati ule malaria ilikuwa imezagaa, maabara haina wagonjwa ishafungwa haitumiki gharama tele na haitumiki. Tunafanya mazungumzo sasa tuwafanyie *research* watu wa *TB* mambo ya *diabetic* labda, imefungwa miaka nenda miaka rudi maabara haifanyi kazi. Zanzibar inatajika tukifanya masihara yetu Zanzibar itafutika.

Mhe. Spika, atakuja hivi karibuni Prof. Green House kutoka *University of San Francisco* California, keshaleta *research proposal* yake, anataka kutafuta hii malaria, malaria wanayoumwa watu inatoka wapi, inatoka Tanzania Bara, Pemba, Makunduchi, Kivunge anataka kufanya utafiti huo, ni utafiti wa aina yake. Sasa tuwe wamoja, tuijenge nchi yetu, tusingalie nyuma tulikotoka.

Nakuja kwenye mkutano wa Makombeni Pemba. Mhe. Spika, amini usiamini Baraza lako tukufu upande ule walinjia kwa vishindo wakiongozwa na Mhe. Mohamed Ali Salim ufunguzi wa barabara ya Makombeni, humjui CCM, humjui *CUF* watu tunakumbatiana na aliyetia fora ni Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba. Mwenyewe sijui yupo, basi alitia fora yeye, sijakwambia nilichokusudia nitakwambia baadaye. Alimwita Mhe. Waziri Kiongozi akamwambia wasalimu Wazanzibari basi tukasikia pale CCM oyee, akaitwa Naibu Waziri Kiongozi tukasikia CCM oyee, akaitwa Katibu Mkuu wa *CUF* alisema vipi vile. (*Kicheko*)

Mhe. Spika: Tusimcheke vitu vyengine kutamka ni vigumu kweli bwana. (*Kicheko*)

Mhe. Spika, nilichokusudia Mhe. Rais alisema hivi, haya ndio niliyokusudia, Mapinduzi ya mwaka 1964 yalikuwa ni kumuondosha Sultani basi, sio mimi. Mhe. Mkuu wa Mkoa akaeleza vizuri sana pale pale, Mhe. Spika, ingekuwa si Mapinduzi ya mwaka 1964 hivyo sisi sijui wengine tungekuwa tuko wapi, haya ni mapinduzi yaliyoleta hivi tukawa huku na kule. Tunagombaniana nini?

Nimemjua Mhe. Pandu Ameir Kificho mwaka 1971 Lumumba, nimemjua Mhe. Juma Duni Haji mwaka 1971 Lumumba pia, yeye alikuwa *Form VI* mimi niko *Form III* pamoja na Mhe. Spika pamoja na Rashid Jabu.

Mhe. Juma Duni niko tayari kwa *correct*, alikuwa ndiye mwenyekiti wa Afro Shirazi Party *Youth League*, mimi mdogo siku hizo Lumumba, yeye anapanda juu ya steji anaghuruma George Fernandis haonekani, kama hamuyajui. (*Kicheko*)

Sijui alikuwa yeye kwa sababu kuna siku moja Mwenyekiti wa Afro Shirazi Party *Youthleague* alipanda Lumumba juu ya steji akaghuruma, sijui alikuwa yeye au mwengine, wakati ule darasa letu asubuhi ukiamka Zakhululi kakimbia, Jumanne ukiamka Najma kakimbia ndio majina hayo nakutajieni nina hakika. Jumatano Zakiya kakimbia, Alhamis Thureya kakimbia, Ijumaa walimu Pateli kakimbia, alisema hivi, Mwenyekiti wa *Afro Shirazi Party Youth League* tumeumbwa kwa *oxygen* ya Unguja, *nitrogen* ya Unguja, *calcium* ya Unguja, uwe na moyo wa kutumikia nchi ya Zanzibar, nikasema yeye au nani. Unajua maana yake nini? Maana yake sisi sote hapa chakula unachokula ni chakula kinachotokana na ardhi ya Zanzibar kwa hivyo, mna *calcium*, *mineral* zote hivyo mmeumbwa ukue ukae utumikie nchi, pigwa pigwa siasa sawa sawa pale. Sijui Mheshimiwa ndio wewe yule au mwengine. (*Kicheko*)

Sasa lengo langu lote ni kwamba sisi sote ni ndugu. Mhe. Rashid Seif nimemjua mwaka 1974 ametoka *Fidel Castro* ameingia *Form V* mimi namaliza

huyo hapo. Nani aliyempeleka Mhe. Mohamed Ali Salim *University of Dar es Salaam* mimi na yeye kama si Mapinduzi ya mwaka 1964. Mapinduzi ndiyo yaliyomfanya Rashid Ahmed Joy mwaka 2005 anapita Mkunazini anapiga beni watu wanauliza nini Joy? Anasema nakwenda kuchukua fomu ya kupigania Urais wa Zanzibar. (*Kicheko*)

Haya Mhe. Spika, nataka kuyaleta taswira tufahamu kwamba sote sisi ni ndugu tufanye kazi kwa mapenzi, tusigombane, tulikotoka mbali, tuko pamoja sasa ee Joy yule nani angelimjua wakati wa Said Khalifa. (*Kicheko*)

Mhe. Spika, mtiririko wangu nakuja Mkutano wa Kibanda Maiti pale Uwanja wa Demokrasia. Mhe. Rais alieleza mengi katika mkutano wake na Katibu Mkuu mwisho alimalizia “waamuzi wa mambo hayo yote ni nyinyi wananchi”. Mhe. Spika, nasema kwamba na mimi naungana na Waheshimiwa Mawaziri kwamba tuyapeleke mambo yote haya wakaamue wenyewe wananchi. Tuachie serikali itulete mswada hapa, namuomba ndugu yangu Mhe. Abubakar Khamis akuombe wewe aingie kwenye kamati husika ili aujadili huo mswada. Kwa sababu Baraza la Mapinduzi tutauzungumza, aingie auzungumze huo mswada kwenye kamati uwekwe sawa uletwe hapa tuupitishie tuwape tume waitishe kura ya maoni.

Kwa sababu ukisema huku watatu na huku watatu italeta vurumai, tuachieni serikali, pesa serikali itaangalia kama uwezo inao itatoa wakati mzuri tutaleta hapa tutawapa wananchi na baadaye tutakwenda kwenye uchaguzi Rais ajae atatizama nini kilichoamuliwa na wananchi. Wananchi wamekubali tutaweka Rais mwenye kura nyingi, wa pili makamo wa kwanza, makamo wa pili tutapata afuatane na yule Rais awe mrithi wake na ndio mkuu wa shughuli za serikali huko, mawaziri imeshasemwa tukisema wingi wa kura pengine Rais wenyewe huyo mwengine hana jimbo huku atakuwa hana waziri, alimradi mambo hayo yote Mhe. Spika, mimi nasema kwamba tupeleke jambo hili kwa wananchi.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, kitabu chako cha kanuni na leo umesoma ukurasa wa 19 na Mhe. Alhaji Mwenyekiti, Mhe. Ali Mzee Ali anaposoma dua hii basi inakuingia. Inasema hivi, “Uibariki Zanzibar iwe nchi ya amani na wote wanaoishi humo wawe na upendo halisi na umoja, utuepushe na tamaa mbaya, chuki na ubinafsi na utulinde na maadui ambao wanaitizama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jicho la husda. Pia umjaalie Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi afya njema na maisha marefu. Umpe hekima na busara ili akisaidiana na viongozi wenzake aweze kuongoza kwa haki na amani kwa manufaa na ustawi wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla”. Sisi tunaitikia amin. Hii ndio dua ya kuiombea Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Dua ya kuliombea Baraza la Wawakilishi, natoka sehemu ya mwisho, “Utuongoze daima katika kujadili mambo yote yatakayoletwa mbele yetu ili tuweze kushinda matatizo yetu kwa manufaa na ustawi wa nchi hii na watu wake”. Tunaitikia amin. Kama dua hii haifai Mhe. Spika, tuiondoshe kwenye kanuni. Mhe. Spika, nimemaliza.

Mhe. Fatma Abdulhabib Ferej: Bismillahi Rahmani Rahim. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kuneemesha neema zote kubwa kubwa na ndogo ndogo kwa kutuwezesha leo hii kutuamsha tukiwa wenye afya na kuweza kuja hapa kuwa leo hii tukiwa na hoja muhimu na nzito kwa maslahi ya wananchi wetu na nchi yetu kwa jumla.

Lakini pili naomba nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii adhimu nikiwa mwanamke wa pili kuchangia hoja hii nzito ambayo imewasilishwa mbele yetu.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kwa kupitia chombo chako hiki kitukufu yaani Baraza la Wawakilishi, kuchukua nafasi hii ya kumpongeza kwa dhati kabisa na kwa moyo wangu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Rais Amani Abeid Karume kwa ujasiri wake na kuonesha kupevuka kisiasa kwa kukubali kwake kukutana na Katibu Mkuu wa CUF Ikulu tarehe 5 Novemba 2009.

Mhe. Spika, nilikuwa kwenye ziara ya kazi Spain na nilipata habari hiyo kwa kupitia *email*. Mwanzo nilishituka sana, lakini baadaye kwa sababu nawaamini sana viongozi wetu sikuwa na wasi wasi kwamba mbele yetu kutakuwa kweupe.

Mhe. Spika, kukutana kwao kulizaa mazungumzo ambayo yaliziaa kitu kinachoitwa maridhiano ambayo yanalenga katika kuijenga Zanzibar mpya ambayo wananchi wake watakuwa na mahusiano mema kisiasa, watakuwa na umoja, mshikamano, watakuwa na maelewano miongoni mwao na hali hiyo itasababisha amani na utulivu wa kudumu ndani ya nchi yetu ambayo ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa nchi yoyote ile. Mhe. Spika, maendeleo ya nchi ya kiuchumi na kijamii huwa vigumu kufikiwa pale ambapo hapana amani na utulivu wa kudumu.

Sote tunaielewa hali ilivyokuwa ya kisiasa toka kuanzishwa kwa Mfumo wa Vyama Vingi angalau kwa kile ambacho nakikumbuka mimi, lakini leo hii asubuhi na kwa kusoma kitabu pia tunajua hali ya kisiasa ilivyokuwa kabla ya Mapinduzi na baadaye sasa baada ya kuanzishwa mfumo wa vyama vingi. Kwa ufupi wakati wote huo jamii ya Kizanzibari imekuwa ikipitia chaguzi ambazo hazikuwa zinaonekana kuleta faraja kwa Wazanzibari.

Mhe. Spika, walionitangulia wamezungumzia sana suala la chaguzi zilizopita za kihistoria kabla ya Mapinduzi, nisingependa kwenda huko lakini napenda nizungumzie hapa karibu kuanzia Mfumo wa Vyama Vingi mwaka 1992 ambapo ndipo mimi mwenyewe uhalisia wake nimeuona. Katika hili naomba nichukue nafasi kidogo Mhe. Spika, niwakumbushe tu wajumbe juu ya matokeo ya kura ya Urais.

Kura ya kwanza kabisa ya Urais ya mfumo wa vyama vingi mwaka 1995, kura hii Mhe. Spika, izingatiwe kwamba ilikuwa ni baada ya Mfumo wa Chama Kimoja wa miaka 30. inaaminika kwamba Wazanzibari waligaiwa sana kabla ya Mapinduzi kuwa kuwepo na vyama vingi, vyama hivi vilipigwa marufuku. Lakini kwa sababu katika dunia hii Zanzibar kama Wazanzibari hatuishi kama kisiwa, inabidi twende na mambo yanavyokwenda duniani, tumelazimika kuingia katika Mfumo wa Vyama vingi na mwaka 1995 itakumbukwa kuwa hiyo ni miaka 30 baada ya kuwa na utawala wa chama kimoja, Zanzibar iliingia katika uchaguzi wa vyama vingi.

Matokeo Mhe. Spika, naomba ku-*quote* hapa, kama yalivyotangazwa na ZEC kwa wakati huo, CCM ilipata asilimia 50.2 ya kura za Urais na CUF ambacho ndio chama kilichofuata kilipata asilimia 49.8 ya kura za Urais. Ukija kwenye viti 50 vya majimbo ambavyo vilikuwepo basi CCM walipata viti 26 na CUF wakapata viti 24.

Mhe. Spika, hali hiyo inaonesha kujiendeleza hata baada ya miaka 15 ya Mfumo wa Vyama Vingi na hapa napenda mzingatie pia matokeo kama yalivyotangazwa ya kura ya Urais ya mwaka 2005. CCM walipata asilimia 53.2 na CUF 46.1. madhumuni yangu hapa Mhe. Spika, ni kuonesha jinsi gani jamii ya Kizanzibari imegawika katika kambi mbili kuu za kisiasa. Kwa kiasi fulani zinakaribiana kwa nguvu zake, kama mtu anapitwa basi anapitwa kidogo tu. Sasa hii hali ya kuwa kuna kambi mbili ambazo zote zina nguvu ndio inayoleta kutokuaminiana baina yetu.

Mhe. Spika, mimi nisingependa kurudi kwa yaliyotokezea, sote tunayaelewa sana sana ni kukumbusha madonda na mimi katika hayo ambayo yametokezea napenda niseme kwamba kambi hizi mbili zote zinahusika, CUF imehusika kwa upande wake na CCM imehusika. Kwa hivyo, hakuna lawama kwamba labda wewe ulikuwa na serikali ndio umehusika zaidi au mimi kama kambi ya upinzani ndiye nilihusika zaidi. Tukubali tu kwamba sisi sote wawili tulikuwa chanzo cha matatizo na migogoro ambayo inaendelea mpaka tu imeanza kubadilika kidogo kufikia maridhiano ambayo yamepatikana hivi karibuni mwezi wa Novemba.

Namshukuru sana kaka yangu, mwalimu mwenzangu ambaye amemaliza kuzungumza Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa jinsi alivyokuwa anaeleza matukio ambayo yametokea baada ya maridhiano haya.

Mhe. Spika, kulifuata sherehe za Mapinduzi ambazo kawaida hufuatiwa na ufunguzi au uzinduzi wa mambo mbali mbali. Wote ni mashahidi wa yale ambayo yalikuwa yanatokea. Hali ilikuwa ni ya mashirikiano na mshikamano wa hali ya juu, wananchi wote vijijini na mijini wamefurahi sana kwamba sasa kama Wazanzibari tuko kitu kimoja.

Sasa Mhe. Spika, njia pekee ambayo wanasiasa wengi na wasomi wengi wamekuwa wakitushauri sisi kama Wazanzibari ya kuondokana na migogoro ambayo imedumu kwa muda mrefu. Kwa mtizamo wangu mimi mwengine anaweza akakataa, kama Zanzibar tuko kwenye mgogoro kwa muda mrefu sana wa kisiasa, huu ni mwaka wa 15. Lakini ikiwa tutakubaliana na hoja ambayo Mhe. Abubakar ameiwasilisha mbele yetu kiini cha hoja yenyewe ambacho ni kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa Mhe. Spika, mimi naamini kwamba huu utakuwa ufumbuzi wa migogoro isiyokwisha ya kisiasa ndani ya nchi yetu. Mhe. Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe hili nakubaliana nalo moja kwa moja.

Tunaweza tukatofautiana kwa *format* gani Serikali ya Umoja wa Kitaifa ije na hilo ndilo jambo ambalo linazungumzika. Kwa hivyo, nashauri Baraza lako tulizungumzie hili lakini hatimaye tufikie maafikiano ya kukubali mfumo huu kwani ni njia pekee itakayomaliza migogoro ndani ya Kisiwa chetu.

Mhe. Spika, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Naomba kwa ruhusa yako uniruhusu nitoe mfano wa nchi moja ambayo wako labda wengine wamepata nafasi ya kuitembelea inaitwa Singapore. Singapore ina eneo dogo sana ni *square kilometer* 697, Zanzibar ni kubwa mara mbili kuliko Singapore.

Mhe. Spika, nchi hii ilipata uhuru kutoka kwa Muingereza mwaka 1963, Zanzibar tumejikomboa kutokana na Mapinduzi mwaka 1964 kwa hiyo wao wametangulia mwaka mmoja tu kuliko sisi. Singapore inawaje ni ndogo ina watu wengi kuliko sisi, ina watu 4,900,000, lakini Zanzibar tuko kama 1.2 (milioni 1.2). Kwa hivyo, sisi tuna *advantage*, tuna *land* kubwa na tuna watu kidogo.

Lakini tafauti yetu na Singapore, Singapore kunazungumzwa lugha nne tafauti na makundi makubwa makubwa ya wananchi wa nchi hiyo. Lugha kubwa ni Kiingereza, Malei, Tamil, Chainize na Mandarine. Halafu wao pia wamo kwenye mfumo wa vyama vingi kama sisi tulivyo na chama chao ambacho kimetawala toka mwaka 1963 ilivyopata uhuru ndio chama tawala hicho

ambacho kinaitwa *Pupils Action Part* ndio kinachoongoza. Lakini kuna vyama vyengine kama *Workers Part of Singapore, Singapore Democratic Part na Singapore Democratic Alliance*. Hivi ni vyama vikubwa vine ambavyo vimo ndani ya Bunge Mhe. Spika.

Lakini tofauti yetu sisi na Singapore ni kwamba wao wana makundi yaliyogawiwa kidini, yaani wao wanaamini katika dini tofauti nyingi, lakini kubwa lao ni *Buddhism*. Buddhism ni asilimia 42.5 Mhe. Spika, Waislamu ni asilimia 14.9, Wapagan ni asilimia 14.8, Wakiristo ni asilimia 14.6, Towism ni asilimia 8.5 na Wahindu ni asilimia 4.

Mhe. Spika, natoa mfano huu tutafakari jinsi gani taifa la Singapore lilivyogawika gawika, lakini kwa sababu ya busara ya kuweka serikali ya umoja wa kitaifa taifa hili pamoja na mambo mengine, lakini kule kuweka umoja wa kitaifa kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa imewafikisha katika hali nzuri sana ya kimataifa ya kupigiwa mfano.

Mhe. Spika, nchi hii ni moja kati ya nchi tano tajiri, ina *official reserve* ya US\$ 170.3 bilioni. Kwa hivyo, ni nchi ambayo hata sisi hapa tumekuwa tuki-*asses* mifano baadhi ya wajumbe wako Mhe. Spika, watakuwa nao wamepata nafasi ya kwenda kuona. Siri ya mafanikio yao ni umoja, mambo haya yote si dini, wala kabila, wala lugha ambayo wanazungumza haijawafanya wao wala vyama vyao vingi havijawagawa wako kitu kimoja.

Sasa Mhe. Spika, nitam-*quote* mara kwa mara kwa sababu amenivutia sana kwa *speech* yake mwalimu mwenzangu Mhe. Waziri wa Afya, anasema sisi sote ni ndugu. Mhe. Spika, karibu asilimia 97 ya Wazanzibari ni Waislamu, lugha yetu kubwa ukiacha wengine wanaozungumza Kimakunduchi na lahaja nyengine za Kipemba na nyenginezo kama Kingazija, lakini lugha yetu kubwa ambayo inatuunganisha sote ni Kiswahili. Lugha yetu ni moja, dini wengi wetu ni moja na wale ambao wamekuwa na dini nyengine hatujawahi kuwa na migogoro ya kidini ambayo imetugawa.

Mhe. Spika, inashangaza sasa ni vipi sisi kama Wazanzibari tunashindwa kufanya kazi pamoja kwa ajili ya manufaa ya taifa letu. Tumekubali makosa ambayo yamo ndani ya siasa ya kutugawa katika kambi mbili kuu na tumekuwa tunavutana. Mhe. Spika, mambo haya lazima tuyafikishe mwisho, na wa kuyafikisha mwisho haya ni sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu na sasa njia imetokea kwa kupitia hoja hii ya Mhe. Abubakar.

Mimi ushauri wangu tutafakari, tutizame *format* kama tunataka kuleta mabadiliko katika *format* kama ambavyo wawakilishi wengine wameanza

kuzungumzia asubuhi, mimi sina matatizo tunafikia pahala tuone kwamba sasa tunakuja na mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaiifa.

Mhe. Spika, hicho au hilo ndilo tarajio la Wazanzibari. Mimi sina wasi wasi Mhe. Spika, tukipeleka kura ya maoni kesho kwa wananchi itakuja *yes*, sina wasi wasi kabisa, wananchi wamechoka kugawiwa na wameona ni kiasi gani migawanyo imetufikisha, *one third* ya wananchi wa nchi hii hawapati mlo wa zaidi ya mlo mmoja, huu ni umasikini wa mwisho, ni masikini sana sisi. Hatuwezi kuendekeza siasa tukaacha maisha ya wananchi wetu, lazima kwanza tuwajali wananchi wetu na kuwajali wananchi wetu ni kuacha matamanio zaidi ya vyama tukaweka utaiifa mbele. Ndio matamanio binafsi na ya vyama tuyaweke upande, matamanio binafsi yanaweza kukupeleka pabaya. Kwa hivyo, uyaweke upande.

Vyama tunavyo tunavipenda sana mwenzangu alisema weka upande tutizame kwanza ni Wazanzibari, wananchi wetu, wengine masikini hata vyama hawana hawajui kumi lipi wala kumi na moja lipi, tunawaburuza, tunawapeleka mambo mabaya sana si ya kukumbusha. Lakini mimi nasema tufike pahali kama wawakilishi halali sisi wa wananchi tuamue kwamba sasa migawanyo hii haitatufikisha pahala. Mifano ipo mingi.

Mhe. Spika, Rwanda waliuana wakauana, ukiangalia zile filamu zake unaweza ukachanganyikiwa. Lakini hivi sasa wamefika pahala wamekaa juu ya meza wametengeneza serikali ya pamoja wako wametulia na nchi ambayo inakwenda *very fast* katika maendeleo. Mhe. Spika, hakuna lisilowezekana, kwa hiyo mimi niwatake wajumbe wenzangu walitafakari hili.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe naliunga mkono hili moja kwa moja. La pili ambalo naliunga mkono ni suala la kwenda kwenye kura ya maoni. Mimi sina pingamizi nalo ni kupanua demokrasia kwa sababu sisi wengine ingawaje hatujui mazingira ya wakati ule yalikuwa vipi, tunasema kwa nini wazee wetu hawakuhusishwa kwenye masuala ya Muungano walikaa watu wawili wakaongea.

Kwa hiyo, kuondosha dhana kama hizo ni vizuri twende zetu kwa wananchi tuwaulize wanataka kitu gani. Ni imani yangu mimi tu kwamba hili halitakuwa na tatizo kwa sababu uhalisia wa wananchi unaonesha kwamba wanataka kuwa kitu kimoja. Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii anasema pale kwamba sisi ni ndugu watu milioni laki mbili, *who is fighting who for the benefit of who?* Yaani ukinipiga mimi pengine mtoto wa mjomba wako, ukimgusa yule mkweo, ndio mambo yenyewe kama hayo.

Hakuna mtu mbali, Zanzibar ni ndogo sana na tumegusana sana na kila mtu anajua hilo, aliyeko CUF ni ndugu baba mmoja mama mmoja na aliyeko CCM, sasa *who is killing who?* Tufike pahala tuone kwamba sisi ni kitu kimoja tukubaliane na hizi hoja ili kuona kwamba tunafikia pahala.

Mhe. Spika, naomba na mimi ninukuu. Nilipata bahati Mhe. Spika, ya kuchaguliwa na wewe kwenda Pemba kwenye Sherehe za Mapinduzi. Nilifurahi sana kwa sababu kwa miaka mingi sijui kama toka nilipokuwa mwanafunzi au nilikuwa nafanya kazi Wizara ya Elimu, sikupata tena fursa ya kwenda kwenye sherehe ile kwa sababu tu zile zile za migawanyo kuona kwamba ile ya wenye serikali, hii si ya wapinzani, ni mambo kama hayo. Lakini niseme kwamba mimi nilifarajika.

Kwa kweli nilifarajika kutokana na hali niliyoiona katika kiwanja cha Gombani Pemba. Wananchi kwa umoja wao bila ya kujali itikadi zao za chama walifika, walishangilia Uzanibari wao, walishangilia Mapinduzi yao, hakukuwa na tatizo lolote. Kubwa ni kwamba nafasi ya kiwanja tu ilikuwa ndogo mbanano ukatokea na ajali ikatokea.

Lakini yale ni mambo ambayo tunayataka, hatutaki kuona kwamba kuna sherehe ya kitaifa mtu hajisikii kwamba na yeye ni mtaifa. Ninahakika siku ile kila Mzanzibari alijisikia kwamba Mapinduzi haya ni yetu, ni yangu, napaswa kwenda kusherehekea. Hiki ndicho kinachoelezwa humu moja kama msingi na haya ndio ambayo tunataka yaendele. Ile ni *fact* na haiwezi kuondoka, kila anayeishi Zanzibar ile ni *fact* na inabakia kuwa ni *fact* na mmoja wa msingi kama ilivyo kwenye hoja.

Mhe. Spika, mimi sina mengi, mengi yameshasemwa si mjuzi sana wa kuchagua *format* za Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Lakini ningependa nimalizie kwa kumnukuu Mhe. Rais na nizungumzie maneno yake ya mwisho katika *paragraph* ya tatu ukurasa wa 33 wa hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Amani Abeid Karume katika kuadhimisha Sherehe za Miaka 46 ya Mapinduzi ya Zanzibar, tarehe 12 Januari, 2010 pale Gombani ambapo mimi nilikuwepo nikiisikia *live*. Mhe. Spika, mimi nilikubaliana na hii *statement* na nataka wenzangu muichukue mtafakari.

Mhe. Spika, Mhe. Rais alisema “Tukubali kutofautiana katika fikra, lakini pia tukubali kuwa mambo yanayotuunganisha ni muhimu zaidi kuliko tofauti zetu za fikra”. Fikra maana yake ndio sera hizo, ili nifike pale mimi nitapita huku na ili nifike kule mimi nitakatia huku, hizo ndio fikra na sikubaliani na wale wanaosema turudi nyuma kwenye mfumo wa chama kimoja, kule ni kuzibana

fikra. Sasa hivi unatakiwa uzitanue fikra kila mtu afikiri na pengine ile unayoiona wewe kwamba ni fikra mbaya kumbe ndio itakayotufikisha *you never know*.

Mhe. Spika, kinachotuunganisha sisi ni Uanzibari wetu. Mhe. Spika, popote unapokwenda katika dunia hii Wanzibari wanajifaraha Uanzibari wao *actual* wanasahau kwamba Taifa la Zanzibar nje halijulikani, mtu anajieleza akiulizwa amekwenda kusoma vyuoni huko anasema mimi ni Mzanzibari watu wanaanza kupata tabu, mpaka aje Mtanzania ndio anasema ah, kumbe ni Mzanzibari/Mtanzania. Wanajitambulisha kwa Uanzibari wao na wanakuwa kitu kimoja popote wanapokuwa. Iweje leo sisi ndani ya nchi yenyewe ambayo watu wanajifaharia wakiwa nje tuwe tunagawana, tunagombana.

Mhe. Spika, nimezungumza vya kutosha na ombi langu kubwa kwa wajumbe tuichangie, tufafanue kwa wale ambao mahodari wa kueleza mifumo tofauti ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, lakini hatimaye tukubaliane basi ili tuwaondoshe wananchi wetu katika matatizo na tuweze kupiga hatua katika maendeleo ambacho hicho ndio wananchi wanachokitaka. Mhe. Spika, nakushukuru, ahsante.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa na afya njema, sina wasi wasi, niko tayari kuelezea matakwa na utumishi wa wananchi wangu wa Jimbo langu la Kwahani kwa faida ya maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Spika, kwanza nataka na mimi nitoe historia japo fupi, ingawa wakati wa Mapinduzi nilikuwa mdogo lakini kwa wakati huo na udogo wangu kwa kwetu Kiwengwa nilikokuwepo nilikuwa nakujua baharini wapi kutwika ngarawa na kurudi nchi kavu, sina wasi wasi.

Mhe. Spika, historia inaweza kutusuta kama sisi hatukuiielewa vizuri na kama hatukuifuata. Tatizo kubwa katika nchi yetu Mhe. Spika, tumeikosea sana serikali au wananchi wetu kuwaondolea somo la historia katika nchi.

Mhe. Spika, mara baada ya Mapinduzi ya 1964 Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alihojiwa tulivyoielezwa sisi. Je, nchi umeshaipindua au umeshakuwa na Serikali yako ya Mapinduzi ya Zanzibar, unategemea kufanya uchaguzi lini? Marehemu Mzee Karume akasema uchaguzi wa Zanzibar utafanyika baada ya miaka 50. Mhe. Spika, naamini mzee wetu aliona mbali sana, kuona mbali sana ndio hayo yaliyotukuta leo. Tulikuwa chama kimoja sasa tuko vyama vingi, lakini tunataka tuwe chama kimoja kwa mfumo ambao utataka kuletwa sijui kwa njia gani.

Sasa niseme tu na mimi uamuzi kama alivyosema Mhe. Haji Mkema Haji. Naomba kama sisi viongozi wa vyama viwili tumo humu katika Baraza hili na tuna kauli njema, bora tukakirudisha chama kimoja hapa Zanzibar tukawa na chama chetu hichi hichi cha CCM kinachotawala. Wajumbe hawa huku warudi huku wajiunge, ili na wao tuondoe huu udhia wa kutaka kupewa madaraka kwa njia ya pembeni.

Mhe. Spika, nakubaliana na maelezo yote yaliyoelezwa hapa, lakini kwa kuwa mimi nimetokana na wananchi wangu wa Jimbo langu la CCM Kwahani, nasema kwa asilimia mia moja namuunga mkono Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora kwa muongozo wake mzuri na maelekezo mazuri na kwa asilimia kubwa ilikuwa tumemaliza kazi.

Lakini kama wajibu wananchi wetu wana haki ya kutusikia na ni lazima tuwaelezee na waelewe umuhimu wa amani na utulivu katika nchi yetu. Mhe. Spika, niseme kwamba mimi katika hili ukurasa wa kwanza suala la makubaliano baina ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Amani Abeid Karume na Katibu Mkuu wa CUF, Maalim Seif Sharif Hamad kwa kusema kwamba wametafuta amani na utulivu na yeye kumtambua Rais na kuondoa yote yaliyopita. Hayo sina pingamizi nayo nayakubali na mimi kwa asilimia mia moja na watu wangu.

Mhe. Spika, binadamu anaweza kufanya kosa akawa hajui kalianzia wapi, binadamu anaweza kujua kafanya kosa akajua kufuta makosa yake. Naamimi Maalim Seif Shariff Hamad toka mwaka 1995 nimo katika Baraza hili tumeshuhudia mengi sana. Umekuja muafaka wa kwanza, ukaja muafaka wa pili, yakaja haya ya sasa hivi Maalim Seif kenda kwa Mhe. Rais kusema yaliyopita kabla mazungumzo hayajakubalika mimi nimekubali. Nakubaliana sana ni ujasiri mzuri.

Lakini tuseme mimi kwa imani yangu, mawazo yangu na hofu yangu, je, karudi kweli? Kwa sababu hii si mara ya kwanza, wala ya pili, wala ya tatu. Mazungumzo ya muafaka wajumbe wapo hapa hapa mmoja Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwa upande ule kule aliyeleta hoja hii, angalau angetueleza katika mazungumzo yale pamoja na kukubali kuleta hoja hii kuna moja, mbili, tatu hatukulitimizwa lakini tumekubali kuliingiza hivyo hivyo, tungepata faraja kubwa sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, tume ile mara baada ya maamuzi ya Butiama wajumbe wakaambiwa warudi tena katika vikao vya pamoja CUF na CCM, lakini viongozi wa CUF walisema kwamba sisi haturudi *abadan* hatutaki, hatutaki. Hii Mhe. Spika, lazima niseme tuna indhari huko mbele tunakokwenda. Kwa

sababu isijekuwa mchezo huu tunapoteza nguvu zetu za maneno hapa, tunapoteza utu wetu kwa wananchi wetu, kuna majungu mengi yanayotokea huko nje tumehongwa pesa wengine sijui nini.

Mhe. Spika, hilo limenikera sana, kwa hivyo yote nasema kwa kuja hili. Lakini mimi nasema tu kwamba namshukuru Mwenyezi Mungu mimi moyo wangu safi, sijala rushwa, wala sina nia ya kula rushwa, hapa palipobakia mimi nataka kuelekea Makka nifute makosa yangu yote. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mwakani Mwenyezi Mungu akitujaalia mara baada ya uchaguzi au kabla katika Wajumbe wa Baraza hili ambao watabahatika kwenda Makka mmoja ni mimi Mwenyezi Mungu akinifikisha na Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu huenda tukafuatana pamoja. Nawadhihirishia watu kwamba nimeikubali hii amani na utulivu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hili sisemi kwa utani, tunapolizungumza suala kama hili dunia inatusikiliza, wananchi wetu wote roho hawana, wengine wanaona suala la shari, mimi naona la kheri kwa sababu kuzozana hakuna faida, kuzozana hakuna neema, kuzozana kuna maovu na kuna kama hasara kwa upande wetu.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa kuwa hoja hii imekuja wakati mzuri japo imechelewa sana kwa sababu kama ilikuwa tumekaa katika meza za pamoja sasa hivi pengine kura ya maoni imeshafanya kazi tunangoja uchaguzi. Lakini bahati mbaya unajua kila jambo lina wakati wake. Niseme Mwenyezi Mungu alivyotujaalia huko kote tulitembea na Maalim Seif Shariff Hamad aliona baada ya makosa makubwa aliyoyafanya ya kibinadamu, ndio inavyotokea kiongozi lazima afanye makosa lakini akielekezwa atafahamu karudi kwa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, kwa mawazo yangu, lakini nauliza tena na namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha amuulize Maalim Seif Shariff Hamad karudi kweli kwa moyo safi? Mimi nina hofu, naamini kwa kauli yake siku nyengine kala kiapo pale uwanjani Kibandamaiti katika jimbo langu, “Nasema nimerudi nipigeni mawe, nimekubali na nime mtambua Rais”. Mimi nashukuru kumtambua Rais si jambo dogo hilo na ni jambo la kijasiri kweli.

Mhe. Spika, nirudie tena namuomba sana mtoa hoja hii akija atatuelekeza vizuri, lakini najua moyo wake safi ambao ameonesha huenda ukaleta faraja ya maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, suala la hoja za wajumbe mbali mbali kusema kwamba wananchi ndio watakoamua maamuzi yote yatakayotolewa hapa kwa maslahi ya nchi hii, yaani watakuwa waamuzi wenyewe. Mimi nasema wananchi wangu wa

Jimbo la Kwahani wao ndio wataamua, naomba waamue wao wenyewe. Mwakilishi wamenileta hapa kuwasemea lakini waamuzi wawe wenyewe kwa sababu waliotuweka hapa kwa ridhaa hiyo ndio wao na wao watatwambia tena tunataka serikali iwe namna hii.

Mhe. Spika, haya hayana utata, nchi nyingi za Ulaya zinajiunga katika Jumuiya ya Ulaya na mara nyingi Bunge huamua au wakakaa katika Baraza la Mawaziri na Mbunge anasema tu kwamba pamoja na sisi uwezo tuliokuwanao lakini hatuna sauti bila ya wananchi. Kwa hivyo, ili nchi yetu kujiunga na Jumuiya ya Ulaya basi lazima pawe na kura ya maoni, wananchi wakisema ndio basi ndio, wakisema hapana iwe hapana.

Mhe. Spika, hili linakubalika wala halina matatizo.

Mhe. Spika, jengine hivi sasa katika wachangiaji wako wote hapa kila moja ana sura ya bashasha sana. Lakini nasema baada ya matokeo ya kura ya maoni, kura ya maoni imesema ndio iwe ndio, kura ya maoni imesema hapana iwe hapana, tusije kurudi hapa tukakunjiana uso. Matokeo yatakayoamuliwa na wenzetu huko tuyaamini kwa sababu wao ndio wanaotupa ridhaa ya kuja hapa na ndio waliotupa ridhaa ya kusema tunayotaka kwa maslahi yao.

Tumekubaliana mtoa hoja kasema “Maamuzi yote yatakayoamuliwa na wananchi ndio yaheshimiwe” na mimi nakubaliana na hayo hayo. Maamuzi ya wananchi tunataka serikali ya umoja, sijui mseto, wakisema ndio tuseme ndio, wakisema hapana tukubali hapana. Kwa hivyo, Mhe. Spika, baada ya matokeo ya uchaguzi Mhe. Rais atakuwa na maamuzi yake mwenyewe kutokana na busara zake.

Kama kiapo chetu katika kanuni zetu Mhe. Sultan Moh’d Mugheiry alikisoma vizuri kwamba Rais anaongoza kwa hekima na busara, basi hata washauri atawapata wazuri ambao watamuongoza wakati huo Rais atakayekuja. Kwa njia moja au nyengine atatazama tu kweli Baraza hili kwa kuwa wananchi wamekataa, lakini kutokana na kuwa katiba haikunizuia namleta fulani. Kwa mfano, Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji njoo huku kidogo, Mhe. Hija Hassan Hija njoo huku, yote kutaka umoja.

Mhe. Spika, mimi nasema toka enzi serikali ya umoja ipo mpaka kufika hivi sasa. Kwa sababu hatuchunguani fulani ana chama gani, fulani ana nini, hayo mengineyo tu ya dhana. Kwa sababu hii nasema Mhe. Spika, katika serikali yetu tumechanganyika, tuna mashemeji zetu, tuna ndugu zetu, ndio tunavyokwenda. Sasa mimi nikitaka tena nichungue mengine mengi zaidi hayana maana.

Mhe. Spika, mimi ombi langu kura ya maoni kwa wananchi wetu matokeo yake tunayathamini na tuyaheshimu. Wakati sisi tumekula kiapo kwa msahafu hapa itakuja kutupa halbadiri kama hii aliyosema Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kaeni mpaka miaka hamsini msahau nyoyo zenu ziwe safi. Alichukulia hayo ili tusahau wale waliopindua, waliopinduliwa, wasahau yaliyopita ili wajenge Zanzibar mpya.

Lakini Mhe. Spika, harakati za dunia kama nilivyosema, pia dada yangu Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kasema kwamba wakati umefika tuingie katika vyama vingi na sisi tunafuata mkondo ule ule hatuna njia. Kwa sababu wenye kustahiki kutupa misaada yao wakisema fanyeni hili kwa manufaa yenu na manufaa yao wao. Manufaa yao wao yanakuja hapa Mhe. Spika, kama hivi tumekaa tukigombana sisi basi wao kuna fungu fulani kule wanaweza kulitafuta ili waje wasuluhishe. Lakini pale haji bure na yeye itakuwa fungu lile lile anapata lake ili kuongezea katika mahitaji yao kwa kutafuta pengine.

Mhe. Spika, niseme kwa ufupi kwamba hili ni suala zito. Mhe. Spika, hata ukiona katika Baraza lako hili mtu mzima analia ujue pana jambo, tena jambo hilo si dogo. Mhe. Spika, Mhe. Abass Juma Muhunzi alikuwa na haki ya kulia, alifikiri machofu mengi yaliyompata katika moyo wake. Alisimama pale pale alipo akasema “Mimi naomba wajumbe wenzangu hebu tumkubalini Rais wetu, tumuamini kama Rais kachaguliwa, tumuamini ndio yeye huyu kwa sasa hivi hatokei mwengine”. Lakini Mhe. Spika, kwa asilimia kubwa alisusiwa. Tunasema ndio yameshapita lakini tunataka yasirudi tena maana yake.

Mhe. Spika, Mhe. Abass Juma Muhunzi alisusiwa, katika meza ile pale alipokaa rafiki yangu Mhe. Hija Hassan Hija alikuwa hakai yuko peke yake tulikuwa tunamuonea huruma. Lakini alisema kweli na kweli inauma sana. Mhe. Spika, mimi binadamu kama utanjia una shida mtu wangu hata wa kawaida tu, mheshimiwa nataka moja, mbili, tatu ningekwambia bahati mbaya, lakini nakwambia katika nafsi yangu sina utakasirika. Nikikudanganya njoo nitakupa baadae sikukupa ndio utakasirika zaidi maana nimeshakwambia kweli.

Mhe. Spika, Mhe. Abass Juma Muhunzi katika kumbukumbu za Baraza lako ilikuwa atungiwe kitabu maalum cha historia ya kumbukumbu yake yeye na Baraza lijalo. Kumbe wenyewe tunaweza kukaa na kusuluhishana kuliko kutafuta wageni kutoka nje kuja kuchukua pesa zetu.

Mhe. Spika, kitendo alichokifanya Mhe. Abass Juma Muhunzi ndio kilichomliza leo. Ningewaomba wajumbe wenzangu wote watakaosimama, maana na mimi naweza kulia kwa uchungu lakini nimejikaza kidogo sili. Hakulilia kitu chengine, kalilia ile hoja masikini aliyoitoa pale akaonekana

mbaya lakini ilikuwa lazima aseme tunaelekea wapi. Lakini yale yale yanarudi sasa Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kasema vizuri, rafiki yangu Mhe. Omar Ali Shehe kasema vizuri na wengineo. Haya ndio tunayoyatafuta, katika dunia ya leo hakuna anayetaka ugomvi. Katika nyumba hata majirani mkiwa mnagombana hakuna maendeleo. Kwa hivyo, mimi nasema maendeleo yoyote yanakuja kwa umoja, kufahamiana, lakini na mafahamiano tuyakubali kwa dhati kabisa bila ya kuwa na utatanishi.

Mhe. Spika, narudia kauli yangu ya mwisho ile niliyoitanguliza kwamba naomba katika hoja hii baada ya haya mawili niliyosema mimi, la kwanza kukubali hoja inayosema kwamba “Kuheshimu na kuyaendeleza yale mazuri aliyozungumza Mhe. Amani Abeid Karume na Maalim Seif Shariff Hamad, Katibu Mkuu wa CUF ili tuyaendeleze”. Haya hayana pingamizi.

Lakini hili la mwisho naomba tena ridhaa ya wananchi waliotuchagua na wasiotuchagua tuwarudishie wao wakayaamue kuyaleta hapa kwa faida ya mustakbali mwema wa nchi yetu.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa ikiwa yamekubaliwa narudia tena pazito sana hapa, namuomba mtoa hoja aje apaeleze vizuri. Je, ikiwa wananchi asilimia 80 wamekataa na asilimia 20 wamekubali, tuwape asilimia 20 kama marekebisho ya vyama vingi?

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwahani nashukuru kwa kutoa taarifa hii ambayo ni nzuri na namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie twende katika mwelekeo wa mustakbali mwema, ahsante.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi jioni hii kuweza kutoa maoni yangu. Mhe. Spika, kwanza nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima na sauti ya kuweza kuzungumza.

Mhe. Spika, hoja aliyoitoa Mhe. Abubakar Khamis Bakary mimi naiunga mkono, lakini nina sababu zangu za kuiunga mkono na hazitokani kwa asilimia mia na chama alichotoka na nilichotoka mimi.

Mhe. Spika, sisi tuna choyo cha maendeleo, tukiona wenzetu wanavyokwenda na jinsi gani sisi tunavyokwenda, kwa kweli tuna choyo kikubwa cha maendeleo. Sasa wataalam wengi katika mazungumzo ya waandishi wa habari meza ya duara, makongamano, semina wanatueleza kwamba Wazanzibari ni juu yenu kukubaliana. Kwa sababu hii mivutano na migongano

inamaliziamifarakano na kudumisha uzorotes haji katika nchi. Sasa sisi tukiendeleza ndio pale mwenzangu mmoja aliposema kuendeleza mivutano hii ni kwa faida ya nani.

Kwa mfano Mhe. Spika, tuna changamoto kubwa sasa hivi ya kuingia katika utafutaji na uchimbaji wa mafuta. Ule umoja wetu na kukubali kwetu kuitetea Zanzibar ulitufikisha pahala pazuri kwamba ile rasilimali sasa tuna tamaa nayo kwamba imo ndani ya mikono yetu. Lakini kwa busara za baadhi ya viongozi waliona kwamba watupatie mwamko wa kitaalamu katika uendeshaji wa shughuli hizo tukiwa kama ni viongozi.

Wamekuja ndugu zetu na marafiki zetu wa Norway wakatupatia mafunzo mazuri sana hapa na moja kati ya walilolitaja ni kwamba shughuli hii ya uchimbaji mafuta ni shughuli inayofanywa na makampuni. Hakuna nchi yenye rasilimali itakayoweza kutoa *risk* katika utafutaji na uchimbaji mafuta. Makampuni haya huwezi kuyaita na biashara hii haiwezi kufanyika ikiwa hapana utulivu katika nchi.

Sasa wakati wenzetu wanafika kutwambia hivyo sisi bado tunang'ang'ania ugomvi na migongano. Hii rasilimali itapatikana lini katika dimbwi la umasikini tulionao sasa hivi, tukiendeleza mivutano na migongano kwa ajili ya tofauti ya sera za vyama.

Mhe. Spika, wataalam wa kisiasa wanasema kwamba kujiunga na chama ni imani, si rahisi kumuondoa mtu kutoka imani moja kwenda imani nyengine. Sasa kwa sababu si rahisi kumtoa mtu kutoka imani moja kwenda imani nyengine na hii imedhihirika hata hapa Zanzibar tunapopazungumza. Njia ya muafaka ni kuchanganya zile imani wakafanya kazi pamoja na sisi ndio tuliokuwa na wajibu wa kufanya kazi hiyo. Tukubali mawili, tukubali kufarikiana tuanze kupoteza. Tutapoteza hadhi yetu, tutapoteza rasiliamli zetu, tutapoteza mpaka hii nchi yetu. Au tukubali tuingie katika mfumo wa makubaliano ili tuweze kuzihifadhi zote hizo na nyenginezo.

Mhe. Spika, Somalia si miaka mingi ilikuwa ikiitwa nchi ya Somalia yenye serikali. Lakini baada ya mifarakano iliyokuwa haimaliziki, sasa huwezi kusema kwamba Somalia kuna serikali. Mara utasikia serikali yenyewe inakaa Ethiopia, serikali yenyewe iko Nairobi, serikali iko Uganda haijulikani.

Mhe. Spika, yote haya ni mambo ambayo ni ya kuzingatia katika uso wa dunia tunaokwenda, sisi hatuwezi kwenda hivi kwa miaka na miaka au karne na karne. *As such* huyo Rais wa Zanzibar anapata kitu gani ambacho ni kikubwa kuliko kuweka watu pamoja katika kufarakana au kuwafarakanisha.

Mhe. Spika, kwa mfano, kuna watu hawataki, lakini kwa sababu ya ubinafsi anapewa Urais wa Zanzibar, hii Zanzibar ilivyo sasa hivi, huu Urais ni wa wapi. Mimi naomba niwaulize wajumbe huu Urais wa Zanzibar ulivyo sasa hivi, mwisho wake ni wapi. Mwisho wake ni Chumbe tu. Ni sisi Wazanzibari tukiungana ndio tutamfanya Rais wetu aweze kuwa na uso wa dunia. Lakini kama hatukukubaliana basi hali itakuwa sio nzuri.

Mhe. Spika, tunayo mifano mingi ambayo migogoro kama hii ambayo haiwezi ikatatuka basi inarudishwa kwa wananchi. Mimi binafsi sina tatizo na suala la kurudishwa kwa wananchi, yaani kupata kura ya maoni. Lakini ninalolizungumza ni hili. Mhe. Spika, mimi *profession* yangu ni ualimu na kuna falsafa moja ya elimu inasema, “bora usisomeshe kuliko kusomesha sivyoy”.

Mhe. Spika, wazungu wanasema “*better no teaching than wrong teaching*”. Nina wasi wasi mimi kwa baadhi ya maneno niliyosikia. Naomba Mwenyezi Mungu isitokezee, lakini nina wasi wasi kwamba huwenda wananchi wetu wakaenda kupewa elimu isiyostahiki katika suala zima la kuingia kwenye kura ya maoni.

Kwa hivyo, mimi napendekeza kwamba suala hili liwe na utaratibu maalum wa kutoa elimu hii na visiachiwe vyama, kwa sababu mivutano ya vyama ndio iliyotufikisha hapa, tukiachia vyama, Baraza likikubali kwamba elimu hii itolewe na vyama, basi kila mmoja atachukua msimamo wake. Ndio tutarudia yale yale, wazungu wanasema “*back to square one to*” tutarudia pale pale, tunakwenda wapi.

Kwa hivyo, ni muhimu sana kwenda kwenye kura ya maoni, lakini ni muhimu sana kutoa elimu inayofaa, ipangwe vizuri elimu na itolewe mifano, kuwe na mtaala maalum wa elimu hiyo na vinaweza vikatayarishwa vipeperushi, inaweza ikatayarishwa makongamamo na kila kitu ili kuweza kutoa elimu hiyo na elimu hiyo isitolewe na vyama. Mhe. Spika, kwa kulinda nini, isije ikatolewa elimu iliyokuwa sio sahihi.

Mhe. Spika, suala hili la kuingia katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa halitampunguzia mtu cheo chake, wala halitampunguzia mtu uluwa wake. Kwa sababu mimi Mhe. Spika, sio waziri, lakini mbona naishi kama waziri. Navuta *oxygen* kama anayovuta waziri, wala sikatazwi *oxygen* kuvuta kwa sababu waziri hajapata siku ile. Kwa hivyo, sisi wasi wasi wetu hasa ni nini, *lunch* atakayopewa waziri inawezekana mimi nakula nzuri zaidi, kwa sababu yeye atakuwa kazongwa na simu hawezi hata kula.

Kwa hivyo, mimi nahisi ile ni hofu iliyojengeka kwamba mimi nitakosa hiki na kile. Lakini naomba tufahamu kitu kimoja, tuko karibu sana na neema, lakini tukifanya masihara basi tutakuwa mbali sana.

Mfano Mhe. Spika, mpe utakavyompa SMZ. Mpe utakavyompa Mhe. Waziri mshahara, tukichimba mafuta atahiyari akae nyumbani asipewe uwaziri, kwa sababu kile atakachokipata katika pato la nchi atakaa ale na familia yake vizuri. Tukiichelewesha sera kwa sababu ya ugomvi tukapiga tena miaka 15 haijapita sera ya uchimbaji wa mafuta kwa sababu ya migogoro ndani ya nchi.

Mhe. Spika, juzi hapa tumeambiwa kukosekana kwa umeme mapato yameshuka kwa kiwango kikubwa, theluthi nzima katuambia Mhe. Waziri pale. Sasa ni tatizo moja tu hilo, sikuambii Mhe. Spika, tuingie katika mdorongo wa matatizo.

Mhe. Spika, mimi nawaomba sana wale wenye wasi wasi wauondowe wasi wasi kabisa, kwa sababu wao kabla ya uwakilishi wao walikuwa wanakula na sasa ni mwakilishi unakula vile vile. Mimi nahisi ukipewa uongozi unazidi wasi wasi kuliko ukiwa wewe si kiongozi.

Jengine Mhe. Spika, napenda nizungumze kuhusiana na mustakabali wa nchi. Jamani tuko nyuma sana, tatizo letu ni kwamba hatufanyi tathmini. Tukitizama elimu yetu inayotolewa ni duni, si stahiki yetu kupata elimu hii na kadiri tunavyokwenda, haidhuru Mhe. Waziri, anajitahidi kuweka vyyo vikuu na kadhalika, lakini wataalamu hawakai, kwa sababu hamna mustakabali mzuri katika nchi. Lazima tujenge mustakabali mzuri katika nchi ili tuwaweke wataalamu wetu wabaki hapa.

Mhe. Spika, vyyo vyetu viweze kuwa na wasomeshaji na maskuli yetu. Leo angalia Mhe. Spika, kunatakiwa milioni 400 za kuondoa mafunza ya embe, serikali haina. Sasa wajibu wetu uko wapi. Kwa hivyo, mimi nahisi kwamba ili tuweze kupata mustakabali mzuri katika nchi yetu, hususan ni kwamba dunia nzima ina mwelekeo wa kwenda katika kukubaliana yaani *reconciliation* na sisi tutaonekana watu wa ajabu sana kabisa, hali ya ucheshi wetu, hali ya ukarimu wetu na hali ya udogo wetu tukawa sisi tumeshindwa kukubaliana. Mimi nitatoa mifano miwili Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Lakini na muda unakimbia kidogo, jitahidi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Haya ahsante. Hii ni hali ninayosema ya kutokubaliana. Ntoa mifano miwili tu nistahamilie Mhe. Spika.

Juzi mimi nilikuwa nikisikiliza habari na nilisoma vile vile katika *internet*. Wanawake wanaotoka Zimbabwe kuelekea Afrika ya Kusini, kwa sababu ya kutoelewana kwao kule, basi wanabakwa njiani hawafiki. Hayo ndio matokeo ya kutoelewana, wanakimbia na matokeo yake kule wanakokwenda hawafiki wanabakwa njiani na kwa hivyo usalama wao ni mdogo sana.

La pili, nililosikia mwenyewe kutoka kwa mfanyakazi wa Umoja wa Mataifa aliyeko Yemen, anasema wananchi wanaotokea Somalia wanaelekea Yemen kwa ajili ya kutafuta hifadhi. Mhe. Spika, naomba jambo hili la kushangaza na kusikitisha tulisikilize vizuri, jinsi gani watu wanafikia ule utu wao kuuondoa iwapo hawakukubaliana.

Mhe. Spika, kulikuwa kuna kikundi cha wanawake kama 10 wa Kisomali, ambao walikwenda Yemen kutafuta ukimbizi, kuna vitambulisho viwili. Kitambulisho cha kwanza kinakuweka kambini na kitambulisho chengine unaruhusiwa kwenda mjini na kutafuta kazi. Wale wanawake wakapewa kile cha mjini kwa madai yao, baada ya muda kidogo mji ukawashinda, wakaja kwenye ile Afisi ya Umoja wa Mataifa iliopo pale Yemen, wakasema sisi tumeshindwa na mji tunataka twende huko kambini. Wakaambiwa njooni siku nyengine, kwa sababu lazima sisi tuulizie kama hiyo kambini ina nafasi au haina.

Basi najikinga na Mwenyezi Mungu na suala hilo lililotokezea. Walizipapatua nguo zote, wakakaa kama walivyojaliwa, halafu wakasema mna uwamuzi sasa kutupeleka kambini au kutuuwa hapa hapa, hali ya kuwa wako hivyo hivyo walivyo. Sasa yale ni madhila ya ile nchi yao kutosikilizana ndio wamefikia hali hiyo. Naamini Mwenyezi Mungu atatupokelea dua zetu, naomba nimalizie hapa Mhe. Spika, ahsante sana naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamuita Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, naomba nitowe taarifa tu kwamba maombi niliyopata ya kutaka kuchangia ni 36, tuliochangia hadi sasa ni 11 maana yake bado wajumbe 25. Mkutano huu ulipangwa umalizike kesho jioni Mwenyezi Mungu akipenda. Shughuli zetu zilioko mbele yetu ukiachia hii ziko mbili ndogo.

Moja Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Baraza wa pili yule na hatimaye kusikiliza hotuba ya Mhe. Waziri Kiongozi. Sasa muda umetukwaza kweli kweli. Ningependa nitilie mkazo kanuni kwamba tujitahidi ni vigumu kidogo, tusirudie rudie yale mazungumzo tunayochangia hapa. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, tujitahidi tubane muda na kwa maana hiyo tujaribu kwenda kwenye *point* tunayokusudia kusema moja kwa moja ili kutoa wasaa mkubwa zaidi kwa waheshimiwa wengine. Mimi ningependa wote tuchangie, lakini muda kwa namna tunavyokwenda itakuwa haiwezekani. Basi nasisitiza

kwamba kwa mujibu wa kanuni tusirudie rudie sana, twende kwenye *point*, tupange taarifa zetu vizuri au dondoo zetu vizuri, ili tuhakikishe kwamba tunatumia muda mfupi lakini tunapata michango mingi na Waheshimiwa Wajumbe wengi tunaweza kuchangia.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Spika, mimi nina taarifa, lakini kwa njia ya ushauri kama itawezekana kwa kiti chako au afisi yako. Ushauri wangu ni kutokana na wajumbe wengi wanapenda kuchangia na kutoa mawazo yao, basi mimi nilikuwa nashauri kwamba kesho asubuhi kipindi cha maswali na majibu tukiondowe.

Mhe. Spika: Sio ushauri mbaya, ni katika mambo ambayo Spika huwa yako katika uwezo wake na kuweza kuelekeza hivyo, ingawa na maswali ni mengi sana Waheshimiwa Wajumbe, lakini tutaangalia hiyo. Maana hata nusu ya yale maswali ambayo tunatakiwa tuyajibu nadhani hatujafika. Tutaangalia, lakini tuchanganye yote hayo pamoja na ushauri ambao umetolewa ili tuweze kutumia muda mchache zaidi. Nimuomba sasa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mhe. Dadi Faki Dadi na baadaye tumsikilize Mhe. Zakiya Omar Juma.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba: Mhe. Spika, na mimi nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataalla kwa kutujaalia tukakutana hapa katika jambo zito la nchi yetu hii. Lakini *Inshaallah* kwa inavyoonekana Mwenyezi Mungu atayatia kwenye wepesi *Inshaallah*.

Mhe. Spika, kama ulivyosema kwamba unatuomba twende kwenye hoja moja kwa moja. Sasa na mimi naomba niende kwenye hoja. Kabla ya hilo naomba nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa busara ambazo amezitumia kusamehe, hii ni hekima na maneno haya yapo katika kitabu. “Mbora wenu ni yule ambaye tumempa hekima” ndio Mwenyezi Mungu alivyosema hivyo. Kwa hivyo, aendeleo na hekima hizo na ustahamilivu pale ambapo ataudhiwa, kwa sababu kila mja ana maarifa yake.

Pia, niipongeze kamati ya makatibu wakuu ya CCM na CUF, kwa jambo hili ambalo wao walishalikubali na sisi kwenye Chama cha Mapinduzi tulilikubali tukatoa maelekezo, lakini shetani aliingia hapo katikati na leo *Alhamdulillah* limekuja. Nianze basi kuchangia.

Mhe. Spika, katika kusoma waraka huu wa Mhe. Abubakar Khamis Bakary, nimegundua mambo kama 7 ambayo naweza nikayalinganisha na waraka wetu wa Chama cha Mapinduzi. Sasa naomba niende moja kwa moja. Jambo la mwanzo ambalo nimeliona liko kila upande ni serikali ya umoja wa kitaifa. Sasa hilo mimi naliunga mkono. La pili, ambalo ni kuwa turudi kwa wananchi

tuwaulize wanasema nini kuhusu hili. Butiama tulisema hivyo na waraka wa Mhe. Abubakar Khamis Bakary, unasema hivyo na hili naliunga mkono.

Kitu kingine cha tano kidogo kuna hitilafu hapa. Lakini ukiliangalia kuna lugha tu hapa ambayo imechezeshwa, maana watu wa lugha hawa, hasa kwa yeye ni mwanasheria ni lugha tu. Mimi naunga mkono kwamba tuwe na Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais. Kwa muundo ule ule kwamba Makamu wa Kwanza wa Rais atoke katika chama ambacho ni cha pili kwa kura za Urais.

Halafu Makamu wa pili wa Urais atokane na chama ambacho Rais aliyeshinda ndipo anapotokea na sababu hii pamoja na kuwa tutakuwa na serikali shirikishi, lakini tulipokwenda kwenye uchaguzi kila mmoja alikuwa na ilani yake. Lakini serikali kwa bahati nzuri wote kwa pamoja tunasimamia ilani ya chama ambacho kimeshinda. Hii itamsaidia huyu mtu wa pili kuwa msimamiaji wa ilani ya uchaguzi wa hicho chama ambacho kimeshinda.

Jambo la sita ambalo naliona katika waraka wa Mhe. Abubakar Khamis Bakary, ni uteuzi wa mawaziri, kila upande upo isipokuwa tumetofautiana vipi wapatikane mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Abubakar Khamis Bakary, alishauri kwamba tuwe na mawaziri ambao wanatokana na uwiano wa kura za wagombea wa Urais, yaani chama kilichopata kura nambari moja na chama kilichopata kura nambari mbili, hapo ndani tuangalie.

Mhe. Spika, suala hili kama walivyokwisha kusema wengine kwamba litatuletea matatizo, vyenginevyo katika kifungu cha katiba ambavyo nitakuja kuvisema baadaye havitajwi tena, kwa sababu huwezi kuwa waziri mpaka uwe Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Sasa kwa muundo huu ambao ametuelekeza na bahati nzuri ametutajia vifungu ambavyo vitafanyiwa mabadiliko hawezi kuingia. Kwa hivyo, hapa namuomba na yeye aondowe hoja yake hiyo ili aweze kukubaliana na haya mawazo ya Butiama ambayo yeye ni mawazo yake.

Kifungu kingine ambacho ni kipya hiki, kuna uteuzi wa ma-RC na ma-DC. Kwa hapa nakuwa mgumu kidogo, siwi mgumu kwa sababu ya huo ukuu wa mkoa, hapana. Kwa sababu haya yatakuja baada ya uchaguzi. Sasa Rais atakayekuja atafanya hivyo atakavyoona yeye mwenyewe. Kwa hivyo, nasema kwamba suala hili tumuachie Rais ateuwe Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya anaotaka yeye, hakuna Rais yeyote ambaye atateua watu ambao wanapenda kuvunja amani, hasa ukiangalia ule mustakabali wa kule juu ulivyo. Kwa hivyo, hili nashauri kwamba tumuachie mwenyewe achaguwe watu ambao ataona yeye wanafaa. Kwa sababu hata viongozi siku zote hawafanyikazi kwa matakwa yao, kweli nafsi nayo inamvuto wa aina yake,

lakini kiongozi aliye bora anafuata kanuni, katiba na maelekezo. Kwa hivyo, nina hakika kwamba hata tukimuachia Rais kuna katiba ambayo inawaelekeza na kuna sheria ambazo zinawaelekeza.

Mhe. Spika, sasa nije katika vifungu 9 ambavyo waraka wa Mhe. Abubakar Khamis umetushauri.

Lifanye marekebisho ya vifungu vya Baraza la Wawakilishi, anatuomba kwamba liangalie na kukubali na kutoa mapendekezo kwa serikali mambo yafuatayo:-

- i. Lifanye marekebisho ya vifungu 9(3), kifungu hiki kinaeleza namna ya Serikali ya Zanzibar ilivyo, serikali ya umoja kwenye maendeleo na demokrasia. Sasa kuna mambo 4 misingi ya mapinduzi yapo hapa ameyaelekeza, naomba haya tusiyaingize tena kwenye katiba. Kifungu hiki kibakie pale kwa madhumuni ya kuendeleza demokrasia tu, tumalizie pale.
- ii. Baraza litamke kwamba muundo wa Serikali ya Zanzibar uwe ni wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayohusisha vyama vyote vya siasa vilivyomo katika Baraza la Wawakilishi na kwamba viongozi wa serikali watokane na uwiano wa kura za Rais katika uchaguzi mkuu.
- iii. Litamke kwamba Serikali hiyo ya Umoja wa Kitaifa itakayoundwa itaendelea kuheshimu na kuthamini misingi mikuu ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964 kama ilivyotangazwa na Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume hapo tarehe 8 Machi, 1964.

Mhe. Spika, kifungu hiki na mimi naungana nacho mkono, kwamba hayo marekebisho yetu ya sheria yaendeleo kuheshimu misingi ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar. Sio jambo baya, ni jambo zuri sana, kwa sababu tutakuwa tunayatunza Mapinduzi yetu.

- iv. Liweke utaratibu utakaowawezesha wananchi wa Zanzibar kushiriki kwa njia ya moja kwa moja kutoa ridhaa yao kuunga mkono mfumo huo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa njia ya kura ya maoni, yaani *referendum* na kwamba kura hiyo ya maoni iwe imeandaliwa na kufanyika si zaidi ya mwezi Mei 2010, au liweke utaratibu mwengine kwa njia ambayo Wazanzibari

wenyewe kwa kupitia wawakilishi wao waliowachagua wataona inafaa.

Hapana. Maoni yangu mimi, naomba twende kwa wananchi moja kwa moja. Ninavyowajua wananchi wa Zanzibar wapenda amani na maendeleo, basi hili watalikubali wala hatuna haja ya kujitia hofu, watakubali tu. Mwanadamu yeyote aliyekamilika hapendi fujo. Kwa maana hiyo, basi wala hatuna sababu ya kuweka muda wa mwezi wa tano. Maana hapa tuta-*commit* serikali halafu yatakuja kutokea matatizo mengine. Ilimradi tu sisi tutamke kwamba mambo haya yafanywe kabla ya uchaguzi. Kwa hivyo, itakuwa serikali tumeshaiwekea *limit*, kwamba hivyo mtakavyo kwenda vyovyote, lakini kabla ya uchaguzi suala hili iwe limekamilika.

- v. Baraza liigize serikali ndani siku saba kuandaa na kuufikisha mbele ya Baraza hili tukufu mswada wa marekebisho ya sheria ya uchaguzi ya Zanzibar (Nam. 11 ya 1984) kwa madhumu ya kuweka utaratibu, masharti na namna ya uendeshaji wa kura ya maoni na pia kuipa mamlaka Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, mbali ya majukumu yake iliyo nayo sasa, pia kusimamia na kuendesha kura ya maoni kwa yale masuala mazito yanayohitaji maamuzi ya wananchi moja kwa moja.

Mhe. Spika, na hapa hivyo hivyo, naomba Mhe. Abubakar Khamis Bakary, kwa sasa na kwa sababu Mhe. Rais wa Zanzibar anatambulika na wananchi wote na chama chenu kimentambua, basi tuendelee kumuamini Rais na serikali yake, hatuna sababu ya kuweka siku saba. Tuiache serikali ifanye kazi zake, nina hakika utakubali.

Jambo la sita iagize serikali kufanya mawasiliano na nchi rafiki. Tuiambie serikali kwamba jambo hili watafute fedha za kulifanikisha, wala hatuna sababu ya kujivua nguo. Tujifunike hivyo hivyo serikali itajua mbinu zake, namna gani serikali itafute fedha kwa jambo ambalo limependekeswa na Baraza la Wawakilishi.

Saba ni pale itakaporidhiwa hoja hii, basi lilitake vyama vyote vya siasa vyenye Wajumbe katika Baraza la Wawakilishi kujikubalisha kuunga mkono hoja itakayopelekwa kwa wananchi na kuwaomba kuidhinishwa uanzishaji wa mfumo wa Serikali ya Umoja ya Kitaifa. Hiyo ndio kura ya maoni yenyewe.

Sasa tuviachie vyama, tusijipe kazi sisi hapa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Ninadhani wote hapa tunatokana na vyama. Sasa kama chama kitakupangia wewe nenda katika jimbo lako la Magogoni ukakutane na watu wako kwamba basi, lakini sisi kama Baraza la Wawakilishi tusijipe hili jukumu, tuache kwa vyama vyenyewe.

Jambo la nane, chini ya Kanuni ya 48 (6) ya Baraza na 73 (3) lijadili rasimu ya Mswada wa marekebisho ya Katiba ya Zanzibar kwa vifungu vinavyohusika ambavyo kwao vimeambatanishwa na hoja hii na ambavyo ni sehemu ya hoja. Ndio vile ambavyo nimeviisema mwanzo kwamba, vile vifungu kwanza ni lazima kwa sababu kifungu cha 39 cha Katiba ya Zanzibar kinazungumza nafasi ya Waziri Kiongozi.

Kwa hivyo, kwa vyovyote kama jambo hili wananchi watalikubali, hii nafasi itakuwa haipo tena. Kwa hivyo, *automatically* tutakwenda kufanya marekebisho. Kifungu cha 42 kinazungumzia muundo wa wizara. Ninadhani kama nilivyochangia kwamba mawaziri watokane na viti vya humu ndani ya Baraza la Wawakilishi. Chama ambacho kimepata viti kwa mujibu wa uwiano bila shaka wataalamu watajua kwamba sasa chama hiki kiwe na mawaziri kiasi kadhaa, labda kwa sababu naye ni mwanadamu huyu Rais anaweza akaona kwamba ateuwe watu ambao sijui kama atafanya hivyo kwa sababu serikali ikilaumiwa yeye ndiye atakayelaumiwa. Labda tuweke nafasi ya kupata maoni kutoka kwa vyama husika na sidhani pia tutakuwa tumembana.

Wawakilishi wakishaingia hapa, watu wapeleke CV zao huko tumuachie Rais ateuwe. Maana pia ile kumwambia lazima ateuwe huyu na huyu, pia ni kumbana katika muundo fulani.

Neno la tisa ambalo Mhe. Abubakar Khamis Bakary, amelipendekeza Baraza liunde kamati ya wajumbe sita; watatu kutoka upande wa serikali na watatu kutoka upande wa upinzani, kwa madhumuni ya kusimamia hatua zote zinazopendekezwa na hoja hii hadi kukamilika kwake kama ilivyo katika ratiba ambayo ni sehemu ya hoja hii.

Hapa sishauri kwamba tuunde tena kamati. Unajua mijadala hii tena umesema kutoka upande wa serikali na upande wa upinzani. Ninadhani kwa sababu ya kuwa chama cha CUF kimeshatamka hadharani kwamba serikali hii inaitambua kwamba ni serikali halali na Mhe. Amani Abeid Karume amefanya mambo mengi. Pia, tuiachie serikali. Sisi tuwaambie hivi kwamba jambo hili, serikali tunawaomba kwamba lisifike kwenye uchaguzi liwe limeshakamilika.

Mhe. Spika, kwa kuwa hoja hii inavyojionesha kwamba watu ni kuzunguka tu. Mzunguko wa binadamu kila mmoja ana akili zake katika kichwa, lakini

asilimia kubwa ya wanaosimama hoja wanaoiunga mkono. Ni kidogo sana ambao wanasema vyengine, nani hataki umoja. Labda nikwambieni kwamba sisi ambao tupo Mikoani, shughuli hizi za utulivu wa watu ndio kazi yetu.

Sasa ikija hoja kama hii leo kwamba sasa watulie kwa pamoja, washirikiane, kama *TASAF*, hongera *TASAF*, tulikuwa hatujafika hapa. Ndio nikasema hoja hii ikenda kwa wananchi hawaikatai *unless* watoke watu waende wakatie maneno, lakini kama wataachiwa wenyewe wamalize. Sisi tuna mifano ya *TASAF* hasa Pemba, watu walikuwa hawapo vizuri, lakini imekuja *TASAF* watu wanajenga madarasa ya skuli pahali pamoja, wanajenga zahanati pahala pamoja, Hivyo, wapo hivi kwenye maendeleo. Je, hili?

Kwa maelezo hayo Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, na mimi niseme kwamba hoja baada ya kufanyiwa marekebisho ya vifungu ambavyo nimevisema, ninaiunga mkono.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mkuu wa Mkoa kwa maelezo yako na mchango wako huo. Sasa tumsikilize Mhe. Zakiya Omar Juma na baadae tumsikilize Mhe. Thuwaibah Edington Kissasi.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuniona na kunipa nafasi angalau na mimi niweze kutoa mawazo yangu kuhusiana na hoja muhimu ambayo ipo mbele yetu.

Mhe. Spika, ninataka nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku ya leo ikawa imefika na tukawasilishiwa hoja hii mbele yetu na tukaweza kutoa maoni na mawazo yetu. Lakini pia, Mhe. Spika, nishukuru kwamba hii hoja pamoja na kwamba Mhe. Abubakar Khamis Bakary, ameiwasilisha na ninamshukuru sana kwa hilo, kwamba na wenzetu wanasema kuwa ni hoja yao. Kwa hivyo, kama alivyomalizia mwenzangu ninadhani hakuna ambaye haiungi mkono.

Sasa nitangulie kwa kusema kwamba ninaiunga hoja hii mkono asilimia mia kwa mia. Lakini pia, tutazame leo Mhe. Spika, kwa nini tupo hapa. Mimi ni mgeni sana wa mambo ya hoja kwa sababu hoja nyingi, kwa sababu nilikuwa nikisikia tu kuna hoja binafsi, lakini hazijawahi kupita, leo ni mara ya kwanza tunajadili hoja, ninashukuru sana kwa hili.

Sasa kwa nini tupo hapa, ndio hicho kilichotuleta kujadili hoja hii kutokana na mustakabali wa nchi yetu ambayo chanzo na kiini kama wenzangu wengi waliotangulia kuzungumza ni maridhiano ambayo yamepatikana kwa kukutana kwa Mhe. Rais wa Zanzibar Mhe. Dr. Amani Abeid Karume na Maalim Seif Sharif Hamad, wakiwa wao ndio viongozi wakuu wa siasa katika nchi hii.

Ni jambo muhimu sana na tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kulifikisha suala hili viongozi hawa kwa kukutana. Ni jambo ambalo kwa kweli lilikuwa linatazamiwa muda mrefu, lakini kama wengine walivyotangulia kusema kwamba linakwenda kwa muda na muda sasa umefikiwa.

Mhe. Spika, wengi watu pengine wanajiuliza na kutaka kujua kwamba kwenye maridhiano hayo kuna nini, lakini mimi binafsi sioni sababu na wala sina haja ya kutaka kujua nini kimezungumzwa, maadamu tu nimeelewa lengo na madhumuni ya maridhiano yaliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, kama nimefahamu sawa sawa, maridhiano yale yamelenga kuitoa nchi yetu katika misugvano ya kisiasa na siasa za chuki na hasama ambazo zimeendelea kwa muda na kama ilivyoenezwa na mengine sitaki kurudia, kwamba kulikuwa na historia tangu huko nyuma ya mambo hayo ambayo chanzo chake huwa kinatokana na chaguzi ambazo zilikuwa hazipati ridhaa.

Mhe. Spika, kutokana na hili, basi ninampongeza sana Mhe. Rais pamoja na Mheshimiwa Katibu Mkuu wa Chama chetu kwa kuona kwamba kuona haja ya kufikia hilo lengo. Kama tunavyozungumza mambo haya yanakwenda kwa kupata na kukosa. Hivyo, wakafikia pahala wakasameheana wakakubaliana kusamehe ya nyuma, lakini kwa kutizama mbele kwa mustakabali wa nchi yetu, sidhani kama walitazama maslahi yao binafsi kwa sababu wote wawili ukiwatizama umri wao na hali halisi ya maisha tunavyokwenda, basi chochote kizuri kinachokuja mbele yetu, basi wao wameweza wakawa ni mashahidi wa kushuhudia, lakini pengine hata hawatofikia kuyaona na sio wao pengine hata mimi ninaweza kutangulia.

Mhe. Spika, sote tuliopo hapa tumepitia na tumeona hasara na shida ya kutengana, lakini pia kipindi hiki kifupi tumeona faida na raha ya kuwa pamoja. Mhe. Mugheiry, amezungumza mambo mengi na kabla yake Mhe. Waziri wa Elimu na yeye ameyaeleza yake ya kutosha ya kuthibitisha maneno haya.

Sasa hii peke yake ni kuonesha ni jinsi gani, sio viongozi tu lakini hata wananchi kwamba wamechoshwa na ile hali ambayo tumeizoea na inatokea katika nchi kila baada ya miaka minne mitano inajirudia. Sasa kama alivyotangulia kusema Mhe. Omar, kwamba wenzetu wameshanawa mikono katika hili, lakini hivi sasa jamii nzima ya Wazanzibari walioko ndani na nje ya nchi pamoja na wahisani na marafiki na Jumuiya za kimataifa wanasikiliza nini Wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar watafikia katika kuliendeleza suala hili na kulipa nafasi yake, na kutuweka katika hali ambayo tutakuwa tuna siasa za kutofautiana kwa mawazo kama alivyozungumza Mheshimiwa mmoja hapa.

Tunatofautiana kwa mawazo na fikra, lakini tunafika pahala tunaingia kwenye chaguzi anayeshinda anaridhika kashinda na anayeshindwa halikadhalika anakubali kuwa nimeshindwa, wanapeana mikono, tunarudi pahala pamoja na kufanya kazi kwa pamoja ya kuleta maendeleo katika nchi yetu kwa mustakabali wa nchi yetu na nchi kwa jumla kujiletea maendeleo ya kisiasa na kiuchumi.

Mhe. Spika, kuna msemo maarufu wa kisiasa unaosema kwamba siasa haina adui wa kudumu wala haina rafiki wa kudumu. Sasa hii inategemea mazingira na inategemea haja na wakati ule ambao ni muafaka. Kama walivyozungumza wenzangu Mhe. Spika, sitaki niyarejee, lakini Mhe. Fatma, alikuwa yupo nje ya nchi, siku ya tarehe 5 baada ya mazungumzo tarehe 7 kulikuwa na mkutano na ikatoka kauli ya kuitambua serikali, kweli mfadhaiko ulikuwepo, lakini kwa sababu ya sentensi hii maarufu ya kisiasa, kwamba unafika wakati siasa zinabadilika. Sio kwa sababu mtu kashindwa, sote ni washindi katika hili, kama kulikuwa kuna makosa sote tumefanya makosa hayo.

Sasa haya sio mambo ambayo tumekusudia kuja kujadili hapa, lakini tumekusudia kwenda mbele na sio kurudi nyuma kutizama yale makosa, makosa yamepita tumesamehena, tumeomba dua mbili kubwa katika Ijumaa mbili zilizopita na tumeiombea nchi yetu pamoja na sisi wenyewe. Kwa hivyo, *inshaalla* Mwenyezi Mungu atakuwa anatuongoza huko badala ya kuturudisha nyuma.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nilikuwa ninataka nisemee zaidi suala hili ambalo tunalijadili hapa mbele yetu na kwamba sote tuwe kitu kimoja. Sitaki niwaambie watu wote wawe kama mimi, lakini mimi binafsi katika kujadili masuala kama haya, huongozwa zaidi na utashi wa kizalendo, yaani ninakuwa Mzanzibari kwanza halafu ndio kinafuata chama changu.

Haya si mageni kwetu sisi Mhe. Spika. Kabla ya kumtambua Rais Karume tarehe 7 ya mwezi wa Novemba, tulifanya jambo moja ambalo wewe Mhe. Spika, ni shahidi pamoja na maafisa wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, Waziri na Naibu Waziri na Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu, tulipitisha bajeti ya mwaka 2008/2009 ya Mhe. Mansour, asilimia mia kwa mia, tulinyanyua mkono sote hata Rais hajatambuliwa.

Ni kinyume pengine na utaratibu wa misimamo ya chama, tulikuwa hatujamtambua Rais, hatujaitambua serikali, lakini ni kwa nini tulifanya vile? Kwa sababu tuliweka maslahi ya nchi mbele, mambo mengine yakafuata nyuma. Kwa hivyo, ninadhani vyovyote tutakavyokuwa tunafanya kwa mustakabali wa nchi hii, basi Uzanzibari unakuwa ni nambari wani, halafu

itikadi ikiwa ni CUF au CCM, ikiwa huna chama, ikiwa una chama chochote chengine itakuwa nambari mbili, kwa sababu nchi ni yetu sote, wala hakuna mtu atakayesema ni yake au ana hati miliki katika hii nchi.

Kwa hivyo, muhimu zaidi tunapokuwa viongozi kwa mlango wowote tuliopitia, basi ukishafika huku ndani, suala linalokuja mbele yetu, likihusu jamii kwa jumla basi Uanzibari unatangulia.

Mhe. Spika, sipingi suala la kura ya maoni, ninaliunga mkono sana na ni utaratibu mzuri, lakini kura ya maoni kwa mawazo yangu, kwa sababu mimi kura ya maoni ninavyoiona ni sawa sawa na kura yoyote ya kawaida ambayo kwa mara ya tatu na keshokutwa tunaingia ya nne, bado haijaleta muskabali mzuri.

Wasi wasi wangu ni kwamba au pengine ushauri wangu ni kwamba tutakapoingia katika kura ya maoni tujiandae vizuri na tuweke utaratibu mzuri ili lile ambalo tunakusudia, kupitia hiyo kura ya maoni liweze kuwa na ridhaa, isije ikatokea mizozo na tofauti.

Lakini pia, Mhe. Spika, huwa zinatumika na silaha kubwa ni umoja na mshikamano. Tunalia na kero za muungano siku zote. Mhe. Waziri Kiongozi, yupo hapa, yeye ni wakala wetu katika vikao na Waziri Mkuu juu ya masuala haya, lakini siku tuliosimama kidete hamna CUF, hamna CCM, tukasema leo hapa suala la mafuta ni suala la Wanzibari, hatukutafuta kura ya maoni. Suala lile limepita. Mhe. Waziri, juzi kalitangaza rasmi kwamba hili suala limeondoshwa katika orodha ya mambo ya muungano.

Kwa hivyo, sipingi suala la kura ya maoni, lakini ninasema inapotokezea haja ya muhimu, haja ya kujenga basi na hekma inatumika na si kwa njia nyengine yoyote, isipokuwa tunafanya ule umoja wa kutanguliza maslahi ya nchi na tukashikama na tukawa sote tuna sauti moja. Basi Mhe. Spika, kama wengine walivyotangulia kusema ni kwamba hakuna kinachoshindikana ambacho kipo juu kama mwenzangu mmoja alivyotangulia kusema, yaani ndani ya dunia hii.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nikiondoka katika suala hilo la maelezo ya pamoja, ninataka niingie katika hoja sasa na labda ninukuu kidogo baadhi ya vipengele. Hoja inasema katika kipengee cha 2, kinasema kwamba katika uchaguzi wa Zanzibar mara zote umeambatana na hali ya mivutano mikubwa ya kisiasa ambayo mara nyingi imepelekea kugawanyika kwa jamii ya Wanzibari na hivyo kuathiri maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Kipengele cha pili kutoka mwisho kinasema, “Wanzibari kwa ujumla wao bila ya kujali itikadi zao za kisiasa na kupitia taasisi zao mbali mbali,

Wameonekana kuuunga mkono na kufurahia hatua ya matokeo ya viongozi wao wawili kukutana. Na kwa kuwa Jumuiya za kimataifa kupitia kauli za nchi zao zimetangaza kuwapongeza viongozi hao kwa hatua kubwa ya kihistoria waliyoichukua na kutaka kuwaunga mkono katika juhudi hizo, huku zikiahidi kutoa msukumo wa misaada zaidi katika kuisaidi nchi ya Zanzibar ipige hatua kubwa zaidi za maendeleo”.

Na kwa kuwa kuna haja ya kuinusuru Zanzibar yetu na Wazanzibari wote kuungana kwa pamoja bila ya kujali vyama vyao, itikadi zao, kabila zao, dini na kadhalika.

Hapa Mhe. Spika, tunaona ni jinsi gani kwamba hizi zote zimelenga kuwa tuangalie zaidi maslahi ya nchi. Mhe. Spika, amesema Mhe. Rashid, hapa kuwa tunakuwa na choyo, ukipanda boti ukishuka tu pale Dar-es-Salaam, kule siasa zipo kama hapa kwetu na vyama ni hivi hivi vya Kitanzania ambavyo sote tumekuwa tuna vyama vya kitaifa pamoja na wao, lakini unaona ni jinsi gani wenzetu wanavyopiga hatua. Ukenda mwezi tu au miezi miwili ukenda Dar-es-Salaam, tena usije ukapotea zaidi, ukenda Arusha na Mwanza huko ndio hakusemeki Mhe. Spika, unaweza ukafikiri labda upo Ulaya.

Sasa hili ni jambo ambalo linatulazimisha na linatusononesha katika nyoyo zetu, kuona kwa nini sisi, Mhe. Fatma, katoa mifano na vigezo vingi tu kuhusiana na nchi ya Singapore. Nchi hii ina ma-*group* mengi sana, lakini bado wamefika pahala utaifa wao ndio umetangulia, hawasemi chama chetu, kabila letu au kitu gani. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa naona hilo ni suala la kusisitiza zaidi kuliko kusema tuingie katika itikadi hata Mhe. Rais Abeid Amani Karume, angelisema nikashauri vikao vya chama kama nikutane naye au nisikutane naye, mpaka leo kusingekuwa na maridhiano, kwa sababu tuna itikadi.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kuingia katika marekebisho ili wapate na wenzangu nafasi ya kusema chochote.

Mhe. Spika: Muda unakimbia sana.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Na mimi Mhe. Spika, nitajitahidi kwenda mbio kama gari. Kuhusu na marekebisho kama yalivyotendeka katika ukurasa wa 6, na mimi nilikuwa ninashawishika na kifungu hiki cha 9(3) na haya mambo ambayo yameorodheshwa ya (a), (b), (c), (d) na (f). Kwa kweli mengine yanaonekana yamepitwa na wakati kidogo. Kwa hivyo, nilikuwa na mimi ninashawishika kidogo kufanywe marekebisho hapa yanaweza kufanywa.

Kwa kumalizia naomba kuungano mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Zakiya Omar Juma, kwa mchango wako huu. Ninafikiri kwa muda uliobakia tumpe Mhe. Thuwaiba Edington Kissasi.

Mhe. Thuwaiba Edington Kissasi: Ninakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuzungumza katika hoja hii nzito iliopo mbele yetu ambayo itapelekea kuweka mustakabali mzuri wa uongozi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, na mimi nimtangulize Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwa wazima na wenye afya njema tukaweza kufika hapa kutekeleza wajibu wetu huu.

Mhe. Spika, ninataka na mimi nianze kwa kusema kwamba kwa kuwa hoja hii kimsingi inatokana na chama changu cha Mapinduzi, basi ninasema sina wasi wasi nayo, kwa sababu ndani ya chama changu tumeliona mapema hili kwamba ni suala jema na zuri, lakini wenzetu kwa bahati Mwenyezi Mungu amewajaalia kulielewa hili kwa utaratibu mzuri zaidi na hatimaye, leo tarehe 28 Januari, 2010 Mhe. Spika, basi ni miaka miwili kasoro miezi miwili tu tokea tuliposema rasmi kule Butiama kwamba suala hili liende kwa wananchi.

Mhe. Spika, ni kawaida kuwa binadamu sote hatupo sawa sawa, wengine wana ufahamu wa haraka, wengine wanaufahamu wa taratibu na wengine ufahamu wao kama huna subra basi unaweza ukatoa maneno ambayo labda yanaweza yakapelekea kutokueleweka.

Mimi ninataka nimpongeze Mhe. Rais wa Serikali yetu hii ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwamba ni kiongozi ambaye amekuwa na subra, ni kiongozi ambaye amekuwa mstahamilivu, ameweza kutulia akiwasubiri wenzetu wamuelewe, akisubiri wenzetu wafahamu na sisi akatuweka katika mstari huo, tukaweza kuwa wastahamilivu na kuwa na subra, na kumbe subra njema leo tumeiona nyota yake Mhe. Spika.

Sote tumekuwa wastahamilivu, sote tumekuwa na sisi tufuate hekma za Mhe. Rais. Basi leo bila ya kutarajia hapa wenzetu wamekuja na hoja ambayo kiini chake ni Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, hakuna sababu, mimi sioni kwa sababu tukisema vyenginevyo tutakuwa tunakwenda kinyume na yale ambayo tumeyataka wenyewe karibu miaka miwili iliyopita. Wenzetu wameelezwa leo, basi tuungane nao.

Mhe. Spika, kama walivyotangulia wenzetu ndani ya Baraza hili, suala hili kimsingi liende kwa wananchi basi tukubaliane hivyo. Lakini liende kwa namna gani. Mimi ninasema kwamba watakvayoshauri wao na ninaamini kama walivyoamini Waheshimiwa wengi humu, kwamba tukiwaelewesha visuri wananchi wetu hawana sababu za kulikataa, kwa sababu lengo letu sote ni hilo hilo la umoja na mshikamano na utulivu.

Sasa niseme basi vipengele vile ambavyo Waheshimiwa kutoka upande huu wametamka, mimi niungane naye kwa vipengele vile na kwa sababu ya muda sioni haja ya kuvipitia, lakini cha kwanza, cha pili na cha tatu kimsingi kwa kuwa vinatokana na kwetu tunakubaliana.

Lakini katika marekebisho ambayo wameyafanya wenzetu, kuanzia ushauri wao kwamba baada ya Urais, ile nafasi ambayo chama kinashinda afuate Waziri Kiongozi, sisi tukashauri hapana kwa sababu ni vyama viwili vitakuwa kwenye uongozi, kilichoshinda na kile kilichotokea cha pili, basi kuwe na Makamu wawili wa Rais.

Hii mantiki yake Mhe. Spika, ni kwamba kwa kuwa sera ni tofauti. Sera ya chama kitakachoshinda itakuwa tofauti na chama kilichoshindwa. Maana yake kama ingekuwa sera ni sawa sawa, basi kusingekuwa na haja ya kuwa na chama chengine. Wangukuja huku moja kwa moja. Lakini kwa kuwa wana sera zao, basi hakuna sababu ya kumueka kiongozi wa kukaa baada ya Rais atokane na chama ambacho sera zake haziendani.

Lakini kwa kuwa lengo ni maendeleo ya nchi hii tumesema, basi apewe Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini kwa ajili ya kumkaimu na kuendeleza sera za chama chake rais ambaye chama chake kimeshinda, basi kuwe na makamu wa rais ambaye atakuwa anashikilia nafasi zake na kuendeleza kazi zile. Hii yote Mhe. Spika, inachelea tofauti za sera, tofauti za misimamo, lakini wakati tunakwenda kwenye uchaguzi kunakuwa na ilani za vyama. Kwa hivyo, huyu makamu wa pili atakuwa anasimamia ilani ya chama chake kilichoshinda.

Tumekuwa na wasi wasi Mhe. Spika, kutokana uzoefu tulivyojifunza kutoka na wenzetu wa Zimbabwe, juzi tumesikia wengine Kenya wamerushiana viti, lakini tumuombe Mwenyezi Mungu tusifike huko. Tumuombe Mwenyezi Mungu atuelekeze katika njia ambayo tutakwenda vizuri, tutaelewana, *Inshaallah* kwa mtizamo wangu Mhe. Spika, nataka nione mbali kama alivyoona Mhe. Abass Juma Muhunzi.

Mhe. Spika, Mhe. Abass Juma Muhunzi, aliona mbali sana kipindi fulani, wenzake hawakumuelewa wakamuona ni msaliti mkubwa sana, lakini sasa

kumbe ndio hili tunalolijadili hapa leo. Mimi nataka nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Abass Juma Muhunzi kwa kuona mbali kiasi kile.

Sasa na mimi Mhe. Spika, nataka niseme hapa kwenye Baraza lako naona mbali, umbali wangu mimi Mhe. Spika, ni kwamba tunaelekea kwenye mfumo wa chama kimoja sasa. Historia inajirejea Mhe. Spika. Vyama vingi vilikuwepo huko nyuma tulikuwa tukisema ni historia, lakini kuanzia mwaka 1992/95 tukarudi kwenye vyama vingi. Sasa kwa hivi tunavyokwenda kwa sababu hatimaye kwa imani yangu na ufahamu wangu huyu Makamu wa Kwanza wa Rais akijikuta kumbe haachiwi mamlaka, akijikuta yupo yupo tu, basi hatimaye ataunga mkono sera za chama kile kilichoshinda. Na kama ataunga mkono sera hizo, basi ndio keshakuja huyo, mimi naona huko.

Siku moja *Inshaallah* kama sio hapa, lakini nitakumbukwa kwa kauli yangu hii kwamba tutaona aa, kwa nini tuwe na vyama vingi? Sote letu ni moja kujenga nchi yetu, tuwe na maelewano, tukuze watoto wetu, tukuze uchumi wetu, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie na mafuta yetu, sasa tunatofautiana nini. Kwanza siasa ni mchezo tu, wengi wamesema hapa, basi tuelekeze mchezo wetu kwenye chama kimoja ili tuelewane vizuri zaidi.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary, ame-*quote* kwenye *paper* yake kwamba tuache tofauti zetu za kisiasa na hili alilisema Mhe. Abass Juma Muhunzi, zamani sana, kwamba hebu na tuacheni hizi itikadi zetu za kisiasa tumuunge mkono Mhe. Rais, katika shughuli zake za maendeleo, ndio haya tunayofanya hapa leo.

Mhe. Spika, mimi sitaki nichukue muda mwingi sana, lakini niseme kwamba suala la mawaziri Mhe. Rais, sisi tumeshauri kwa upande wetu kutokana na viti vinavyotokana na majimbo, lakini pia, tumeshauri wengi wetu upande huu Mhe. Spika, basi suala la Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya aachiwe mwenyewe Mhe. Rais. Tumuamini Mhe. Rais, atakaposhinda, tumuamini madhali amechaguliwa huyu uwezo anao na washauri atakuwa anao, tusimpore madaraka yote tena tukawa sisi kazi yetu kumpangia, tumuachie mamlaka yake, tumuache awe na washauri wake, aunde serikali, awachague Wakuu wa Mikoa wake anaowaona kuwa watamsaidia kwenye kazi zake na Wakuu wa Wilaya.

Mhe. Spika, mimi nasema mengi yameshasemwa na kwa kuheshimu kanuni za kutorejea rejea, basi niseme kwamba kwa sababu narudia tena suala zima limetokana na sisi huku, wenzetu leo wamefahamu tunasema *Alhamdulillah* na Mwenyezi Mungu atawaongezea ufahamu huo na hatimaye tufikie katika

mfumo wa chama kimoja ndani ya nchi yetu ya utaifa mmoja, Uzanibari na umoja sio wa kitaifa, lakini ni umoja wa Kizanzibari. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Katika orodha wa shughuli za kesho na tukisema tupunguze muda wa mjadala kutoka dakika 20 zilizotajwa na Kanuni na kukubaliana na dakika 15. Kwa hivyo, tutamudu kusikiliza Waheshimiwa Wajumbe 12 tu kwa muda huo wa masaa matatu, yaani kuanzi saa 3:00 hadi 6:00.

Tukichukulia kwamba shughuli ya mjadala imalizike kwa kipindi cha asubuhi na majumuisho yafanyike jioni. Vile vile, jioni hiyo iende ile kazi ya kuchagua Mwenyekiti wa Baraza kabla sijamwita Mhe. Waziri Kiongozi, kwa ajili ya kuhitimisha shughuli zetu za Mkutano huu wa Kumi na Nane (18).

Kwa hiyo, nataka niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kwamba, kesho maswali na majibu hayatakuwepo na tutaanza saa 3:00 asubuhi kwa ajili ya mjadala huu. (*Makofi*)

Kutokana na hali hiyo, tukubali haki hiyo ya kuiuliza serikali kwa kesho tunaizuia kidogo, isipokuwa twende kwenye mjadala moja kwa moja. Vile vile, naomba kama mlivyofika leo na kuomba nitokee hata kabla ya wakati, nadhani tufanye hii kazi na kesho tuwe hivyo kwa kipindi cha asubuhi pamoja na jioni kwa jumla.

Lakini nataka niseme kwamba jambo hili tunalolifanya hapa ni suala kubwa sana. Mimi nimekuwa Spika tokea mwaka 1995 nimekuwa nikitafuta wasaa wa kufanyakazi pamoja tokea mwaka 1996. Nakumbuka Novemba mwaka 1996 nilikwenda na kuanza kuzungumza na Wawakilishi wangu wa upande wa Upinzani, basi waliwahi kuniuliza hivi wewe umetumwa na nani kazi hii, waliokuwepo kipindi kile wanakumbuka. Kwa kweli nilizungumza nao kutoka wilaya moja baada ya nyengine kwa muda wa siku nne, yaani tulikuwa tukikutana kuanzia saa 3:00 mpaka 7:00 au kuzidi.

Nia na madhumuni nilikuwa nikitafuta utaratibu wa utulivu na amani, ili tufanyekazi pamoja kwa maendeleo ya wananchi mwaka 1996. Waheshimiwa Wajumbe, nimekuwa nikifanya au nasema hivyo katika vikao karibu vyote. Mwisho kabla ya kikao hiki kwenye semina tuliyo kutana pale Tibirinzi nilikuwa nikizungumzia mambo haya ya kufanyakazi kwa pamoja, kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii na wananchi wake.

Mjadala unavyoendelea moja kati ya kazi kubwa ambayo haijaka vizuri ni muundo wa serikali, yaani huu mjadala wetu unaoendelea. Kwa hivyo,

tunakwenda kupumzika na tuzingatie hilo na kesho tukirudi tuweze kuendeleza mjadala wetu na tuone tunafika wapi, hatimaye kama kuwapelekea wananchi tunawapelekea nini.

Kwa machache hayo, basi tukubaliane kuahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 29/01/2010 saa 3:00 asubuhi. Tukiwa tunarudi kuzingatia mustakbali wa nchi yetu, ili kesho tumalize salama. Nakushukuruni sana.

*(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 29/01/2010
saa 3:00 asubuhi)*

